*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Sita – Tarehe 23 Machi, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):**

Taarifa ya Utendaji ya Mamlaka ya Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 *(The Annual Performance Evaluation Report for the Financial Year 2012/2013).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 53

**Mgogoro Kati ya Walimu Moshi Vijijini na Maafisa wa Halmashauri Moshi**.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA** aliuliza:-

Je, Serikali itatatua lini mgogoro wa muda mrefu kati ya Walimu wa Moshi Vijijini na Mafisa wa Halmashauri ya Moshi kuhusu maslahi yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mgogoro ulikuwepo katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, hususan mwaka 2012 ulitokana na madai mbali mbali ya Walimu kutoshughulikiwa ipasavyo.

Serikali wakati wowote inathamini sana kazi inayofanywa na Walimu na hivyo msisitizo umekuwa ukitolewa kwa maafisa elimu kutoa kipaumbele cha kuwahudumia Walimu kikamilifu.

Katika kusimamia hili, Serikali imekuwa inachukua hatua za kinidhamu kwa maafisa elimu ambao wamebainika kutotimiza wajibu wao ipasavyo ili kuimarisha utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, Serikali imesimamia ulipaji wa stahili mbalimbali za Walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, hadi mwezi wa Februari, 2015 jumla shilingi milioni 676.7 zimelipwa kwa Walimu 579 kwa ajili ya malimbikizo ya mishahara.

Pia shilingi milioni 645.8 zimelipwa kwa Walimu kwa ajili ya uhamisho, likizo, matibabu, gharama za mazishi na masomo.

Aidha Serikali imesimamia uendeshaaji wa vikao vya pamoja kati ya Walimu na Maafisa wa Chama cha Walimu Tanzania, Idara ya Utumishi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ili kutoa elimu kwa Walimu kuhusu stahili zao mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho kubadili utaratibu wa kuwahudumia Walimu kwa kuimarisha mfumo wa kushughulikia stahili zao, ili kuwa na chombo kimoja kitakachoshughulikia ajira, nidhamu na upandishaji madaraja. Kuundwa kwa chombo hiki, kutenga fedha za kutosha katika Bajeti na kuimarisha matumizi ya mfumo ya *Lawson* kutamaliza matatizo ya Walimu kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Naomba kujua wale maafisa elimu pale Moshi Vijijini, waliokuwa wanatesa walimu, wanasumbua walimu, wanawahangaisha walimu wakati wanapofika pale kudai haki zao.

Hao maafisa Elimu mliosema, mmewachukulia hatua za kinidhamu, ni akina nani waliowachukuliwa hizo hatua za kinidhamu na adhabu yao waliyopewa ni ipi ili turidhike kweli hawa watu wanaowatesa walimu, wanaowasumbua walimu siku zote wamechukuliwa hatua?

Pili, hapa Bungeni tumekuwa tunaomba hiki chombo kimoja cha kuratibu shughuli za walimu, matatizo ya walimu, naomba kujua zimefika wapi na kitaanza lini? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Augustine Lyatonga Mrema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ziko hatua mbalimbali za kinidhamu zimechukuliwa dhidi ya maafisa elimu ambao pia wamekuwa wakileta usumbufu na kutotoa huduma sahihi kwa walimu wetu.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa ametaka idadi ya maafisa elimu kwa majina lakini pia na adhabu zao, naomba uridhie baadaye nikuletee ili uweze kumfikishia Mheshimiwa Mbunge aweze kuona hatua kadhaa ambazo sisi tunazifanya kwa marekebisho na hatua hzi tumezifanya nchi nzima kwa wale ambao walikuwa hawatoi huduma vizuri kwa walimu na tumeendelea kusisitiza kwa maafisa elimu kutoa huduma hii vizuri kwa walimu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, chombo hiki kinaanza lini? Chombo hiki kwa utaratibu kimeshaanza tarehe 1 Julai, 2014. Sasa hivi kimekamilisha zile hatua mbali mbali za kisheria chini ya Tume ya Utumishi, ili zitakapokamilika sheria zake na Kanuni na taratibu za namna chombo kitakavyofanya kazi, mara moja kitaanza kufanya kazi hiyo, lakini tayari hatua hiyo imefikiwa.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa imani yangu ni kwamba, walimu ni nguzo kubwa sana ya kuleta mabadiliko ya kielimu nchini. Mwezi Desemba, 2014, niliuliza swali la msingi kuhusu mchakato wa malipo ya walimu na katika Ofisi ya Waziri

Mkuu ilinijibu kwamba suala hilo linashughulikiwa *specific* katika Wilaya ya Kisarawe kwamba, itakapofika mwezi Februari, 2014 walimu wote watakuwa wamelipwa *areas* zao zote.

Mheshimiwa Spika, lakini mpaka wiki iliyopita, karibu walimu 39 hawajalipwa *areas* zao, lakini licha ya hivyo wana madai mbalimbali.

Je, Serikali inatamka vipi katika *commitment* yake iliyoiweka katika wilaya ya Kisarawe, kuhakikisha kwamba walimu wale wanalipwa madai yao yote.

**SPIKA:** Swali wala halikuwa la Kisarawe.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake Mheshimiwa Jafo, pia lingeweza kuulizwa na yeyote nchini ambako tuna walimu na bado walimu wana madai ambayo wanayadai. Nataka kutoa taarifa lakini kwamba, madeni yote ambayo yalikuwa yamehakikiwa, yamekusanywa na Serikali kwa walimu na Chama cha Walimu kikatamka jumla ya bilioni 61.7, yaliweza kuchukuliwa.

Lakini kazi kubwa iliyofanywa ni kuhakiki kuweza kujua ukweli wa madeni haya na kama ifuatavyo tumeweza kufanya ulipaji na ulipaji huu ni wa nchi nzima. Kwa hiyo, kila Halmashauri imeguswa.

Mwezi Julai, 2013 mpaka Juni, 2014, tumeshalipa jumla ya bilioni 25.7. Kwa hiyo, utakuta walimu wanalipwa maeneo mbalimbali. Kuanzia Julai, 2014 mpaka Novemba, 2014, tumeshalipa jumla ya shilingi bilioni 10.9. Lakini pia mwezi Desemba, 2010, tulilipa madeni yasiyokuwa ya mishahara, kwa sababu haya yote unayoyatamka ni yale ya mshahara. Jumla ya bilioni 5.33 tumeshalipa kwa walimu maeneo mbalimbali.

Hapa sasa kufikia Desemba, madeni yote yaliyobaki ya jumla bilioni tatu, yameshahakikiwa na taarifa zimekwenda Hazina, tunasubiri Hazina waweze kuwalipa.

Kwa hiyo, utakuta kila Halmashauri walimu ambao wamejitokeza kulipwa wanaendelea kulipwa kwa awamu kadiri tunavyowalipa na hatulipi Halmshauri nzima kwa pamoja, kwa sababu majina yanakwenda kwa mtiririko na majina haya yanalipwa kwenye mishahara yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Dakika 10 zimechukuliwa na swali hilo.

Na. 54

**Serikali ya Mkoa wa Katavi Kuzuia Wawekezaji**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA (K.n.y. KOMBO KHAMIS KOMBO)** aliuliza:-

Serikali ya Mkoa wa Katavi imezuia Mwekezaji Mzalendo kuwekeza katika sekta ya kilimo mkoani humo:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho ni kwenda kinyume na kauli mbiu ya kuongeza ajira kwa wananchi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kitendo hicho kinadumaza maendeleo ya mkoa huo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mbunge Mgogoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mkoa wa Katavi ni moja ya mikoa katika Tanzania ambayo inaupa kipaumbele uwekezaji katika Nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama njia ya kuharakisha maendeleo na kuongeza ajira. Mkoa umeshiriki katika kuandaa na kuwa mwenyeji wa makongamano ya uwekezaji matatu ya kitaifa yaliyolenga kuhamasiha uwekezaji na kutangaza fursa zilizopo katika mikoa ya Rukwa, Kigoma na Katavi yenyewe.

Hadi sasa mkoa umekwishapokea maombi ya wawekezaji wazalendo 18. Kati ya hao waliomba kuwekeza katika sekta ya elimu wako watatu, sekta ya utalii, wako wanne, biashara na viwanda wako watatu, ufugaji wa nyuki na kilimo wako wanne. Waombaji hao wamepatiwa ushirikiano na wanaendelea na taratizu za kuwekeza katika sekta hizo.

Mheshimiwa Spika, mkoa umeunda timu ya uratibu na uwekezaji ambayo pia ina majukumu ya kutangaza maeneo ya uwekezaji, pamoja na kupokea na kuchambua maombi ya wawekezaji, kutoa maelekezo ya taratibu ya uwekezaji na kuratibu upatikanaji wa maeneo ya kuwekeza.

Kumbukumbu zilizopo katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Katavi hazionyeshi kuwepo mwekezaji aliyekataliwa kupatiwa eneo la kuwekeza katika kilimo. Hivyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge atoe usharikiano kwa Serikali kumjua mwekezaji aliyezuiliwa kuwekeza ili ufuatiliaji ufanyike na ikithibitika, hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyotanguliwa kuelezwa katika sehemu (a) ya jibu hili, Serikali haina sababu yoyote ya kumzuia mwekezaji anayetaka kuwekeza, badala yake wawekezaji wote wa ndani na nje, wameemdelea kukaribishwa ili kuwekeza katika fursa zilizopo nchini, ikiwemo sekta ya kilimo.

Nirudie tena kueleza kuwa, endapo itathibitika kwamba kitendo hicho kilifanyika, Serikali haitasika kuchukua hatua stahiki kwani kitakuwa kinarudisha nyuma jitihada za kuupatia maendeleo mkoa wa Katavi na taifa kwa ujumla wake. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imezoea kuwakumbatia wawekezaji wa nje na kuwafanyia mambo yao kwa haraka kwa kuwapa ardhi na kuweza wawekezaji wa nje kuchukua ardhi na kwenda kuichukulia mikopo bila kuiendeleza na wengi wao ni matapeli.

Je, Serikali, ina mkakati gani sasa wa kwasaidia wawekezaji wazalendo kwa haraka kuweza kufikia malengo yao ya kuwekeza ndani ya nchi ili na Watanzania wawekeze kunufaika na uwekezaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, lakini ulikuwa usaidie yule mwingine, utasaidiaje kutoa taarifa zake?

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA**: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa sababu mwenye swali hayupo na hatuwezi tukaliacha swali linaelea hewani.

**SPIKA:** Haya, utamwambia.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali sasa imekuwa makini sana kwa wawekezaji, hasa wa nje, kwa maana ya kutaka kujua ukweli wa nia yao ya dhati ya uwekezaji kwenye sekta yoyote wanayoihitaji hapa nchini. Mambo yanayofanyika ni kwanza kutambua nchi anayotoka.

Lakini kujua mtaji alio nao na uhalisia wa mradi wenyewe ambao anataka kuuwekeza ili kuondoa migogoro ya wawekezaji wa nje wanaopewa maeneo hapa kwetu, kukaa na maeneo hayo kwa muda mrefu na wakati mwingine kubadilisha hata nia. Badala ya kuwekeza kwenye eneo aliloombea, anafanya mambo mengine ambayo hayakurusiwa.

Kwa hiyo, umakini huu upo, wakati huo huo tunaendelea kutoa nafasi za wazi kwa Watanzania wenyewe, kwa maana ya Watanzania walioko ndani ya nchi ambao wanataka kuwekeza kwenye sekta mbali mbali.

Kwa Watanzania ni rahisi kujua ukweli wake, lakini pia uwezo wake wa kifedha kupitia taasisi za kifedha na sasa Serikali inaendelea kuweka utaratibu wa kuwezesha Watanzania ambao wanataka kuwekeza kwenye sekta zao kwa kuwaongezea mitaji, jambo hili litapanua uwekezaji wa ndani zaidi.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali la nyongeza.

Tunajua nchi yetu ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha wawekezaji wanakuja nchini ili isaidie kwa kiasi kikubwa kuondokana na tatizo la ajira, hasa kwa vijana, lakini wawekezaji wengi wamekuwa wakija wakitumia ardhi yetu kukopa mikopo. Lakini wanashindwa kuwekeza kwa kitu ambacho wameomba kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Kwa mfano, kuna mwekezaji mmoja Kirwa, alikuja kwa ajili kuwekeza kulima mibono, lakini baadaye hakufanya hiyo shughuli na matokeo yake akaanza kuvuna mbao, bila Serikali kujua. Sasa je, Serikali inalijua hilo, na kama inalijua, imechukua hatua gani kwa wawekezaji kama hao wanaokuja kuchukua maeneo kwa jambo lingine, lakini wanafanya shughuli nyingine kinyume na uataratibu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Anaweza asilijue hilo, laikini swali la msingi amelielewa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU)**: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kama ambavyo nimejibu pia kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Mkiwa, juu ya namba ambavyo sasa Serikali iko makini kwa wawekezaji wote wa nje, hata wa ndani ambao wanaomba kuwekeza kwenye setka moja, lakini wakafanya jambo lingine tofauti.

Uwekezaji huu hufanywa kwenye maeneo yetu ya Halmashauri za Wilaya kote Nchini na tumezipa malmlaka Halmashauri za wilaya kufanya ufuatiliaji wa wawekezaji ambao wameomba kwenye maeneo hayo husika.

Kwa hiyo, basi, ni rahisi nasi pia kupata taarifa ya jambo lolote linaoendelea kinyume na matarajio ambayo tumekubaliana kwenye maandishi.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, bado niwahakikishie na hasa Mheshimiwa Mbunge, kwamba, mwekezaji huyo wa Kilwa, na kwa kuwa Serikali ipo pale Kilwa, iko kwa Mkuu wa Wilaya, iko Halmashauri ya Wilaya.

Bado tutawasiliana baada ya kutoka hapa, kujua mwekezaji huyo ni nani aliwekeza kwenye eneo lipi, ili pia tuone hatua zilizochukuliwa kwenye ngazi ya awali ili tuwasiliane pia na Mkuu wa Mkoa wa Lindi, tuone namna sahihi walivyoichukua na sasa jambo hili kwa nchi nzima, kutoa mianya kwa wawekezaji wa ndani au wa nje, kwa mikataba tuliyoiweka, kufanya jambo nje ya mkataba ambao tumeuweka. *(Makofi)*

Na. 55

**Mradi wa Maji wa Masoko Wilayani Rungwe**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Mradi wa Maji wa Masoko Wilayani Rungwe uliotarajiwa kunufaisha wananchi wa vijiji 15. Ulisainiwa mwaka 2009 na ulitegemewa kukamilika na kukabidhiwa kwa wananchi mwezi Agosti, 2011 lakini hadi leo hakuna hata kaya moja iliyopatiwa maji ya mradi huo.

Je, Serikali ina nia ya kweli ya kuwapatia wananchi hao maji hasa ikizingatia kuwa miradi mingi mipya imeanzishwa humu humu nchini na kukamilika wakati wa mradi wa masoko ambao ungekamilika miaka minne iliyopita bado unakwekwa kando.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa David H. Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Masoko ni miongoni mwa miradi mikubwa ya maji inayotekelezwa Wilayani Rungwe, ambao unagharimiwa na Serikali kwa asilimia 100. Ndani ya mradi huu, vipo vyanzo vitatu vya maji, ambavyo ni Mbaka, Kigange, Ndurunga, vinavyohuduia Kata tatu, Masukuru na Ikama vyenye vijiji 15 vya Halmashauri ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, gharama za mradi huu kwa mujibu wa mkataba ni shilingi bilioni 4.7 na fedha iliyokwishalipwa ni shilingi bilioni 1.2. Mkandarasi alisaini mkataba tarehe 25 Mei, 2010 na alitakiwa kukamilisha kazi tarehe 30 Mei, 2012, baada ya kuongezewa muda wa ziada.

Mradi huu umesimama kwa muda mrefu kutokana na mgogoro unaoendelea kati ya Halmashauri na Mkandarasi baada ya mkataba kuvunjwa na sasa hivi suala hili lipo chini ya msuluhishi likisubiri maamuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayo nia ya dhati ya kuendeleza na kukamilisha miradi yote nchini ukiwemo mradi huu wa Masoko.

Katika Bajeti ya mwaka 2014/2015 Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 1.5 kwa Halmashauri ya Rungwe na tutaendelea kupeleka fedha kadiri zitakavyopatikana hadi mradi huu utakapokamilika.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba pesa zilizotolewa mpaka sasa ni bilioni moja nukta mbili saba ambayo ni asilimia ishirini na tano ya gharama ya mradi na amesema kwamba kuna mgogoro. Lakini hata kusingekuwa na mgogoro hii asilimia 25 isingeweza kumaliza mradi.

Matatizo hapa ni kwamba pesa hazipelekwi kule, mradi mabao ungekamilika mwaka 2012 leo tunazungumzia habari ya asilimia 25 na Wizara ilituambia kwamba mpaka sasa pesa za ndani ambazo wamepokea kwa ajili ya miradi ni asilimia 35 tu. Lakini tunaona miradi inakwisha na inafunguliwa. Nilitaka kumwuliza Naibu Spika kwamba hiyo inayofunguliwa ni kwa sababu inapewa kipaumbele…

**SPIKA:** Huwezi kuniuliza mimi.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri, samahani.

**SPIKA:** Mwulize Waziri lakini kupitia kwangu.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika nilitaka kukuuliza kama hizi bilioni moja nukta tano sita zilizotengwa mwaka huu atazisimamia na kuuweka huu mradi katika kipaumbele ili na wenyewe uweze kwisha?

Swali la pili dogo ni kwamba Kamati yangu katika miezi miwili iliyopita tumepita katika mikoa 17 tukikagua miradi, na kuna jitihada imefanyika na tunaona mawaziri wanafungua miradi. Picha zinapigwa na ni kitu kizuri. Nilichotaka kupendekeza ni kwamba, kwa nini wasiende pia kwenye maeneo ambayo yana matatizo ya maji au katika miradi ambayo inasuasua, waende na waandishi wa habari pia wapigwe picha? Kama hilo watalikubali lini watakwenda kuukagua mradi wa masoko?

**SPIKA:** Ahsante, umenyumbua sana swali la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Profesa Mwakyusa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninakubaliana naye kwamba kumekuwa na changamoto katika mradi wa masoko na yeye ni mjumbe katika Kamati hiyo ya Kilimo Mifugo na Maji. Kamati imeshafika katika mradi huu. Lakini Serikali imefanya jitihada ya kupeleka fedha hizo na hivi ninavyoongea ziko Shilingi milioni mia tano sitini na mbili, hazijafanya kazi yoyote kwa sababu Halmashauri iko katika mgogoro na Mkandarasi. Kwa hiyo, Kamati yake na sisi wizara tushirikiane kusaidia kumaliza mgogoro huu ili mradi huu uendelee kutekelezwa. *(Makofi)*

La pili, nakubaliana naye kwamba ipo miradi ambayo imefanikiwa na inaendelea kuzinduliwa lakini hatuendi tu kwa ile tunayoizindua. Ipo pia ambayo imekwama kutokana na fedha na hii nayo tunafika na kusukuma kuona kwamba miradi hii inatekelezwa. Nimwahidi tu

kwamba hata Masoko nako hakujatengwa, tutafika na Kamati imefika na maeneo mengine yenye changamoto kama hizo. Si tu kuzindua bali kuangalia changamoto zilizokwamisha miradi hiyo.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka kumwuliza Waziri kwamba karibu miradi yote ya maji hapa nchini imekwama kwa sababu ya kukosekana fedha. Je, Serikali ina kauli gani juu ya hali hiyo?

**SPIKA:** Ahsante sana, swali la moja kwa moja, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Akunaay.

Ni kweli kwamba miradi mingi imekwama ikiwa kwamba changamoto ni fedha, kukosekana kwa vyanzo vya maji. Nakubaliana naye na nimefika Manyara nimepokea taarifa za utekelezaji wa miradi katika Wilaya yake. Waziri wa Fedha ameshatuahidi kwamba atatupatia fedha ili tuweze kulipa wakandarasi wanaodai.

**SPIKA:** Tuendelee na Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, atauliza swali hilo.

Na. 56

**Ongezeko la Watu na Uchache wa Rasilimali Nchini**

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU** aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko kubwa la watu nchini Tanzania lakini rasilimali zimebaki zile zile, ongezeko hilo limesababisha kukua kwa haraka miji/vijiji hivyo kuongezeka pia mahitaji ya rasilimali kukidhi mahitaji ya ongezeko la watu. Kutokana na uchache huo wa rasilimali ikilinganishwa na ongezeko la watu kumesababisha migogoro mikubwa kati ya Hifadhi ya Taifa, wafugaji na wakulima:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe miradi mikubwa ya kutenga maeneo, kuwajengea miundombinu stahiki, kuwapa mbinu na stadi za kutumia rasilimali hizo chache za wakulima na wafugaji ili waweze kuendesha shughuli zao kwa tija?

Je, Serikali inafahamu kuwa ongezeko kubwa la watu ni kiini cha mabadiliko ya tabianchi na inachukua hatua gani dhidi ya jambo hili?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu. Haijaandikwa Dalaly imeandikwa Dalae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga, lenye sehemu A na B kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ongezeko la idadi ya watu nchini ni changamoto katika matumizi ya rasilimali hususan ardhi vijijini. Ongezeko hilo linachochea migogoro mbalimbali kwa kuwa mahitaji na matumizi yanaongezeka kila siku wakati ardhi yenyewe haiongezeki.

Mheshimiwa Spika, ni kweli vile vile ongezeko la idadi ya watu ni kiini cha mabadiliko ya tabia nchi ikiwa hatusisitizi umuhimu wa hifadhi ya mazingira.

Takwimu za idadi ya watu Tanzania zinaonesha kuwepo na ongezeko la idadi ya watu kutoka milioni kumi na mbili *point* tatu mwaka 1967 hadi watu milioni arobaini na nne *point* tisa mwaka 2012 wakati ukubwa wa ardhi ni ule ule.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa idadi ya watu kunaashiria ongezeko la mahitaji ya rasilimali hasa ardhi kama nilivyoeleza kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiuchumi na kijamii kama makazi, kilimo, ufugaji na mahitaji ya nishati zinazotumiwa na binaadamu kama vile kuni, mafuta, makaa ya mawe na mafuta mazito.

Vile vile ni kweli ongezeko la matumizi ya rasilimali hizi hasa nishati, huongeza uzalishaji wa hewa ukaa ambayo inasababisha ongezeko la joto kwenye uso wa dunia na mtawanyiko wake huishia kuwa na vipindi vya joto, ukame, mafuriko, maradhi ambayo ni maafa makubwa.

Mheshimiwa Spika, jitihada mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na kuridhia mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi na itifaki ya Kyoto ya mwaka 1997 na Kuandaa mpango wa kitaifa wa kuhimili athari za Mabadiliko ya Tabianchi ya Mwaka 2007.

Aidha kwa sasa Serikali inatekeleza mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ulioandaliwa mwaka 2012. Mkakati huu unaelekeza sekta mbalimbali kama vile sekta ya kilimo, maji, madini, nishati na kadhalika kuzingatia kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi ya Tanzania kuwa na mpango na matumizi bora. Mkakati huo umeanza kutekelezwa katika Wilaya ya Mvomero na utasaidia wakulima na wafugaji kuendesha shughuli zao kwa tija.

Aidha kwa mwaka 2014/2015 Serikali inaendelea nakukamilisha kazi ya kuandaa Mipango na Matumizi Bora ya Ardhi ya Wilaya ya Tarime, Rorya, Newala na Geita na baadaye kufikia wilaya zote nchini ili kuwezesha matumizi ya ardhi kwenda sambamba na ongezeko la idadi ya watu.

**SPIKA:** Ahsante, Dkt. Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Waziri kwa majibu yake mazuri. Napenda nimwulize swali moja tu la nyongeza. Nakumbuka kwamba kwenye Wilaya ya Igunga ambako jimbo la Igunga lipo kuna mbuga inaitwa mbuga ya Wembele, ambayo ndiyo sehemu kubwa ya jimbo lile.

Mbuga hii enzi za zamani iliweza kutumika kwa wakulima na wafugaji, lakini pia kwa kuhifadhi wanyama bila mgogoro wowote. Lakini siku za karibuni kumekuwepo na migogoro kati ya wafugaji na wakulima na mwaka jana iliweza kutokea wakulima watano waliuawa kati ya ugomvi wa wakulima na wafugaji.

Sasa, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, kwamba Serikali ina mpango gani wa haraka wa kulipima eneo hili katika maeneo ambayo wafugaji watatumia, wakulima watatumia, lakini pia tutahifadhi maeneo ambayo kuna mazalia ya ndege wa aina tofauti tofauti wanaokuja kutoka Ulaya kufanya mazalia kule. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, swali la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwanza namshukuru sana na kumpongeza kwamba anahimiza matumizi bora ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji na hata wanyamapori.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwamba kuna mpango katika Wilaya ya Tarime, Rorya, Newala na Geita, nikasema baadaye katika Wilaya zingine. Naomba niahidi kwamba, kwa sababu yameshaanza kutokea maafa hata ya watu kuuawa basi na Wilaya ya Igunga iwe moja ya Wilaya za mwanzo baada ya Wilaya nilizozitaja katika kuwa na mpango mzuri na bora wa matumizi ya ardhi, ili yale mambo yote matatu yaweze kwenda sambamba lakini bila migogoro.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kupata fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Ni kweli kwamba kati ya mwaka 1961 wakati nchi yetu inapata uhuru na leo idadi ya watu imeongezeka zaidi ya mara nne. Kwa uwiano huo huo idadi ya watu imeongezeka katika jimbo la Tunduru Kaskazini, hasa kwenye maeneo ya Muwesi, Kalulu, Hulia na Twende mbele, maeneo ambayo yanapakana na Hifadhi za Taifa.

Swali langu ni kwamba. Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia upya mipaka ya maeneo ya Hifadhi ili kuweza ku-*balance* au kuweka uwiano kati ya umuhimu wa Hifadhi za Taifa, lakini pia na mahitaji muhimu ya kiuchumi na kijamii miongoni mwa wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Injinia Ramo Makani, Mbunge wa Tunduru, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, kwamba idadi ya watu inaongezeka na kama alivyosema yeye lakini ardhi haiongezeki wala rasilimali zingine juu ya ardhi na ndani ya ardhi haziongezeki. Ni kweli kwamba kumekuwa na mashindano makubwa ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima na kati ya watu na wanyamapori.

Kwa hivyo kama nilivyoeleza, nitaiongelea vile vile Wilaya ya Tunduru na Wilaya nyingine. Ninafikiri kwa kweli lazima mipango na matumizi bora ya ardhi ieneee nchi nzima na ninashukuru na ninapata faraja kwamba suala hili la ardhi, mipango na matumizi bora na suala zima la ardhi liko kwenye mapendekezo ya Katiba Inayopendekezwa.

Ndiyo maana tunasukuma wananchi waweze kupitisha Katiba ile ili masuala kama haya ya kugombania ardhi yaweze kupewa kipaumbele kama inavyotakiwa na mahitaji ya nchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

Na. 57

**Tanzania Kuwa Miongoni wa Nchi Masikini Duniani**

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye rasilimali nyingi za asili kama vile wanyama, ndege, madini, misitu, gesi, bahari, mito mikubwa, maziwa makubwa, milima, mabonde na ardhi yenye rutuba lakini ni nchi masikini duniani.

Je, ni sababu zipi za msingi zimesababisha hali hii?

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mrefu, kati na mfupi wa kutatua tatizo hili na kuiondoa Tanzania katika dimbwi la umasikini?

Je, wananchi (wazawa) wa nchi hii wanashirikishwaje katika kumiliki rasilimali hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu A, B na C kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye rasilimali nyingi za asili lakini ni kweli vile vile ni moja ya nchi masikini duniani, ambapo nafurahi kuona kwamba sasa Tanzania inaondokana na umasikini.

Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zinazochangia Tanzania kuwa na hali hii ni pamoja na maendeleo hafifu katika sekta ya kilimo, kiwango kidogo cha ujuzi na wataalam tulio nao ambao wangeweza kutumika katika kuzitumia fursa zilizotajwa, ukosefu wa teknolojia ya kisasa ambayo ingetumika katika sekta za uzalishaji kama vile kilimo, uvuvi, viwanda na mifugo.

Miundombinu hafifu ya usafiri na vifaa vya usafiri, kuongezeka kwa idadi watu ambayo inatoa msukumo mkubwa wa matumizi ya rasilimali zilizopo. Ukosefu wa ajira za kudumu hasa kwa sehemu kubwa ya nguvu kazi ikiwemo vijana na wanawake, ukosefu wa mitaji kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na mtikisiko wa kiuchumi duniani.

Mheshimiwa Spika, B, ili kuondoa umasikini Serikali imeandaa mipango mbalimbali ya kitaifa na kisekta kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025 ambayo inatekelezwa kupitia mpango wa muda mrefu wa miaka 15 kutoka mwaka 2011/2012 mpaka 2025/2026 ambao nao umegawanywa katika awamu tatu, yaani miaka mitano mitano.

Kwa hiyo Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2011/2012 hadi 2015/2016 na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Tanzania ni sehemu ya Mipango ya muda wa kati wa utekelezaji wa dhana nzima ya kuondoa umasikini nchini. Kwa upande wa mipango ya muda mfupi Serikali inatekeleza Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya kila mwaka kwa lengo lile lile la kuondoa umasikini.

Mheshimiwa Spika, C, kupitia sera, sheria na Kanuni mbalimbali kutegemea na eneo ama sekta husika, Serikali imeendelea kutoa fursa za ushiriki wa wananchi katika kumiliki rasilimali. Mathalan katika eneo la Ardhi Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 Kifungu cha 20 kinatoa fursa za umiliki wa rasilimali hiyo kwa wananchi. Vile vile Sera ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi pia inatoa nafasi kubwa ya wananchi kumiliki rasilimali, ikiwemo ardhi.

Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Kurasilimisha Biashara na mali za wanyonge Tanzania ili itumike kama dhamana kwa wananchi wanaoomba kukopa ikiwa ni sehemu ya kuwawezesha kupata mitaji. Katika kuhakikisha kuwa wananchi wanashirikishwa, Serikali kupitia Bunge Maalum limeweza kuingiza masuala yote yanayohusu ardhi na rasilimali nyingine za nchi ndani ya Katiba Inayopendekezwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninampongeza Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa babu zetu wakati wa ukoloni walitumia silaha kama vile mapanga, sime, nyundo, mishale kulinda uhuru wao na hali kadhalika. Mpaka sasa hivi nchi yetu inahujumiwa rasilimali zake na wawekezaji uchwara, wawekezaji feki, wawekezaji matapeli na wahujumu uchumi. Mheshimiwa Waziri, unatushauri wananchi wa Tanzania tutumie silaha gani kupambana na hawa wawekezaji?

Swali namba mbili, kuna rasilimali ambazo hazijawahi kutumika mpaka sasa hivi tangu tupate uhuru. Mheshimiwa Waziri unatushauri nini hasa sisi wabunge watunga sera ili tuweze kutunga sheria itakayotuwezesha kutumia hizo rasilimali haraka iwezekanavyo ili kuondoa umasikini Tanzania?

**SPIKA:** Haya, swali refu sana, Mheshiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo, maswali yake yote mawili.

Kwanza, ni kweli kwamba Watanzania walijitahidi sana kupigania uhuru wao. Lazima niseme kwamba hii ni nchi moja ambayo ilipata uhuru wake kwa amani, lakini kwa kujenga hoja zaidi badala ya kutumia silaha.

Kwa hiyo, naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Watanzania wote kwa ujumla kwamba suala la uwekezaji ni suala muhimu kwa wawekezaji wa ndani na wa nje. Lakini ni kweli kwamba kati ya wawekezaji wanaotoka nje inawezekana wengine siyo wale ambao tunawahitaji.

Kwa hiyo, silaha ambazo tunaweza kuzitumia vizuri ni kuwa na sera nzuri, sheria nzuri, utekelezaji mzuri na mkakati mzuri wa kujua nani atanufaisha nchi wakati yeye anapata faida yake.

Kwa hiyo, naomba tuwe macho wote lakini kwa kweli tusikatae wawekezaji kutoka nje kwa sababu dunia nzima hata walioendelea kama Marekani na Ulaya bado wanavutia wawekezaji kwenye nchi zao. Sisi Watanzania vilevile tunahitaji wawekezaji kutoka nje.

Lakini ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba tuwe macho kwa kuona watu ambao watatunufaisha kwanza kwa kutuletea teknolojia, mitaji, ajira kwa ajili ya vijana wetu na manufaa yote yanayotokana na uwekezaji.

Pili, ni kweli bado tuna rasilimali ambazo hazijatumika na hasa ukilinganisha na mahitaji yetu ya kuondoa umaskini. Kwa hiyo, kupitia sera mbalimbali katika sekta mbalimbali kwa kushirikiana na wananchi lazima tutumie raslimali zilizopo.

Ninaomba Watanzania wajue kwamba raslimali ya kwanza ni raslimali watu ambayo inapaswa ipewe elimu na maarifa yanayotakiwa ili sisi wenyewe tuwe na uwezo wa kutumia raslimali zetu. Lakini ni kweli vilevile vizazi vijavyo vinategemea raslimali hizi kwa hiyo hatuwezi kuzimaliza kwa wakati mmoja.

**SPIKA:** Swali lingine linakwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa.

Na. 58

**Juhudi za Kupunguza Idadi ya Watu Wasiojua Kusoma na Kuandika.**

**MHE. DKT. GERVAS A. MBASSA** aliuliza:-

Kumekuwepo na juhudi nyingi za kupunguza idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, lakini bado idadi hiyo inazidi kuongezeka kote nchini.

(a) Je, ni asilimia ngapi ya wananchi wa Tanzania (Bara na Visiwani) ambao hawajui kusoma na kuandika?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kurudisha au kuboresha kisomo cha Elimu ya Watu Wazima?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza posho ya Walimu wa MEMKWA ili wafanye kazi yao kwa ufanisi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, Mbunge wa Biharamulo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, takwimu za Sensa ya Watu na Makazi za Mwaka 2012 zinaonyesha kuwa watu wazima wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ambao hawajui kusoma na kuandika ni 22.4% kwa Tanzania Bara na Visiwani ni 15.8%.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuboresha kisomo kwa watu wazima, Serikali inatumia mkakati ifuatayo:-

Inatekeleza mpango wa uwiano kati ya Elimu ya Watu Wazima na Jamii (MUKEJA) ambao huwahimiza wanakisomo kutafakari, kuchambua na kubainisha matatizo yao na kubuni mbinu ya kuyakabili kwa vitendo.

Aidha, inaimarisha utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Msingi kwa walioikosa (MEMKWA) na kutekeleza *program* ya "Ndiyo Ninaweza" yenye lengo la kutoa elimu kwa vijana na watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, kupitia luninga na seti za *DVD* zenye masomo.

Vilevile, Serikali inaendesha mpango wa utoaji wa elimu masafa na ana kwa ana kwa vijana na watu wazima wanaojiendeleza.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kiwango cha posho kinachotolewa kwa wawezeshaji wa MEMKWA ni kidogo na kinapunguza ari ya wawezeshaji katika kujituma kufanya kazi. Katika jitihada za Serikali kukabiliana na changamoto na changamoto hiyo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 imeweka msisitizo wa kuweka utaratibu na mazingira wezeshi ya kuhakikisha Elimu na Mafunzo, ikiwemo Elimu ya Watu Wazima, inatolewa kwa ufanisi katika ngazi zote, kwa njia Huria na Masafa.

Hivyo, kutokana na sera hii mpya, Serkali itaangalia upya uwezekano wa kuongeza posho kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 20,000/= kwa mwezi.

**SPIKA:** Ahsante, Dkt. Antony Gervas Mbassa, Swali la nyongeza!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza lakini nianze tu kwa masikitiko makubwa sana kwamba swali hili muhimu sana limepewa majibu mepesi kulingana na hali ya sasa ya elimu jinsi ilivyo.

Kwanza, ni kweli kabisa sasa hivi wawezeshaji au Walimu waliokuwa wakifundisha MEMKWA na MUKEJA wamekata tama, kwani tangu mwaka 2013 hawajalipwa hata senti moja. Leo Mheshimiwa Naibu Waziri analitangazia Bunge lako Tukufu kuwa kwamba wanalipwa shilingi 20,000/=, siyo kweli. Walikuwa wakilipwa kiasi cha shilingi 5,000/= na mpaka hivi sasa hawajalipwa.

Je, ni lini Walimu au Wawezeshaji hawa watalipwa kwa muda wote ambao wamejitolea kufanya kazi hii kwa kiwango alichokitamka Mheshimiwa Naibu Waziri?

Pili, nimekuwa nikihudhuria vikao vya Halmashauri muda wote tangu nimeingia katika Bunge lako Tukufu na nimewahi kuuliza katika Halmashauri Afisa anayehusika na elimu ya watu wazima kunipatia walau orodha tu ya vituo vilivyo katika Jimbo langu na hakuweza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa kauli gani au Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anatoa kauli gani kwa niaba ya Serikali kwa watu kama hao wanaokwamisha maendeleo ya wananchi?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata hili swali la Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, wataalamu walikwenda kwa kina kuangalia Halmashauri ambayo yeye anatokea, yaani Halmashauri ya Biharamulo.

Naomba nikiri kabisa hayo aliyozungumza kwa Halmashauri yake, wawezeshaji wa MEMKWA hawajalipwa kuanzia mwezi Machi, 2013. Ninaomba kupitia Bunge hili Tukufu, sasa nitoe tamko kwa Halmashauri ambayo tuna uhakika nayo, ambayo ni Halmashauri ya

Biharamulo. Kuanzia sasa hivi ninapotamka, Halmashauri ile ilipe *areas* zote kuanzia mwaka 2013 mpaka sasa ambazo ni 20,000/= kwa mwezi. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa Maafisa Elimu wa Elimu ya Watu Wazima, ambao inaonyesha hawajali kabisa umuhimu wa Elimu ya Watu wazima, ninaomba wajue kabisa kwamba sasa mimi nitaanza kupita kwenye Halmashauri.

Kwa kweli siwezi kwenda Biharamulo kwa sababu nimetoka Kagera juzi, lakini nitachukua Halmashauri kama kumi, nikaone hao Maafisa Elimu ya Watu Wazima upande wa Elimu ya Watu Wazima ambao hawajali Elimu ya Watu Wazima na kutuletea kiasi cha watu wazima wengi ambao hawajui kusoma na kuandika. Tutawachukulia hatua kama ambavyo tutaona inafaa. *(Makofi)*

Lakini nirudie kwamba Halmashauri ya Biharamulo tumegundua kwamba haijawalipa wawezeshaji tangu Machi, 2013. Sasa sina uhakika huenda na Halmashauri nyingine nazo zimefanya hivyo hivyo. Kupitia swali hili la Mheshimiwa Dkt. Antony Gervas Mbassa, naomba Halmashauri zote Tanzania kama kuna Halmashauri ambayo haikuwalipa wawezeshaji, basi ilipe *areas* kuanzia kipindi ambacho haikuwalipa mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, ahsante!

**SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Yussuf Hussein, swali la nyongeza!

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, suala la kupunguza idadi ya wanaojua kusoma na kuandika katika nchi yetu ni suala mtambuka. Je, Mheshimiwa Waziri…..

**SPIKA:** Ngoja kwanza, tunapunguza nini?

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Wasiojua kusoma na kuandika.

Mheshimiwa Waziri, je, una taarifa kwamba Dodoma *Nkuhungu Primary* hiyo shule kwa muda wa miezi mitatu wanafunzi hawaendi shule kwa sababu ya kukosa vyoo?

Je, idadi hii haitaongeza idasdi ya watu wasiojua kusoma na kuandika katika nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Waziri kachimbe vyoo sasa, haya!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza sikuwa na habari, yeye ndiye amenihabarisha. Lakini kwa sababu Nkuhungu ni hapa hapa Dodoma, naomba niseme kwamba nitakwenda Nkuhungu kati ya hizi siku mbili au tatu zijazo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba tuendelee na swali linalofuata, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, atauliza swali hilo.

Na. 59

**Ada za Vyuo Vya Utumishi wa Umma na Vyuo Vikuu vya UDOM na UDSM**

**MHE. AMINA NASSOR MAKILAGI** aliuliza:-

Serikali ya Tanzania ina nia ya kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania:-

Je, mchanganuo wa ada za Vyuo vya Umma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma ukoje na unaendana na hali halisi za Watanzania wa kipato cha chini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala zima la utoaji wa elimu na utozaji wa ada katika vyuo mbalimbli nchini limekuwa likitofautiana kwa muda mrefu. Kwa sasa, Tanzania ina jumla ya Vyuo Vikuu 53 na Taasisi 21 zinazotoa shahada. Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 Kifungu 6.4.3 kilikuwa kinaruhusu Taasisi ya Elimu ya Juu kupanga na kusimamia vyanzo vya mapato ikiwa ni pamoja na kutoza ada za masomo.

Mheshimiwa Spika, ada katika Vyuo Vikuu vya Umma, ikiwa ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dodoma zinatofautiana kati ya chuo na *program* ambayo mwanafunzi anasomea. Kwa mfano, katika *program* ya Uhandisi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza shilingi 1,300,000.00 wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoza shilingi 1,500,000.00 kwa *program* hiyo hiyo kwa mwaka.

Katika *program* za Sayansi na Ualimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza shilingi 1,300,000.00 wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoza shilingi 1,200,000.00. Aidha, katika *program* za ualimu wa Sanaa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoza shilingi 1,000,000.0 wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinatoza shilingi 800,000.00

Mheshimiwa Spika,kwa kuzingatia tofauti za kiasi cha ada kinachotozwa na Vyuo Vikuu nchini, Serikali ilifanya utafiti wa kina kwa kushirikisha wadau mbalimbali ili kuweza kupanga ada elekezi kwa *program* zote zinazofundishwa katika Vyuo Vikuu vyote.

Mwongozo wa ada elekezi umekwisha andaliwa na kwa sasa Serikali inaandaa mfumo *(software)* wa kukokotolea ada zitakazotumika katika Vyuo Vikuu vyote nchini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Makilagi swali la nyongeza!

**MHE. AMINA NASSOR MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa majibu mazuri na kuipongeza Serikali kwa mpango wa kuangalia upya na kutoa mfumo wa ada elekezi katika vyuo vyote hapa nchini, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa kuwa, vyuo binafsi nchini kikiwemo chuo cha *IMTU* na vingine baadhi yake vimekuwa vikitoza ada kubwa sana na baadhi ya vyuo hivyo vimekuwa vikitoza kwa dola na siyo shilingi na wakati mwingine Serikali inapotoa mikopo kwa ajili ya vijana wanazingatia viwango vya Serikali hivyo wanashindwa kusaidiwa kwa sababu ile ada haitoshi.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa wakati ikifanya utafiti na kutoa ada elekezi na hivi vyuo binafsi viweze pia kuingizwa katika mpango huo. Ili walau ada iweze kusaidia hata wananchi wa kiwango cha chini waweze kupata elimu ya juu?

Pili, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inaongeza wigo na fedha ili vijana wetu sasa waendelee kupata mikopo, badala ya kuendelea kutoa kipaumbele kwa wanaosoma masomo ya Sayansi na elimu ya sekondari? Wigo uongezeke kwa vijana wanaochukua fani zote.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana!

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina Makilagi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza amezungumzia Vyuo kutoza ada kwa dola. Naomba nizungumze kupitia Bunge hili Tukufu kwamba siyo chuo tu bali kuanzia *kindergarten*, shule za msingi, shule za sekondari mpaka Vyuo Vikuu, hakuna mahali ambapo wanaruhusiwa kutoza ada kwa dola. Ada zote zinatozwa kwa fedha za Kitanzania.

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba amezungumzia *IMTU,* ni kweli *IMTU* walikuwa wameshafanya kitu kama hicho lakini tuliwachukulia hatua, tuliwaandikia barua kali na hawaendelei kufanya hivyo. Kama kuna chuo ambacho kinaendelea kufanya hivyo naomba kiache mara moja na kama kuna chuo ambacho mna uhakika kinafanya hivyo Waheshimiwa Wabunge mtusaidie basi ili na sisi tuweze kuvifuatilia hivyo vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ameuliza swali lingine hapo hapo kwenye swali la kwanza kwamba hivi Vyuo Vikuu vingine vinatoza ada za juu na hasa Vyuo binafsi na vyuo vya Serikali vinatoza ada ambayo ni ya nafuu kidogo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri kwamba hivi vyuo vikuu vinatofautiana, Vyuo Vikuu vya Serikali vinatoza ada ambazo zina unafuu kwa sababu vinapata ruzuku kutoka Serikalini. Lakini ukija kwenye vyuo vikuu ambavyo ni vya binafsi navyo vipo vya aina mbili. Kuna vyuo vikuu ambavyo vipo kwa ajili ya faida kama chuo cha *IMTU* ni kama kipo kibiashara.

Kwa hiyo utakuta bei zao zipo juu lakini kuna Vyuo Vikuu ambavyo kama taasisi za kidini kama Vyuo Vikuu ambavyo vinaongozwa na Makanisa na Taasisi za Kidini za Kiislamu wao wanakuwa wanatoa huduma zaidi, kwa hiyo ada zao kidogo ni nafuu.

Swali la pili ambalo ni kama la tatu anazungumzia kuhusu tupanue wigo ili tuweze kutoa mikopo kwa fani ambazo hatujazichagua. Hapa naomba nikiri kwamba inakuwa ni vigumu kwa sababu ya hali halisi ya Bajeti, lakini kama kuna wanafunzi ambao hata kama hawachukui zile fani ambazo tumeziorodhesha kama wanafunzi wenye ulemavu huwa tunawapa hata kama wanachukua fani ambazo hatukuzipa kipaumbele.

Lakini pia kuna wanafunzi ambao tukithibitisha kwamba ni yatima, nao wanapata mikopo. Wanafunzi wengine ambao tunawaangalia ni wale ambao kaya zao hazina uwezo kabisa, tukithibitisha huwa wanapewa mikopo bila kujali fani ambazo zipo kwenye vipaumbele.

**SPIKA:** Mheshimiwa John J. Mnyika, swali la nyongeza liwe fupi.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Wizara ya Elimu imekuwa ikijibu hasa wakati wa Bajeti iliyopia kwamba utafiti ulishakamilika, mwongozo wa utaratibu wa be elekezi ulikuwa kwenye hatua za mwisho. Lakini inaonyesha kwamba leo tena tumejibiwa kwamba pamoja na kuwa mwongozo umekamilika lakini *software* haijakamilika, miezi mingi imepita wanafunzi wanaendelea kuumia na mzigo mkubwa wa ada.

Je, ni lini hasa hiyo *software* itakamilika ili kuwanusuru wanafunzi wa vyuo mbalimbali ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mzigo mkubwa wa ada?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kulijibu swali la Mheshimiw John J. Mnyika, ambalo ni swali muhimu sana kwa Watanzania wote kujua majibu yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba imechukua muda mrefu huu mfumo kukamilika, lakini naomba kutoa jibu la uhakika kwamba mfumo huu ambao ni *software* ili tuweze kukokotoa hizi ada na ziwe ni haki utakamilika mwezi ujao wa Aprili, 2015. Ahsante sana.

**SPIKA:** Umeeleweka, tunaendelea na swali linalouata Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 60

**Matukio ya Uvunjifu wa Amani**

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza:-

Kwa bahati mbaya inapotokea uvunjifu wa amani hujumuisha wananchi wote (anayehusika na asiyehusika); na wakati mwingine matukio hayo husababisha athari za uharibifu wa mali na kupoteza maisha hata kwa wananchi wasiohusika.

Je, Serikali itatoa msaada gani kwa wananchi watakaofikwa na maafa kutokana na matukio hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI (K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kuweli kuwa madhara kwa binadamu na uharibifu wa mali hujitokeza katika baadhi ya matuko ya vurugu. Mara nyingi madhara hayo ya kudhuru watu, kuharibu mali na miundombinu mbalimbali husababishwa na watu au makundi ya watu waovu wanaoshiriki vurugu.

Mheshimiwa Spika, hakuna sheria yoyote inayotoa haki ya fidia kwa mtu au kundi la watu wanaopata madhara kutokana na kadhia ya vurugu zinapojitokeza. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watu wote wanaobainika kuwa chanzo au kichocheo cha uvunjifu wa amani na kusababisha vurugu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wananchi na jamii kwa ujumla kujiepusha na vurugu zinazoweza kusababisha madhara kwa watu na mali. Ni vema tukaitikia wito wa Jeshi la Polisi wa Utii wa Sheria Bila Shuruti, ili kuepukanana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na matukio ya uvunjivu wa amani.

Mheshimiwa Spika, jamii ijenge utamaduni wa kutatua changamoto, makinzano na tofauti za kiitikadi au kiimani kwa njia ya amani, utulivu na kuvumiliana (Mazungumzo).

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Fakharia Shomar, swali la nyongeza!

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa masuala hayo ya uvunjifu wa amani hujitokeza hasa kwenye masuala ya shughuli za kisiasa.

Je, Mheshimiwa Waziri atawaelezea nini wananchi?

(b) Katika maelezo yake ameeleza kwamba, hakuna sheria inayotoa fidia kwa wahanga ambao hukumbwa na majanga hayo katika vurugu pasipo kutarajia. Je, ni nini ushauri wa Serikali kwa Wananchi wanaopatwa na kadhia hiyo?

Mheshimiwa Spika, ninaomba maswali yangu mawili yapate majibu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Fakharia Khamis, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, vurugu hizi zinatokea katika mikusanyiko ya watu inayosababishwa na mitazamo ya kiuharakati, utofauti wa itikadi na katika mikutano mbalimbali ya kisiasa. Hii inachangiwa na mihemuko na namna ambavyo watu wameshawishiwa kufanya jambo hilo.

Swali la pili, ushauri wa Serikali ni kuwaomba Watanzania na Wananchi kujiepusha ama kutoa taarifa pale ambapo wanaona kuna viashiria vya uvunjifu wa amani na kuwaomba tu pale panapotokea jambo kama hili, wasijihusishe na jambo hilo ili kuwaepusha na vurugu zinazoweza kutokea.

**SPIKA:** Tunaendelea, hamkusimama kabla, mkisimama sasa haiwezekani. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuri atauliza swali.

Na. 61

**Kujenga Jengo la Mahakama ya Wilaya – Rufiji**

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo la Mahakama ya Wilaya lenye hadhi katika Wilaya ya Rufiji?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga Mahakama zenye hadhi katika Wilaya zote za Tanzania. Hadi sasa jumla ya Mahakama za Wilaya 40 zipo katika Mpango wa Ujenzi wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Hata hivyo, Mahakama ya Wilaya ya Rufiji haipo katika mpango wa ujenzi wa mwaka huu, kutokana na Serikali kuweka kipaumbele cha ujenzi wa Mahakama katika maeneo ambayo hakuna majengo.

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, majibu ya Mheshimiwa Waziri yamenisikitisha sana.

(i) Kwa kuwa Wilaya ya Rufiji ni kongwe na majengo yake mengi yamejengwa kwenye miaka ya 1920 huko, tangu enzi ya Mkoloni na leo Mheshimiwa Naibu Waziri anasema Serikali haina mpango wa kuyaboresha majengo hayo likiwemo hilo la Mahakama. Je, Serikali haioni kwamba haiwatendei haki Wananchi wa Rufiji ambao wanastahili kupata huduma za kisheria za mahakama pamoja na Mahakimu wanaofanya kazi katika Wilaya ya Rufiji? *(Makofi)*

(ii) Katika Bunge Tukufu hili tulipitisha Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa Mahakama ambao tulitarajia ungeweza kuboresha huduma za kijamii kama makazi na vitu vingine kwa Mahakimu wetu wakiwemo wa Wilaya ya Rufiji ambao mpaka leo wanapanga mitaani, maisha yao siyo mazuri. Vilevile tulitarajia masilahi ya Majaji ya Mahakimu wetu, lakini mpaka sasa Serikali hii imeshindwa kutimiza hilo, wanapeleka fedha kidogo kwa kusuasua, wanapiga chenga na stori tu. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyogeza ya Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, wajina wangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninakubaliana na Mheshimiwa Mchuchuli kwamba, Mahakama ni muhimu sana katika suala zima la utoaji haki, lakini ninaomba pia nimjibu kwamba, angalau Wilaya ya Rufiji inayo majengo ya Mahakama. Hadhi ya Mahakama siyo majengo ni mamlaka. Mheshimiwa Diana Chilolo, amekuwa akilalamika tu kwamba, Wilaya ya itilima, Wilaya ya Singida Vijijini, hata ile mamlaka ya Mahakama ya Wilaya hawana na wao wako tayari watumie majengo ya Mahakama ya Mwanzo ili kupata ile hadhi tu ya Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ninataka kumthibitishia kwamba, tunao mpango wa kujenga Mahakama za Wilaya katika Wilaya zote na tunazo hapa Wilaya 43 na pia kufanyia ukarabati Mahakama za Wilaya 42. Kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, Wilaya ya Rufiji haipo. Tunadhani katika mwaka wa fedha unaokuja wa 2015/2016, kama anazo hoja za kutosha basi tutaingiza Mahakama ya Wilaya ya Rufiji katika mpango wa ujenzi na ukarabati.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Mbunge anasema kweli tumepitisha Mfuko wa Mahakama lakini fedha haziendi. Hii ni changamoto ambayo tunayo sasa hivi katika nchi yetu, lakini ni kweli tunaamini uwepo wa Mfuko wa Mahakama kwa kiasi kikubwa, utasaidia kutatua changamoto mbalimbali za utoaji haki katika nchi yetu. Kile kitendo cha Serikali kuongeza Bajeti ya Mahakama kutoka shilingi bilioni 102 mpaka bilioni 196 kwa Mwaka wa

Fedha 2014/2015, kwetu inaonesha ni dhamira ya dhati ya kutaka kuziwezesha Mahakama katika jukumu lake la msingi la kutoa haki katika nchi yetu.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kuniona. Katika jibu la swali la msingi Mheshimiwa Waziri amesema uchakavu wa majengo siyo tatizo, suala ni utendaji wa kazi. Zipo Mahakama za Mwanzo hapa nchini ambazo zilijengwa wakati wa mkoloni na zinahatarisha hata maisha ya watu, zinabomoka na mfano ni Mahakama ya Mtowisa.

Je, Waziri anasema nini kuhusu ukarabati wa Mahakama hizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ningependa kujibu swali moja la nyogeza la Mheshimiwa Malocha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba niweke vizuri, nilichokuwa ninajaribu kujibu ni kwamba, hadhi ya Mahakama siyo majengo ni mamlaka. Tunatambua kwamba, uchakavu wa majengo ni changamoto katika suala zima la utoaji haki. Nilichokuwa ninafafanua, zipo Wilaya ambazo hata ile mamlaka tu ya Mahakama ya Mwanzo au Mahakama za Wilaya hazina. Kwa hiyo, ninakubali uchakavu wa majengo ni tatizo, lakini kama nilivyosema, tunao mpango wa kukarabati majengo ya Mahakama katika Wilaya mbalimbali.

Nimesema katika Mahakama za Mwanzo, tume-*identify* zaidi ya Mahakama 381 kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati. Katika Mahakama za Wilaya, tayari tumeshaainisha Mahakama 42 kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati. Nirudie dhamira ya dhati ya Serikali ya kuhakikisha tunaboresha vitendea kazi vya Mahakama, yakiwemo majengo na magari ili iweze kutimiza jukumu lake la msingi la kutoa haki katika nchi yetu.

**SPIKA:** Tuendelee na swali linalofuata; Mheshimiwa Hussein Nassor Amar!

*(Lililokuwa Swali Na. 62 la Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe liliondolewa)*

Na. 62

**Vikundi vya Kuweka na Kukopa – *SACCOS***

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya kuweka na kukopa *SACCOS* hasa kwa watu waishio mijini tu:-

(a) Je, kwa nini Serikali haitoi kipaumbele kukopesha *SACCOS* za vijijini?

(b) Je, ni vikundi vingapi vya *SACCOS* vitapatiwa mkopo katika Jimbo la Nyang'hwale kwani hakuna hata *SACCOS* moja iliyopatiwa mikopo kwa awamu hii?

**SPIKA:** Samahani sikusema, Swali Na. 62 limeondolewa. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri endelea na majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'hwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* kama vilivyo *VICOBA*, ni miongoni mwa Taasisi Ndogo Binafsi za Kifedha *(Micro Finance Institutions*), ambazo huanzishwa, huendeshwa na kusimamiwa na Wananchi wenyewe. *SACCOS* ni Taasisi ya Vyama vya Ushirika vya Kuweka na Kukopa Fedha, huanzishwa na kumilikiwa kwa asilimia 100 na wanachama wake. Taasisi hizi zimeenea mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali haitoi fedha kukopesha *SACCOS* kutoka kwenye bajeti yake. Hakuna lengo wala fedha zilizotengwa zenye madhumuni ya kukopesha *SACCOS.* Hata hivyo, wapo wadau wengine wa maendeleo kama vile Baraza la Taifa la Uwezeshaji, baadhi ya Mifuko ya Jamii na baadhi ya Mabenki, hutoa mikopo kwa *SACCOS* kwa masharti na makubaliano kati ya pande mbili hizo husika.

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, Serikali ilikwishajiondoa katika kufanya biashara. Kwa kuwa *SACCOS* ni taasisi binafsi za ushirika wa kuweka na kukopa fedha na kwa kuwa Serikali kama nilivyoeleza haina lengo katika bajeti yake la kukopesha taasisi yoyote kama hizo *SACCOS,* ni wazi kuwa hakuna kikundi chochote cha *SACCOS* kutoka Jimbo la Nyang'hwale au Jimbo lolote nchini, kitakachopewa mkopo na Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunashauri Vikundi vya *SACCOS* Jimboni Nyang'hwale na popote nchini, wawasiliane na wabia wengine wa maendeleo kama vile Baraza la Taifa la Uwezeshaji, Mifuko ya Jamii na Mabenki, kwa ajili ya kupata mikopo hiyo. Ikumbukwe kwamba, wabia hao hutoa mikopo hiyo kwa masharti na makubaliano ambayo yanaafikiwa baina ya pande hizo mbili bila kuishirikisha Serikali ambayo hukubaliwa na kuzifaidisha pande zinazohusika.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu maswali haya vizuri sana, lakini ninaomba niongeze swali moja dogo.

Kwa kuwa sisi Wabunge tunasumbuliwa sana kule, vikundi mbalimbali vinakuja tunakosa majibu, leo majibu yametoka. Ninaiomba Serikali itoe ushauri kwenye vikundi waweze kupata hiyo mikopo na kuweza kunufaika nayo ili waweze kuwa na maisha bora kwa kila Mtanzania. Je, Serikali ina mpango gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, lazima nikubaliane na Mheshimiwa kwamba, katika hili suala la *SACCOS* kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa Umma hasa kwa kuwa *SACCOS* yenyewe inatawaliwa na sheria mbili; Sheria ya Ushirika kama Chama cha Ushirika. Kwa hiyo, kuna misingi ya uanachama katika ushirika ambayo ni muhimu wanachama wale wenye *SACCOS* wakajua. *SACCOS* hiyo hiyo pia inatawaliwa na Sheria ya *Microfinance,* ambayo sasa ni Sheria ya Taasisi za Fedha. Kwa hiyo, sasa kwa upande huo wale wanachama wanapokuwa wana *SACCOS* ile, wanawajibika kuwa na SACCOS ambayo inazingatia masharti na madhumuni, dhamana ya Taasisi ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni muhimu sana tutoe elimu kwa umma ambayo ni shirikishi, kwa maana ya wadau wote ambao tunahusika kutoa elimu hiyo. Kubwa zaidi ni kwamba, *SACCOS* yenyewe kwa malengo yake ya asili kabisa ni kuondoa umaskini. Sasa wanapowajibika kama chombo cha fedha ni muhimu pia wakajua kwamba, kwenye chombo cha fedha ni biashara, kuna faida na hasara na inayowajibisha wanachama wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kuwa jukumu hili ni kubwa na lina umuhimu, kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaenda kulifanyia kazi wadau wote ili tuongeze elimu kwa umma kwa wananchi kuhusu *SACCOS.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa wako wafanyabiashara ambao wamekuwa mstari wa mbele sana kusaidia *SACCOS* za Akina Mama na Vijana nchini mfano Dkt. Reginald Mengi:-

Je, Serikali itakuwa tayari kumpongeza mfanyabiashara huyu anayefanya kazi nzuri kwa Watanzania; Wanawake na Vijana pamoja na kuwahamasisha wafanyabiashara wengine wanaosaidia kuinua kiwango cha mchezo wa mpira wa miguu nchini wachukue jukumu hili la kusaidia *SACCOS* za Akina Mama na Vijana ili kuongeza kasi ya maendeleo ya Wanawake na Vijana nchini?

**SPIKA:** Tena mpira wa miguu na mikono ndani ya *SACCOS!* Haya! *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, wahusika wanaofanya kazi na *SACCOS* kuna mfumo wa Mabenki ambapo kuna *CRDB, NMB, Akiba Commercial Bank* wamejitokeza sana ku-*support* hizi *SACCOS,* halafu kuna vyombo vingine kama *PRIDE, FINCA* na vingine. Vilevile kuna wadau wengine ambao ni watu binafsi kama hivyo akina Mzee Mengi, *NGOs* na Taasisi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ujumla ninaomba nimpongeze Dkt. Mengi pamoja na watu wengine wote ambao wanahamasisha *SACCOS* kwa lengo la kuwakomboa Watanzania kutoka kwenye wimbi la umaskini na kuzifanikisha *SACCOS* hizo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niwapongeze na kuwahamasisha wadau wote wa *SACCOS,* waendelee kuzipa msukumo ambapo Serikali tutashirikiana na wadau wengine kama nilivyosema mwanzo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Ngoja tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Mheshimiwa Leticia Nyerere anauliza swali hilo. Nani anayeuliza kwa niaba yake? Mheshimiwa Paresso!

Na. 63

**Udhibiti wa Maambukizi ya Ugonjwa wa Ebola**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. LETICIA M. NYERERE)** aliuliza:-

Wapo raia wa baadhi ya nchi zilizokumbwa na Ugonjwa wa Ebola kama vile Liberia, Sierra Leone, Guinea na kadhalika; ambao wanaingia nchini kwa kutumia au kuunganisha safari na ndege za mataifa mengine:-

(a) Je, Serikali imetoa utaratibu gani wa ukaguzi wa ndege na abiria wanaoweza kuingia nchini kwa kutumia ndege za nchi nyingine?

(b) Je, Tanzania inadhibiti vipi mipaka yetu ya nchi kavu na ile ya majini?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa mwongozo kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa homa wakati wa kuingia nchini *(Screening Protocol for Ebola Hemorrhagic Fever at Point of Entry)* na unatumika kutambua wasafiri wanaotoka katika nchi zenye maambukizi ya Ebola. Mwongozo huu unatekelezwa kwa pamoja na Maafisa kutoka Sekta ya Afya, Uhamiaji na Uongozi wa Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mwongozo huu, ndege zote zimeelekezwa kuhakikisha ujazaji wa fomu maalum unafanyika kwa wasafiri ndani ya ndege na kueleza endapo wametoka au kutembelea nchi zenye maambukizi ya Ebola katika kipindi cha siku 21 kabla ya safari kuja Tanzania. Aidha, wasafiri wote watokapo kwenye ndege hupita kwenye kipima joto *(thermo scanner)* na baadaye kwa Maafisa wa Afya, kuulizwa maswali yanayolenga kubainisha iwapo wametoka katika nchi hizo. Hatua ya mwisho, Maafisa wa Uhamiaji hukagua upya hati za kusafiria kubaini safari zilizofanyika katika kipindi cha siku 21. Endapo itagundulika kuwa abiria ametoka katika maeneo yenye Ugonjwa wa Ebola, hurejeshwa kwa Maafisa wa Afya kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ushiriki wa sekta mbalimbali na kudhibiti ugonjwa usiingie nchini, Ofisi ya Waziri Mkuu iliratibu mkutano wa wadau mnamo Januari, 2015 ambapo sekta zote na wadau kwa ujumla zilikumbushwa kuendelea kushirikiana katika kudhibiti Ugonjwa wa Ebola usiingie nchini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha ufuatiliaji katika mipaka ya nchi majini na nchi kavu. Utaratibu unaotumika ni sawa na ule wa vituo vikubwa vya ndege. Vipima joto *(thermo scanners*), vimesambazwa katika vituo vya mipakani ikiwemo mipaka ya nchi kavu na bandari kama Horohoro, Kabanga, Sirari, Namanga, Tunduma na Bandari ya Kigoma. Aidha, vyombo vya majini huwasilisha taarifa za hali ya afya za mabaharia na wasafiri kabla ya meli kutia nanga kupitia fomu maalum iitwayo "*Maritime Declaration of Health*." Serikali pia imeimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa Ugonjwa wa Ebola kwa ngazi ya jamii kwa lengo la kuhakikisha kuna utambuzi madhubuti wa wasafiri iwapo wamepitia maeneo ya mipaka isiyo rasmi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Katika majibu haya ya Waziri ameeleza kwamba, abiria wanaoingia katika viwanja vya ndege wakigundulika wana maambukizi ya Ebola hurejeshwa katika nchi husika.

(i) Tunapenda kupata taarifa ni watu wangapi mpaka leo wametambuliwa na kurejeshwa katika nchi zao?

(ii) Serikali hii imekuwa haina mikakati ya kudhibiti magonjwa ya milipuko yanayotokea. Kwa mfano, Ebola wamekuwa wakitoa matangazo mbalimbali ya kuelimisha Wananchi lakini haya matangazo ni kama yamesimama, wanasubiri tena mpaka janga lianze kuibuka ndiyo wanakumbuka tena kuelimisha Wananchi. Je, kwa nini hamna mikakati ya muda mfupi na ya kudumu ya kutoa elimu kwa Wananchi ili waweze kuepukana na magonjwa ya milipuko?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Ninadhani Mheshimiwa Mbunge hakunisikia sawasawa, katika jibu la msingi nimesema msafiri anapobainika kwamba, ametokea kwenye nchi ambazo zina maambukizi, huyu ndiyo baada ya pasipoti yake kukaguliwa na Maafisa Uhamiaji, anarejeshwa kwa Wataalamu wa Afya wa kwetu kwa ajili ya mahojiano zaidi.

Mheshimiwa Spika, maelekezo ya Shirika la Afya Duniani hayaruhusu msafiri au mgonjwa kurejeshwa huko alikotoka, isipokuwa matibabu na hatua zote za kum-*isolate* zinafanyika hapo hapo ambapo atakuwa ametambulika kwamba anao ugonjwa au ana dalili za Ugonjwa wa Ebola.

Kuhusu matangazo na mkakati ni kweli kwamba, matangazo yanaendelea, vipeperushi mbalimbali vimetolewa na sasa hivi upo utaratibu ambao utaanza kutumika mwezi huu kwamba; tumeweka kwenye *push mobile*, mtu yeyote mahali popote nchini atakayemwona mtu mwenye dalili hizi za kuwa na Ebola, basi anaweza kupiga simu bila ya gharama yoyote kwa namba maalum ili watu wa afya waweze kuchukua hatua mara moja.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba swali lilikuwa linahusu masuala ya Ebola, lakini hapa Tanzania tuna tatizo kubwa sana la *Yellow Fever*. Wakati ambapo tunapaswa kuchomwa chanjo hiyo, Watanzania wengi hawachanjwi wakati wanaposafiri na matokeo yake matapeli wengi wanakuwa wanauza zile kadi bila ya Watanzania kuchomwa chanjo hizo.

Je, Serikali inalijua hilo na inatoa tamko gani kwa sababu hata ukifika Airport unaonyeshwa ile kadi ili uinunue? Ninaomba kujua kwa sababu kuna nchi zingine wana masharti magumu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Hii mikato mikato ya kupata *documents* za namna hii ni jambo ambalo halishauriwi kabisa. Siyo tu kwamba wewe unayetumia mikato hiyo unakuwa unajiweka katika hatari mwenyewe, lakini pia unapeleka hatari katika nchi unayokwenda. Kwa hiyo, ninaomba kutoa ushauri kwamba, Watanzania wanaosafiri kwenda nchi ambazo bado zina mahitaji ya kwenda na Kadi za Chanjo za *Yellow Fever,* wasitumie njia za mikato. Safari hizi siyo za ghafla, kwa hiyo, atumie utaratibu wa kawaida kwenda katika Vituo vya Afya apimwe, apewe utaratibu wa chanjo na apewe kadi kama taratibu zinavyotaka.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi nilitaka kujua kutokana na matatizo ya mazingira Duniani sasa hivi, ndege zote zikitoka Tanzania kuna masharti ya ndege hizi ambayo imeipa Tanzania kuwa ndege hizi zinanyunyiziwa dawa kabla hazijaondoka nchini kwetu kwenda nchini mwao.

(i) Je, wakati ndege hizi zinakuja nchini mwetu mbona hatuoni masharti ya Tanzania kuwawekea nchi hizo nazo ndege zinyunyiziwe dawa kabla hazijaja kwenye *air space* au viwanja vyetu?

(ii) Je, Serikali sasa itachukua hatua gani ya kulazimisha nchi hizo kabla ya ndege zao kuingia nchini mwetu nazo zinyunyiziwe dawa kama tunavyofanyiwa sisi zikitoka hapa?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, suala hili la kunyunyizia dawa kwenye ndege zinapoingia au zinapotoka nchini hapa ni suala la kiafya na ni hatua inayochukuliwa kwa tahadhali ya kuua wadudu wanaoweza kuhamisha maradhi kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Sasa hivi Mashirika mengi yanayokuja au kuondoka hapa nchini, wanafanya hivyo hivyo, wanapuliza ile dawa baada kuondoka kwa muda mfupi na ni utaratibu ambao wanashauriwa wote kufanya namna hiyo.

**SPIKA:** Ahsante tunaendelea na Wizara ya Ujenzi; Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, kwa niaba yake Mheshimiwa Omari Nundu.

Na. 65

**Kivuko Wilaya ya Pangani**

**MHE.OMARI R. NUNDU (K.n.y. MHE. SALEH AHMED PAMBA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kuipatia Wilaya ya Pangani Kivuko cha pili:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezeka?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Ujenzi ilikamilisha ununuzi wa Kivuko kipya cha Pangani II, chenye uwezo wa kubeba tani 50, yaani magari madogo 6 na abiria 100, mwezi Aprili, 2010. Kivuko hicho kinaendelea kuhudumia Wananchi wa Pangani bila matatizo. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara imetenga fedha kutoka katika Mfuko wa Barabara kwa ajili ya kununua kivuko kipya cha pili ili Wananchi wa Pangani wawe na vivuko viwili kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

Wakala wa Ufundi na Umeme *(TEMESA)*, unaendelea na uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kujenga kivuko hicho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Nundu, swali la nyongeza kwa ufupi.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Ninamshukuru Naibu Waziri kwa maswali mazuri hasa kwa kutukumbusha kuwa mwaka 2010 tulijengewa Kivuko pale. Nitaka kujua hasa kwa kuwa mmesema kwamba mmetenga fedha kwa mwaka huu wa fedha za kununua au kujenga kivuko kipya.

(i) Ninataka kujua na mwaka unamalizika huu. Kivuko hicho cha pili kitapatikana lini? Hilo ndiyo swali langu la kwanza.

(ii) Pangani sasa hivi inachanganya na hata vivuko hivi viwili vikijengwa bado kuna suala la barabara ya kuiunganisha Pangani na Tanzania na Dunia ambapo hakuna hata barabara moja ya lami. Pamoja na kuwa barabara inayotegemewa kujengwa ina urefu wa kilomita zaidi ya 200 ukichanganya na mabadiliko yaliyotokea lakini Tanga mpaka Pangani ni kilomita 50 tu. Tunachoomba; kwa nini Serikali isikipe kipaumbele kipande kile cha Tanga mpaka Pangani ili Pangani nayo iwe imeunganishwa na sehemu za Dunia kwa barabara ya lami kutokea Tanga? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, mchakato wa ununuzi wa kivuko hiki umeshaanza maana *tender* zimeshatangazwa na sasa tunafanya uchambuzi. Tutakapokamilisha zoezi hili tutaendelea na hatua ya kusaini mkataba na kuagiza kianze kujengwa.

La pili, ni kuhusu Barabara ya Tanga – Pangani kwamba ipewe kipaumbele. Serikali imeshatoa kipaumbele na barabara hii imeshafanyiwa usanifu umekamilika. Hivi sasa tumeweka Mradi huu katika Miradi ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili iweze kufadhiliwa na iweze kujengwa. Mara fedha zitakapopatikana, kazi hiyo ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami itaanza.

**SPIKA:** Swali linalofuata Mheshimiwa Dkt. David Malolle na kwa niaba yake Mheshimiwa Lusinde!

Na. 66

**Ujenzi wa Barabara ya Ihumwa - Hombolo**

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE (K.n.y. MHE. DKT. DAVID M. MALOLLE)** aliuliza:-

Serikali imejenga chuo kizuri cha kisasa huko Hombolo lakini barabara za kufika chuoni hapo ni mbovu sana:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara kutoka Ihumwa – Hombolo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa David Mciwa Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Ihumwa – Hombolo ni sehemu ya Barabara ya Mkoa wa Ihumwa - Hombolo - Gawaye - Mayamaya, yenye urefu wa kilomita 55.75 inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabarani nchini *(TANROADS)*.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti ya Hospitali pamoja na kuzingatia vipaumbele vya Serikali vilivyopo hivi sasa, Serikali haina mpango wa kujenga barabara hiyo ya lami kutoka Ihumwa mpaka Hombolo. Wizara ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* itaendelea kuifanyia matengenezo mbalimbali barabara hii kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika kwa urahisi wakati wote wa mwaka hadi hapo uwezo wa Serikali kifedha utakaporuhusu.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Dkt. David Mciwa Mallole, Mbunge, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza niipongeze Serikali kwa ujenzi wa barabara za lami katikakati ya Manispaa ya Dodoma. Nina maswali mawili ya nyongeza yafuatayo:-

(i) Bajeti ya kuitengeneza barabara ile kila mwaka kwa kiwango cha changarawe na kwa sababu asili ya udongo wa pale ni mwepesi sana kuyeyuka, ina inaigharimu Serikali pesa nyingi. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka ianze kudunduliza na kuitengeneza taratibu taratibu barabara ile ili mwisho wa siku iweze kukamilika yote badala ya kusubiri pesa nyingi kuweza kuitengeneza wakati yenyewe haina uwezo?

(ii) Serikali ina mpango gani kuzimalizia barabara zinazozunguka Manispaa ya Dodoma Mjini; kwa mfano, inayotoka Ipagala kuzunguka kupitia African Dream, inayopita kwenye makazi ya Mheshimiwa Spika; kwa nini Serikali haizimalizii hizi barabara ili kuturahisishia Wakazi wa Mkoa wa Dodoma kuweza kupata barabara za lami za uhakika? Ahsante.

**SPIKA:** Umekuwa mwanifu kweli kwa Mheshimiwa. Tunaomba majibu Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Lusinde, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninaomba nizipokee shukrani zako na pongezi kwa Serikali, kwa kazi ambayo inaendelea kufanyika katika ujenzi wa barabara nchini. Swali lake la kwamba fedha za matengenezo ambazo tunazitumia kila mwaka kwa barabara hiyo kwa kuweka changarawe ni nyingi; ni kweli na ndiyo maana tumeweza kuainisha barabara hizi tumezitengea Mfuko Maalum wa Barabara ili tuhakikishe kwamba zinapitika.

Lengo la Serikali jinsi tunavyoweza kupanua uchumi ni kuzijenga barabara zote hizi ziwe za lami. Sasa haya ninasema tutayafanya kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Swali lako la pili kuhusu Barabara za Dodoma Mjini ni kazi ambayo inaendelea. Tulikuwa na Mradi uliofadhiliwa na Benki ya Dunia *Phase* ya Kwanza na sasa tunaendelea ku-*negotiate* tupate *Phase* nyingine tuweze kuzijenga hizo barabara ambazo zimebakia katika Mji wa Dodoma.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wenyewe umeisha na maswali yameisha. Ninaomba niwatambue baadhi ya wageni tulionao humu ndani.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni wa Mheshimiwa Pindi Chana, Naibu Waziri Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ambao ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Jumuiya ya Wazazi kutoka Mikoa ya Njombe, Kilimanjaro, Iringa na Mwanza, wakiongozwa na Ndugu Evarist Lupenza. Ninaomba wasimame hapo walipo wote kama wapo.

Majina yote yale kumbe wako wachache tu! Karibuni sana wageni. *(Kicheko)*

Wapo wageni 11 wa Mheshimiwa Amina Makilagi, ambao ni kundi la viziwi kutoka Dar es Salaam, wakiongozwa na Ndugu Tungi Mwanjala. Wasimame walipo; ahsante sana na karibuni. Tunafurahi kuwaoneni, sijui kama tafsiri ipo siku hizi? Imeshaondoka hapa.

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Suleiman Jafo, ambaye ni Ndugu Mohamed Salum.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Tundu Lissu, ambao ni Mchungaji Jeremiah Samwel Mpefo na Ndugu Joseph Noah Maji, kutoka Kanisa la *FPCT* Ikungi. Ninaomba Wachungaji hao wasimame walipo; ahsante ni sana na karibuni.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao ni Waheshimiwa Madiwani 19 wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, wakiongozwa na Makamu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi. Ninaomba hawa nao wasimame walipo; ahsanteni sana, karibuni sana.

Tuna wageni sijui ndiyo hawahawa wameongozana, kuna Viongozi wanne wa *VICOBA*, madereva wawili na Katibu wa Mbunge wa Mufindi Kaskazini. Hawa *VICOBA* nao wasimame. Mmesimama pamoja *okay,* ahsante sana. Leo swali la *VICOBA* lilikuwepo hapa, ninadhani mmefaidika nalo.

Tuna wageni waliokuja kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Waheshimiwa ninaomba msijifanye kama mko nje nitawajata! Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ninakusikiliza wewe.

Tuna wanafunzi 200 na walimu kumi kutoka Shule ya Msdingi Mount Evarest iliyopo Mbweni Dar es Salaam. Ninaomba wanafunzi hao wasimame; ahsante sana na karibuni sana. Mmependeza sana na msome vizuri.

Tuna Wanakamati kumi kutoka Taasisi ya Imetosha, inayohamasisha kupinga unyanyapaa na mauaji dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Ninaomba wasimame walipo; ahsante sana.

Hawa ndugu Jumapili ijayo, ninadhani tarehe 29, watafanya matembezi ya hisani na mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mathias Chikawe. Ninadhani ni mwaliko kwa wale watakaoweza washirikiane nao katika hayo matembezi ya hisani siku hiyo ya tarehe 29, ninadhani habari zaidi mtazieleza.

Tuna wageni watano kutoka Kampuni ya Tanzania Awards Intertional Ltd, ambayo inajihusisha na utoaji wa tuzo ya jamii kwa taasisi na watu binafsi, wakiongozwa na ndugu Deonatus Julius Maregesi, Mwenyekiti. Wasimame walipo; ahsante sana. Ninadhani hiki kitu bado hatukijui vizuri, labda mtatumia nafasi hii kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge.

Matangazo ya kazi; ninafanya protokali ninaanza na Wenyeviti kwanza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa tano wamepewa ruhusa hawa watakuwa na kikao cha Kamati ya Bajeti katika ukumbi ambao wao wanaufahamu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa C.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba mchana, watakuwa na kikao chao katika Ukumbi wa Msekwa. Ninaomba hao wanaohusika waendelee.

Katibu, hatua inayofuata.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, lakini msifanye kama ni *fashion, is not a fashion,* haiko kwenye Kanuni kila baada ya maswali Mwongozo wa Spika. Mheshimiwa Mnyika!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 47 (4) inayosema; iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura halisi na lina masilahi kwa Umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa.

Katika Mkutano uliopita wa Bunge, Mheshimiwa James Mbatia, alitoa hoja ya dharura juu ya suala la uandikishaji wa wapiga kura katika Mfumo wa BVR. Kwa busara zako ukaona jambo lile lisijadiliwe bali lipelekwe kwenye Kamati ya Uongozi lishughulikiwe. Kamati ya Uongozi ikafanya uamuzi kwenye mambo mawili; moja, Tume kuweza kukutana na wadau kupitia *TCD* pamoja na wadau wengine. Pili, Tume kuweza kukutana na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ili hatimaye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ikimaliza kazi yake, basi Bunge liweze kutaarifiwa na hatimaye hatua za mjadala ziendelee na hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nimesimama muda huu kwa sababu jambo hili limeendeleza tena sintofahamu wakati huu tunapozungumza. Jana katika Jimbo la Njombe Mjini na Majimbo mengine ya Mkoa wa Njombe, ilipofika jioni kwenye zoezi la uandikishaji, Wananchi waliambiwa hakuna vifaa, baadhi ya vifaa vimeisha, hivyo waandike majina yao pembeni waendelee leo asubuhi. Taarifa nilizozipata leo asubuhi, Wananchi hao wameambiwa hawawezi kujiandikisha na uandikishaji unaisha siku ya leo.

Wakati Wananchi hawa wakiendelea kutakiwa kupata mwongozo wa Kibunge utakaowezesha siku kuongezwa jambo hili kufanyika, kuna ukweli mwingine ambao upo nyuma ya pazia ambao Serikali haitaki kuusema waziwazi kwamba; mpaka sasa hivi ninavyozungumza, taarifa ambayo Serikali iliitoa kwamba waliagiza mashine 2,100 hazikuwa za kweli, mashine ambazo wameagiza mpaka sasa ni 800. Utaratibu waliokubaliana na kampuni ya South Africa inayohusika na kuwa wakala ni kwamba, mashine za ziada zikihitajika, huyo wakala hata kama

akilipwa anatakiwa a-*press order* kwa mtu mwingine, kwa hiyo, mashine haziwezi kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, sasa Mkoa wa Njombe peke yake kwa hali hii taarifa za ndani zinaonesha kwamba, uandikishaji Njombe peke yake utakwenda mpaka tarehe 28 mwezi Aprili. Hata kama hizi mashine zikija sasa hivi, kwa taarifa za ndani inaonesha vilevle kwamba, uandikishaji kwa vyovyote vile kama ni nchi nzima, hauwezi kukamilika kabla ya mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, kuna sintofahamu ya Wananchi wa Njombe ambao wanakoseshwa haki ya kujiandikisha; kuna sintofahamu ya Watanzania kwa ujumla wake, ambao hawajui ratiba na wataandikishwa lini; kuna sintofahamu ya kwamba, je, Katiba Inayopendekezwa kura ya maoni itafanyika kweli tarehe 30 Aprili huku kukiwa hakuna uhakika wa uandikishaji!

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako ili sasa Bunge lipewe taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo ilikwenda kufanya kazi kwa niaba ya Bunge, jambo hili lijadiliwe na Bunge lipitishe maamuzi ya kuwanusuru Wananchi na kadhia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.

**SPIKA:** Mwongozo huu utajibiwa wakati mwafaka, tunaendelea.

Katibu, hatua inayofuata.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa wa Mwaka 2015
### *(The National Payment Systems Bill, 2015)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja!

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni inasema, Spika anaweza kujibu Mwongozo mara moja au wakati mwingine, ndiyo maana nikasema tutakujibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa wa Mwaka 2015 *(The National Payment Systems Bill, 2015),* pamoja na marekebisho yake, sasa usomwe kwa Mara ya Pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mbunge wa Kisesa, kwa kuujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri katika vikao vilivyofanyika Dar es Salaam na Dodoma mwezi Machi, 2015. Vilevile tunawashukuru wadau na washauri mbalimbali ambao kwa nyakati tofauti wametoa ushauri na mapendekezo yao kwa lengo la kuuboresha Muswada huu. Aidha, namshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalam wake, kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonyesha wakati wa maandalizi ya Muswada huu.

Naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada huu umezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Uchumi pamoja na ushauri wa wadau wengine ambao wametoa kuhusiana na Muswada huu.

**SPIKA:** Wanaotoka watoke *quietly!*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, chimbuko la Muswada huu ni matokeo ya maboresho yaliyofanywa na Serikali katika Sekta ya Fedha nchini ambayo yalianza miaka ya tisini na yanayoendelea hadi hivi sasa. Maboresho katika Sekta ya Fedha yalisababishwa kutungwa kwa sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006 na Sheria ya Benki Kuu ya Mwaka 2006. Maboresho haya yameruhusu kuanzishwa kwa benki binafsi na taasisi mbalimbali za fedha na hivyo kuifanya Sekta ya Fedha kukua na kusababisha mabadiliko katika utoaji wa huduma zake ambapo hivi sasa benki na taasisi za kifedha hutoa huduma kwa kutumia mifumo ya malipo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kupitisha Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Mwaka 2003 pamoja na kutungwa kwa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Nchini *(TCRA)* na kutungwa kwa Sheria ya *Electronic and Postal Communications Act, 2010*, kumekuwa na ongezeko kubwa la kampuni za mawasiliano hapa nchini ambazo nyingi hujishughulisha na utoaji huduma za kifedha kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maendeleo haya ya kiteknolojia katika Sekta ya Fedha, zipo changamoto nyingi zilizojitokeza katika kusimamia mifumo ya malipo nchini, ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Changamoto kubwa iliyopo hivi sasa ni kutokuwepo kwa sheria moja mahususi inayobainisha na kusimamia masuala yafuatayo:-

(i) Utaratibu unaotumika kuhaulisha malipo;

(ii) Nyenzo za malipo ya kielektroniki;

(iii) Wajibu wa watoa huduma za mifumo ya malipo hususan kwa taasisi zisizo za kifedha;

(iv) Haki za watumiaji wa huduma za malipo;

(v) Usiri na utunzaji wa takwimu za kielektroniki za mteja;

(vi) Ulinzi wa watoa huduma, yaani taasisi zisizo za kifedha na wateja dhidi ya athari zitokanazo na kufilisika kwa mtoa huduma (*insolvency*);

(vii) Utaratibu wa kuendesha akaunti ya udhamini kwa huduma za kifedha kwa njia ya kutumia simu za kiganjani;

(viii) Utaratibu wa kutoa fedha za kielektroniki, yaani *e-money*, kwa watoa huduma za mifumo ya malipo na makosa ya jinai na ya matumizi ya mitandai, yaani *cyber crime* katika mifumo ya malipo ikiwemo adhabu kwa watakaofanya makosa.

Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto hizo, Serikali inapendekeza kutungwa kwa Sheria Mahususi ya Mifumo ya Malipo Nchini, 2015. Sheria hii inakusudia kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Benki Kuu kupewa mamlaka kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini;

(ii) Kuweka utaratibu wa kusimamia na kudhibiti watoa huduma wa mifumo ya malipo nchini;

(iii) Kuweka utaratibu wa utambuzi wa nyenzo za kielektroniki zinazotumika katika uhaulishaji wa fedha katika mifumo ya malipo nchini;

(iv) Kusaidia katika kuendeleza, kuboresha na kufanikisha mifumo ya malipo kwa lengo la kukidhi haja na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayotokea nchini kutokana na kutumia teknolojia ya mawasiliano katika uhaulishaji wa fedha baina ya taasisi mbalimbali na wananchi na;

(v) Kutoa adhabu kali kwa watakaokiuka masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Spika, nchi washirika wenzetu zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za *SADC*, tayari zimetunga sheria za mifumo ya malipo ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika mifumo yao ya malipo. Hadi hivi sasa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetunga Sheria ya Mifumo ya Malipo ni Kenya mwaka 2011, Rwanda mwaka 2010. Katika nchi za *SADC,* Afrika Kusini ilitunga Sheria hii mwaka 1998, Zimbambwe mwaka 2001, Botswana na Namibia mwaka 2003, Zambia mwaka 2007 na Msumbiji mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo ni utaratibu unaowezesha uhaulishaji wa fedha kutoka kwa mtumiaji mmoja kwenda kwa mwingine katika uchumi kwa kutumia nyenzo za malipo zinazotumia taratibu za Taasisi za Fedha. Mifumo ya malipo inayotumika Tanzania imegawanyika katika aina mbili kulingana na viwango vya fedha zinazohaulishwa. Aina ya kwanza ni mfumo wa malipo wa viwango vya juu (*high value*) ambavyo ni zaidi ya shilingi milioni kumi au Dola za Kimarekani elfu kumi. Aina ya pili ni mfumo wa malipo wa viwango vya chini *(low value)* ambavyo havizidi shilingi milioni kumi au chini ya Dola za Kimarekani elfu kumi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo ya viwango vya juu unaotumika Tanzania ni *Tanzania Interbank Settlement System (TISS),* ambao ulianza kutumika mwezi Aprili, 2004. Mfumo huu ni mfumo wa kielektroniki unaounganisha Benki za Biashara na Benki Kuu ya Tanzania kwa njia ya mtandao ili kuwezesha uhaulishaji wa fedha kwa uharaka *(real time)*. Aidha, mfumo huu unatumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Bodi ya Mapato ya Zanzibar. Vilevile hivi sasa Serikali inafanya malipo yake kwa kutumia mfumo wa *TISS* kupitia Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo ya viwango vya chini unaotumika Tanzania unajumuisha malipo ya hundi *(electronic clearing house)*, malipo kwa njia ya muamala na kadi *(card payment switches)*, huduma za kibenki kwa njia ya mtandao *(internet banking)*, malipo kwa njia ya simu za kiganjani *(mobile phone payments)* na huduma za kutuma fedha *(remittance services)*.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa malipo ya hundi (*Electronic Clearing House au ECH),* ulianza kutumika mwaka 2003 na umewezesha kupunguza siku za kupata fedha kwa mteja kutoka siku 24 hadi siku tano. Aidha, malipo kwa njia ya simu za kiganjani yalianza mwaka 2008 kuanzia na mtandao wa *Vodacom (M-Pesa),* baadaye mitandao mingine kama vile *Tigo (Tigo Pesa), Zantel (Ezypesa)* na *Airtel (Airtel Money),* nayo ilianza kutoa huduma hiyo. Utaratibu huo wa malipo unatumika kuhaulisha fedha pamoja na kulipia ankara za huduma mbalimbali kama vile maji na umeme.

Mheshimiwa Spika, huduma ya malipo kwa njia ya simu za kiganjani imewezesha Wananchi wengi ambao walikuwa hawapati huduma za kifedha kufikiwa na huduma ya kutuma na kupokea fedha. Hadi kufikia Novemba 2014, Wananchi zaidi ya milioni 15, sawa na asilimia 60 ya watu wazima, wanatumia huduma hii. Aidha, akaunti za huduma za fedha na za simu za kiganjani zilizoandikishwa zinafikia milioni 40.

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni:-

(i) Kuboresha usimamizi, kuongeza udhibiti na kuimarisha mifumo ya malipo nchini;

(ii) Kuiweka nchi katika mazingira mazuri ya ushindani wa kibiashara;

(iii) Kudhibiti changamoto zinazoweza kutokea katika sekta ya fedha na kutengeneza mazingira bora ya kiufanisi katika mifumo ya malipo nchini;

(iv) Kuzuia na kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza katika mifumo ya malipo.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya mambo muhimu ambayo tumeyazingatia katika Muswada huu:-

1. Mamlaka ya Benki Kuu katika kusimamia mifumo ya malipo nchini;

2. Kuweka utaratibu wa kutambua nyenzo za kieletroniki za kuhaulisha malipo;

3. Kuweka utaratibu wa kutoa leseni kwa watoa huduma ya mifumo ya malipo;
4. Kuainisha utaratibu wa kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki na namna ya kufikia utimilifu wa malipo hayo;

5. Mamlaka ya Benki Kuu ya Tanzania katika kuandaa kanuni na taratibu za kusimamia mifumo ya malipo nchini;

6. Kulinda watumiaji wa huduma za malipo ya kielektroniki dhidi ya athari zitokanazo na ufilisi wa mtoa huduma kwa kutoa kipaumbele kwa malipo ya mteja;

7. Kutambua utaratibu wa kutoa dhamana katika mifumo ya malipo ambapo Benki Kuu itaweka utaratibu wa kutunza fedha kama dhamana kwa ajili ya kudhamini madeni au majukumu ya mshiriki malipo pindi atakaposhindwa kutimiza wajibu wake wa kuhitimisha malipo;

8. Kulinda siri na utunzani wa takwimu za kielektroniki za mtoa huduma ambapo taarifa zitatolewa tu pale ambapo zinahitajika kwa mujibu wa sheria;

9. Kuweka utaratibu wa kuendesha akaunti ya udhamini hususan kwa huduma za uhaulishaji wa fedha kwa njia ya kutumia simu za kiganjani;

10. Kuweka utaratibu wa kutoa fedha za kielektroniki kwa watoa huduma za mifumo ya malipo;

11. Kudhibiti uhalifu wa kielektroniki katika mifumo ya malipo;

12. Kuweka adhabu kwa watakaokiuka sheria hii; na

13. Kubainisha ushirikiano wa wasimamizi wa sekta ya fedha na taasisi nyingine za Serikali katika mfumo wa malipo nchini.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu 12 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza yenye Ibara ya Kwanza hadi ya Tatu, inabainisha masharti ya awali, jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria ambapo Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha ataitangaza kupitia Gazeti la Serikali na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika sheria.

Sehemu ya Pili yenye Ibara ya Nnekama ilivyofanyiwa marekebisho, inaainisha mamlaka na majukumu mbalimbali ya Benki Kuu ya Tanzania kuhusu usimamizi na udhibiti wa mifumo ya malipo ya kielektroniki. Kupitia Jedwali la Marekebisho, Ibara ndogo ya (2) inayohusu Gavana wa Benki Kuu kufanya mashauriano na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha wakati wa utekelezaji wa majukumu yake na kuwasilisha taarifa kwa Waziri wa Fedha kuhusu mifumo ya malipo ya kielektroniki imefutwa, ili kumwezesha Gavana kutekeleza majukumu yake ya kiutendaji kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu yenye Ibara ya Tano ha Ibara ya 14 kama ilivyorekebishwa inaainisha sharti la kutoendesha mfumo wa malipo bila leseni, vigezo na sifa zinazopaswa kuzingatiwa ili kupata leseni ya mfumo wa malipo, taratibu za uwasilishaji wa maombi ya leseni ya mfumo wa malipo na uendeshaji wake.

Sehemu hii inabainisha mazingira yatakayosababisha kusimamishwa na kufutwa kwa leseni ya mfumo wa malipo ambapo kupitia Jedwali la Marekebisho, Ibara ya 10(2), imefanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa Benki Kuu kutoa *notice* ya siku saba kabla ya kufuta leseni. Aidha, pale ambapo leseni imefutwa kwa mujibu wa sheria, Benki Kuu itatoa taarifa kwa umma kuhusu ufutwaji huo kupitia vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, aidha, sehemu hii pia inabainisha makosa yatokanayo na kukiuka masharti yaliyobainishwa katika eneo hili pamoja na adhabu zake ambapo kupitia Jedwali la Marekebisho Ibara ya 14(a) na (b) imefanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kuwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka mitano au faini na kifungo kwa mtu binafsi badala ya faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka mitano au kifungo na faini kwa pamoja kama ilivyobainishwa kwa Muswada hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, adhabu kwa kampuni imefanyiwa marekebisho na kuwa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano kwa kampuni, badala ya faini isiyozidi shilingi milioni hamsini kwa kampuni kama vile ilivyopendekezwa awali kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nne yenye Ibara ya 15 hadi Ibara ya 20 kama ilivyorekebishwa, inaainisha sharti la kutotoa nyenzo za malipo ya kielektroniki bila leseni au idhini iliyotolewa na Benki Kuu, sifa stahiki za nyenzo za malipo na taratibu za kuwasilisha maombi ya upatikanaji wa leseni za kutoa nyenzo za malipo, taratibu za kusimamisha na kufuta leseni za kutoa nyenzo za malipo.

Hata hivyo, kabla ya kufuta au kusimamishwa kwa leseni husika, mhusika anaweza kupewa nafasi ya kuwasilisha utetezi wake. Aidha, sehemu hii inabainisha adhabu kwa mtu au kampuni itakayokiuka masharti yaliyobainishwa katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kupitia Jedwali la Marekebisho, Ibara ya 19(2) imefanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa Benki Kuu kutoa *notice* ya siku saba kabla ya kufuta leseni au idhini ya kutoa nyenzo za malipo. Vilevile, sehemu hii imefanyiwa marekebisho katika Ibara ya 20(a) na (b) inayohusu makosa ya kukiuka masharti ya sehemu hii kwa kuongeza adhabu kuwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka mitano, au faini na kifungo kwa pamoja kwa mtu binafsi, badala ya faini isiyozidi shilingi milioni kumi au

kifungo kisichozidi miaka mitano au kifungo na faini kwa pamoja kama ilivyobainishwa kwa Muswada hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, aidha, adhabu kwa kampuni imefanyiwa marekebisho na kuwa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano kwa kampuni badala ya faini isiyozidi shilingi milioni hamsini kama ilivyopendekezwa awali kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tano yenye Ibara ya 21 hadi Ibara ya 23, inaainisha namna uwasilishaji wa hundi kwa njia za kielektroniki na kukubalika kwa hundi au kivuli cha nakala ya hundi iliyothibitishwa katika ushahidi kwenye shauri lililopo Mahakamani na Vyombo vinginevyo vya Kimahakama.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Sita yenye Ibara ya 24 hadi Ibara ya 31 inaainisha sharti la kutotoa fedha kielektroniki bila leseni au idhini ya Benki Kuu, utaratibu wa kuwasilisha maombi ya leseni au idhini ya utoaji wa fedha za kielektroniki, usimamishaji au ufutaji wa muda wa leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki, makosa na adhabu chini ya sehemu. Aidha, marekebisho yamefanyika katika sehemu hii kupitia Jedwali la Marekebisho ambapo kwanza, Ibara ya 29(2) imefanyiwa marekebisho ili kuweka sharti kwa Benki Kuu kutoa *notice* ya siku saba kabla ya kufuta leseni au kusimamisha idhini ya utoaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki.

Pili, Ibara ya 30 Kifungu cha 1(c) imefanyiwa marekebisho ili kubainisha kwamba, orodha ya majina ya wateja yaliyopo katika mfumo wa malipo iwasilishwe kwenye Benki zinazotunza akaunti ya fedha za udhamini badala ya orodha hiyo kuwasilishwa Benki Kuu ambayo haihusiki na utunzaji wa akaunti za wateja.

Mheshimiwa Spika, tatu, kurekebisha Ibara ya 31 ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayekiuka masharti ya sehemu hii kuwa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini au kifungo kisichozidi miaka mitano au faini na kifungo kwa pamoja kwa mtu binafsi badala ya faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kifungo kisichozidi miaka miaka mitano au kifungo na faini kwa pamoja kama ilivyobainishwa kwenye Muswada hivi sasa. Adhabu kwa kampuni vilevile imefanyiwa marekebisho na kuwa faini isiyopungua shilingi milioni mia tano kwa kampuni badala ya faini isiyozidi shilingi milioni hamsini kama ilivyopendekezwa awali kwenye Muswada.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Saba yenye Ibara ya 32 hadi Ibara ya 35, inaainisha sharti la kufungua akaunti ya udhamini kwa mtoa huduma ambaye si asasi ya kibenki au taasisi ya kifedha na taratibu za ufunguaji na uendeshaji wa akaunti hiyo.

Ufunguaji wa akaunti maalum kwa mtoa huduma ambaye ni Benki au Taasisi ya Fedha na usimamizi wake. Sehemu hii imefanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho ambapo:-

(i) Ibara ya 34(2)(b) imeandikwa upya ili kubainisha kwamba muundo wa mikataba ya dhamana utabainishwa katika Kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii.

(ii) Ibara ya 34(2), imerekebishwa ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayekiuka masharti ya Ibara ya 34 yanayohusu uendeshaji wa akaunti ya dhamana ambapo adhabu imeongezwa kutoka kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni hamsini.

(iii) Ibara ya 35 kuhusu uendeshaji wa akaunti maalum, imefanyiwa marekebisho katika Ibara ya 35(2) ili kuongeza adhabu ya mtu atakayekiuka masharti ya kifungu hiki kutoka kiasi kisichozidi shilingi milioni kumi hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni hamsini.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Nane yenye Ibara ya 36 na 37, inaainisha ukomo wa malipo na mipango ya uhalisi wa malipo. Aidha, Sehemu hii inabainisha uhalali, nguvu ya kisheria ya utimilifu wa malipo pamoja na uhalisi wa malipo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tisa, yenye Ibara ya 38 – 40, inaainisha utaratibu wa kufunga na kusimamia ufilisi wa kampuni inayotumia mfumo wa malipo ili kuhakikisha maslahi ya walaji yanalindwa wakati wa ufilisi wa kampuni hizo na kipaumbele cha malipo pindi kampuni zinapofilisiwa.

Mheshimkiwa Spika, Sehemu ya Kumi yenye Ibara ya 41 – 42, inaainisha utaratibu wa dhamana kwa ajili ya kudhamini madeni na majukumu ya malipo ya mshiriki wa mfumo wa malipo pindi atakaposhindwa kutimiza wajibu wake na mipango ya kudhibiti kushindwa kufanya utimilifu wa malipo ili kuhakikisha uwepo wa ukwasi wa kutosha kwa ajili ya utimilifu wa malipo na kuondoa hali ya kushindwa kufanya malipo baina ya washiriki wa mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Jedwali la Marekebisho, Ibara ya 41(3) imefanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa mshiriki wa mfumo wa malipo atakayeendesha mfumo wa malipo bila dhamana ya kutosha kutoka faini ya shingi isiyozidi milioni hamsini hadi kiasi kisichopungua shilingi milioni mia tano.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Moja yenye Ibara ya 43 – 57, inaainisha sharti kwa mtoa huduma wa malipo kuwasilisha kwa Benki Kuu marejesho yanayohusu uendeshaji wa mfumo wa malipo na endapo atakiuka sharti hili atalipa *fine* isiyopungua shilingi milioni hamsini. Aidha, Benki Kuu imepewa mamlaka ya kupata taarifa kuhusu mfumo wowote wa malipo na mtu au kampuni itakayoshindwa kuwasilisha taarifa husika italipa *fine*.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii imefanyiwa marekebisho kupitia Jedwali la Marekebisho ambapo:-

(i) Ibara ya 43(3) imefanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa mtu au kampuni itakayoshindwa kuwasilisha Taarifa kutoka *fine* isiyopungua shilingi milioni tano hadi shilingi milioni kumi kwa siku atakayoshindwa kuwasilisha taarifa kuanzia siku anayopaswa kuwasilisha taarifa husika;

(ii) Ibara ya 44(2) inarekebishwa ili kuongeza adhabu kwa mtoa huduma wa malipo atakayeizuia Benki Kuu kupata taarifa ya mfumo wa malipo kutoka *fine* isiyopungua shilingi milioni tano na kuwa adhabu ya kulipa shingi milioni tano kwa siku ambayo kosa hilo litatendeka;

(iii) Ibara ya 46(4) inafanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa mtu atakayeshindwa kutunza kumbukumbu za miamala ya malipo kutoka *fine* isiyopungua shilingi milioni ishirini na kuwa *fine* isiyopungua shilingi milioni mia tano;

(iv) Ibara ya 47(2) imefanyiwa marekebisho ili kuongeza adhabu kwa mtoa huduma za malipo atakayeshindwa kutunza siri za taarifa za mteja kutoka *fine* isiyopungua shilingi milioni hamsini hadi *fine* isiyopungua shilingi milioni mia moja;

(v) Kufanya marekebisho ya kiuandishi katika Ibara ya 50(5) kwa kufuta maneno "*reasonable expenses*" na kuweka maneno "*expenses and payments*" ili kuleta maana iliyokusudiwa; na

(vi) Kurekebisha Ibara ya 57(2) kwa kukiandika upya ili kuwaongeza katika wigo wa adhabu mtu atakayetoa huduma za fedha za ki-*electronic* au huduma zozote za mfumo wa malipo bila leseni, baada ya miezi sita kupita tangu kuanza kutumika kwa sheria hii. Adhabu kwa mtu atakayekiuka masharti hayo ya mpito imeongezwa kutoka *fine* isiyozidi shilingi milioni mia moja na kuwa *fine* isiyopungua shilingi milioni mia tano au kifungo cha miaka mitano au *fine* pamoja na kifungo.

Mheshimiwa Spika, Sehemu hii pia inabainisha masuala ya utunzaji wa kumbukumbu, utunzaji siri wa taarifa za mteja, kumlinda mlaji katika mfumo wa malipo, makosa ya kimtandao katika mfumo wa malipo, ushirikiano baina ya wasimamizi katika mfumo wa malipo, mamlaka ya kutengeneza Kanuni na Sheria Ndogo na Masharti ya Mpito.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Kumi na Mbili yenye Ibara ya 58 - 59 inahusu marekebisho katika vifungu vya 41 na 52 vya Sheria ya Hawala za Fedha, Sura 215 (*Bills of Exchange Cap. 215)*. Lengo la marekebisho katika sheria hii ni kwa ajili ya kuwezesha uhaulishwaji wa hundi kwa njia za ki-*electronic* katika mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Sasa nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuujadili Muswada huu pamoja na marekebisho yake na hatimaye tukubali kuupitisha na kuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Muswada huu au Mwakilishi wake na ni Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kitandula.

Waheshimiwa Wabunge, mnapoongea tunawasikia! Mheshimiwa Rita Mlaki, tunawasikia! *(Kicheko)*

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA VIWANDA, UCHUMI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Aprili, 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini wa Mwaka 2015 (*The National Payment System Act, 2015.*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hapa leo kuwasilisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Machi, 2015, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Kigoma Malima aliwasilisha mbele ya Kamati Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa wa mwaka 2015. Katika maelezo yake Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha aliieleza Kamati kuwa, Muswada huu unakusudia:-

(i) Kuipa Benki Kuu mamlaka ya kisheria ya kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini;

(ii) Kuweka utaratibu wa kisheria wa kusimamia na kudhibiti watoa huduma ya mifumo ya malipo nchini;

(iii) Kuweka utaratibu wa kisheria wa utambuzi wa nyenzo za ki-*electronic* zinazotumika katika uhaulishaji wa fedha katika mifumo ya malipo nchini; na

(iv) Kusaidia katika kuendeleza, kuboresha na kufanikisha mifumo ya malipo kwa lengo la kukidhi haja ya mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayotokea nchini kutokana na kutumia teknolojia ya mawasiliano katika uhaulishaji wa fedha baina ya taasisi mbalimbali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kusikiliza maelezo ya Serikali, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na 117(9) vya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 ambapo tarehe 12 Machi, 2015, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali ili kupata tafsiri ya matokeo ya sheria inayopendekezwa kwa mazingira halisi ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa utaratibu huu uliiwezesha Kamati kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Uzoefu wa kuhusika katika utaratibu utakaotokana na marekebisho haya ya sheria;

(ii) Mahitaji muhimu ya ufanisi na tija katika kutekeleza sheria inayopendekezwa; na

(iii) Umuhimu wa kutokinzana wala kusigana na misingi bora ya sheria zilizoanzisha taasisi zinazoathiriwa kwa sheria ikiwa Bunge litapitisha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa wadau muhimu ambao uzoefu wao ulifanyiwa kazi na Kamati hii ni pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ambazo marekebisho ya sheria zilizomo katika Muswada huu yanawagusa moja kwa moja. Kamati ilitoa mwaliko kwa wafuatao:-

(i) Benki Kuu ya Tanzania;
(ii) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na
(iii) Tume ya Ushindani Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wadau wengine ni kampuni za simu za mikononi pamoja na kampuni mbalimbali zinazotumia mfumo wa malipo kwa njia ya ki-*electronic* ambazo na pamoja na *Vodacom Tanzania, MIC Tanzania Ltd* yaani *Tigo, Airtel Tanzania, Maxicom African Ltd* na *CRDB Bank Ltd.*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, nawashukuru kwa dhati wadau hao wote kwa kuiwezesha Kamati kufanya uchambuzi wa Muswada huu kwa kuzingatia vigezo muhimu katika utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Muswada. Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini wa mwaka 2015 ulipowasilishwa kwenye Kamati ulikuwa na Sehemu kuu kumi na mbili zenye jumla ya Ibara 59. Kamati ilipitia kwa umakini na kufanya uchambuzi wa kina ili kujiridhisha na mambo yote muhimu katika utungaji wa sheria inayokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo muhimu kabla ya kutunga sheria yoyote ni kujiridhisha na umuhimu wa kuwa na sheria husika. Katika kufanya hivyo, Kamati ilirejea historia ya mfumo wa malipo kwa njia ya ki-*electronic* na kubaini kuwa mfumo huu ulianza kutumika nchini tangu mwanzoni mwa mwaka 2000. Hivyo, sheria inayopendekezwa inakusudia kuweka masharti kwa ajili ya udhibiti na usimamizi wa mifumo ya malipo, udhibiti wa nyenzo za ki-

*electronic,* uhaulishaji wa fedha kwa njia ya ki-*electronic,* watoa huduma wa mifumo ya malipo na uhalali wa nguvu ya sheria kwa mipango ya uhalisi wa malipo.

Mheshimiwa Spika, faida za kuanzishwa kwa mfumo wa malipo nchini ni pamoja na:-

(i) Kuongeza fursa za kijamii na kiuchumi na hivyo kuleta maendeleo endelevu;

(ii) Kuongeza usalama katika sekta ya fedha;

(iii) Kuboresha utekelezaji wa Sera ya Uchumi *(Monetory Policy);*

(iv) Kuongeza na kuboresha biashara katika uchumi kwa malipo ya uhakika na salama; na

(v) Kupunguza misongamano isiyo ya lazima katika Ofisi za Serikali, Mabenki na Kampuni za watu binafsi zinazotoa huduma kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kutumika kwa mfumo huu, huduma nyingi za malipo zimekuwa zikifanyika kwa kutumia miamala ya pesa kwa njia ya mtandao. Kwa mfano, kufanya manunuzi ya huduma mbalimbali, kufanya miamala ya kutuma pesa, kuhamisha pesa kutoka benki kwenda kwenye simu au kutoka kwenye simu kwenda kwenye benki, kulipa ada za magari kwa njia ya mtandao, kulipa ankara za maji, umeme na hata kununua bidhaa kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida nilizoeleza hapo juu, kuanzishwa kwa mfumo wa malipo nchini, mfumo huu umekuwa ukitumika kwa zaidi ya miaka 15 bila kuwepo kwa utaratibu wa kisheria. Kamati inaamini uzoefu huu wa karibu miaka 15 utasaidia kuanzishwa kwa sheria itakayobainisha na kusimamia masuala ya msingi yafuatayo:-

(i) Kuweka utaratibu madhubiti utakaotumika kuhaulisha malipo;

(ii) Kuainisha nyenzo za malipo ya ki-*electronic;*

(iii) Sheria itatoa wajibu wa watoa huduma za mifumo ya malipo, hususan kwa taasisi za fedha;

(iv) Sheria itabainisha haki za watumiaji wa huduma za malipo;

(v) Sheria itatoa mwongozo wa namna ya usiri wa utunzaji wa takwimu za ki-*electronic;*

(vi) Sheria itaweka utaratibu wa kuendesha akaunti za udhamini hususan kwa huduma za kifedha kwa njia ya kutumia simu za kiganjani; na

(vii) Sheria itafafanua utaratibu wa ulinzi wa watoa huduma na wateja dhidi ya athari zitokanazo na kufilisika kwa mtoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia faida za kuwa na sheria hii, Kamati inaiopongeza Serikali kwa kuleta pendekezo lenye tija katika udhibiti wa usimamizi wa mifumo ya malipo, udhibiti wa nyenzo za ki-*electronic,* uhaulishaji wa fedha kwa njia ya ki-*electronic,* watoa huduma wa mifumo ya malipo, uhalali wa nguvu ya sheria kwa mipango ya uhalisia wa malipo na masharti mengine yanayohusisha sheria hii inayopendekezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mambo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Kuepusha urasimu usio wa lazima ambao unakwamisha ufanisi katika utekelezaji wa sheria. Kwa mfano, Kamati ilipopitia Ibara ya 4(2), ilibaini kuwa sharti la Gavana kushauriana na Waziri katika utekelezaji wa Ibara ndogo ya (1) linaongeza urasimu usio wa lazima.

(ii) Kuzingangatia misingi ya haki ya asili *(natural justice),* kwa mfano, katika Ibara ya 19 inayohusu ufutaji wa leseni au idhini ya kutoa nyenzo za malipo haikubainisha muda wa *notice* ya kufutwa kwa leseni iwapo mtoa huduma ya mfumo wa malipo hajasababisha tatizo linaloshughulikiwa kwa kufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mambo haya Kamati ilimshauri mtoa hoja kufanya marekebisho katika Ibara zifuatazo:-

(i) Ibara ya 4, mamlaka na majukumu ya Benki Kuu;

(ii) Ibara ya 10 inayohusu ufutaji wa leseni ya mfumo wa malipo;

(iii) Ibara ya 19 inayohusu ufutaji wa leseni au idhini ya kutoa nyenzo za malipo;

(iv) Ibara ya 29 inayohusu kufutwa kwa leseni au idhini ya kutoa fedha za kielektroniki*;*

(v) Ibara ya 30 inayohusu utoaji wa mzunguko wa fedha za kielektroniki;

(vi) Ibara ya 34 inayohusu uendeshaji wa akaunti maalum;

(vii) Ibara ya 50 inayohusu kujumuisha makosa *(compounding offence)*; na

(viii) Ibara ya 57 inayohusu masharti ya mpito.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jedwali la Marekebisho lililowasilishwa na Mtoa Hoja ni matokeo ya Serikali kupokea maoni na ushauri uliotolewa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Muswada huu. Hata hivyo, Ibara ya 14 inayohusu kosa chini ya Sehemu ya Tatu inayofafanua mfumo wa malipo, Kamati ina maoni kuwa kiwango cha *fine* kilichotajwa katika Ibara ya 14(b) ni kidogo ikilinganishwa na thamani ya miamala inayoshughulikiwa na asasi hizo. Kamati inashauri kiwango hicho kiongezwe.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Kwa niaba ya Kamati, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Fedha, hususan Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Naibu Mawaziri - Mheshimiwa Adam Kigoma Malima na Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Katibu Mkuu - Dokta Likwelile na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania. *(Makofi)*

Aidha, napenda pia, kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Masatu pamoja na wasaidizi wake kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua hadi kukamilika kwa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa lengo kuboresha Muswada huu. Maoni na michango yao imeisaidia sana Kamati kukamilisha utungwaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kupitia Muswada huu. Kwa jinsi walivyoorodheshwa, naomba watambulike kwa umuhimu wao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyotuongoza katika Bunge lako. Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dokta Kashillah, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Angela Shekifu, Ndugu Rachel Nyega na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimuite Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Christina Mughwai!

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI – NAIBU MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha, Mheshimiwa James Mbatia, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya Mwaka 2015 (*The National Payment Systems Act, 2015)*. Maoni haya yanatolewa chini ya Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge lako za mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, utangulizi. Kwa heshima kubwa naomba kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu ya kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada huu muhimu wa kutungwa kwa Sheria ya Mifumo ya Malipo.

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru na kuwaomba Watanzania wote wanaotuunga mkono waendelee kutuunga mkono kwa kuhakikisha kuwa wanajiandikisha katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili wakati utakapowadia wawe na sifa ya kupiga kura na kuhakikisha kuwa wagombea wote wa UKAWA katika nafasi za Udiwani, Ubunge na Urais wanashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla. *TIS – Tanzania Inter Bank Settlement System* ni mfumo wa malipo makubwa na ya haraka unaoendeshwa na Benki Kuu ya Tanzania. Pia, mfumo huu unawezesha ulipaji wa malipo mbalimbali ya kibenki yaliyofanyika kupitia kwenye mfumo wa hundi, mfumo wa malipo ya ki-*electronic,* mifumo ya malipo yatokanayo na mifumo mingine kama vile mfumo wa malipo ya kodi ya kadi pamoja na malipo katika masoko ya fedha.

Mheshimiwa Spika, mbali na *TIS* kuna mifumo mingine ya malipo iliyopo kama ifuatavyo:-

(i) Mfumo wa malipo wa hundi *(automated cheques clearing system),* mfumo huu hutumiwa na mabenki katika kubadilishana hundi.

(ii) Mfumo wa malipo ya kielektroniki *(electronic funds transfer),* mfumo huu hutumika kupitisha malipo makubwa ambayo hugawanywa katika mafungu madogomadogo kama vile mishahara, malipo baada ya kustaafu na kadhalika.

(iii) Mfumo wa malipo ya kadi unaotumia mashine za kutolea hela yaani *ATMs* na ving'amuzi vya manunuzi.

(iv) Mfumo wa kufanya malipo, kuhamisha fedha au kufanya manunuzi kwa njia ya mtandao yaani *internet banking.*

(v) Mfumo wa kutuma au kutumiwa fedha kutoka au kwenda nchi mbalimbali duniani kwa kutumia huduma za *Western Union, Money Gram* na *Coinstar.*

(vi) Mfumo wa kutuma au kutumiwa fedha ndani ya nchi kwa kutumia Shirika la Posta kama vile *Postal, Money Order* na *Money Fax.*

(vii) Mfumo wa kutuma na kupokea fedha kwa njia ya simu za mkononi kama vile *M-pesa, Airtel Money, Tigo Pesa, Z-pesa* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ulioletwa katika Bunge lako Tukufu unapendekeza kutungwa kwa Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka 2015. Muswada huu unapendekeza kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo iliyopo hapa nchini kama tulivyoitaja hapo awali. Aidha, tunaelezwa kwamba Muswada huu utasaidia katika kukidhi haja na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yanayotokea nchini na duniani kote. Pamoja na hayo, Muswada unapendekeza jinsi ya kudhibiti changamoto zinazoweza kutokea katika sekta ya fedha na kutengeneza mazingira bora ya kiufanisi katika mifumo ya malipo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoorodhesha hapo awali, nchi yetu ina mifumo kadhaa ya malipo ambayo ni dhahiri kuwa inatambulika na Benki Kuu ya Tanzania na ni ukweli kwamba katika mifumo hiyo kuna baadhi ya asasi au kampuni zinazofanya kazi ya ulipaji fedha bila ya kuwa na leseni zinazotambulika kisheria na hivyo kuwepo na ugumu wa kuthibiti. Ukosefu huu wa Sheria ya Udhibiti wa Mifumo ya Malipo umekuwa na athari kubwa hasa kwa wateja mara tatizo linapotokea hasa katika mifumo ya malipo kielektroniki ukizingatia pia kuwa teknolojia inabadilika kila siku. Kukosekana kwa sheria mahsusi pia kunaweza kuleta migongano ya kibiashara kati ya makampuni yanayomiliki mifumo ya malipo kisheria kama vile mabenki na makampuni yanayomiliki mifumo ya malipo bila kuwapo kwa sheria maalum.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Muswada. Muswada una jumla ya Sehemu kumi na mbili na jumla ya vifungu 58 lakini Kambi Rasmi ya Upinzani itajielekeza tu kwa vile vifungu ambavyo inaona vinatakiwa kupatiwa ufafanuzi au kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7 kinahusu maombi ya leseni ya mfumo wa malipo. Aidha, kifungu kidogo cha (4) kinasema kwamba Benki kuu ya Tanzania itatoa uamuzi wa kukubali ama kukataa kutoa leseni baada ya muda wa siku thelathini tokea siku ambayo maombi yalifanywa rasmi. Sambamba na hilo, kifungu hiki kinasema kuwa Benki Kuu ya Tanzania inaweza kukubali au kukataa maombi hayo ya leseni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa siku thelathini ni nyingi kwa mtu kusubiri na pia mbali ya siku hizo zote kuna uwezekano wa kukataliwa kupatiwa leseni. Ni dhahiri kwamba muda ni jambo la kuzingatia katika biashara yoyote ile. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa iwapo masharti ya leseni yametekelezwa kusiwepo na sababu ya kuchukua siku nyingi kiasi hicho katika kutoa leseni.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 7(9) kinasema kuwa pale mwombaji asiporidhika na uamuzi wa Benki Kuu wa kunyimwa leseni kama kifungu cha 7(7) kinavyosema, ni kwamba ndani ya siku thelathini baada ya kupokea uamuzi wa Benki akate rufaa kwa Gavana.

*"Where an applicant is aggrieved by the decision made under this section, may apply to the Governor of the Bank within thirty days after receipt of such notice of rejection for review of the decision."*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka ufafanuzi wa mipaka ya kiutawala kati ya Benki Kuu na Gavana wa Benki Kuu kwani tunaamini kabisa kuwa uamuzi wa Benki Kuu ni uamuzi wa Gavana kwa kuwa yeye ndiye Mtendaji Mkuu wa Benki hiyo sasa itakuwaje mtu aliyenyimwa leseni pia aombe au akate rufaa kwa Gavana? Masharti ya kifungu hicho ni sawa pia na masharti ya kifungu cha 26(9).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 20 katika Sehemu ya Nne ya Muswada kinahusu utendaji wa makosa. Kifungu cha 20(a) na (b) vyote vinaonesha kuwa faini imeweka wigo wa juu yaani "*not exceeding*". Hii ni hatari kwani kuna uwezekano faini inaweza kutolewa ikawa ya chini ukilinganisha na kosa kiasi kwamba haitakuwa na athari yoyote kwa mtenda kosa. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka vifungu hivi viwekewe wigo wa chini yaani "*not less than*" na kiwango cha juu aachiwe Hakimu kuamua kulingana na kosa lenyewe. Aidha, masharti ya kifungu hiki yanafanana pia na masharti ya vifungu vya 31, 35(2), 41(3), 43(3), 44(2), 46(4) na 47(2).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 51 kinahusu kumlinda mlaji katika mfumo wa malipo na kifungu cha 51(2) kifungu kidogo cha (b) kinaongelea jinsi ya kushughulikia malalamiko na utatuzi wa migogoro. Kambi Rasmi ya Upinzani na wadau walipendekeza kwamba suala la utatuzi wa migogoro lisiachwe kwa mtoa huduma na mteja peke yao bali kuwe na mtu wa tatu kama vile Benki Kuu au taasisi nyingine kuona kwamba watu hawa wawili wanatendewa haki.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 56(3) cha Muswada kinasema kwamba:-

*"Gavana wa Benki, bila ya kuchapisha kwenye Gazeti, anaweza kutunga sheria ndogo, masharti na kutoa maagizo, miongozo, viwango, amri na sekula za kudhibiti mwenendo wa jinsi madhumuni ya sheria hii yanavyoweza kutekelezwa".*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa vipi watu watazifahamu sheria hizi na miongozo itakayotolewa na Gavana ili waweze kuitekeleza iwapo haitatangazwa Gazetini. Tunashauri kwamba sheria hizi ndogondogo na miongozo kama ilivyo kwa kanuni zote zitangazwe kwenye Gazeti ili wadau waweze wazifahamu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua umuhimu wa kuletwa kwa Muswada huu japo kwa maoni yetu umechelewa kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zinajitokeza kila siku katika mifumo ya malipo iliyopo na wateja kukosa pa kukimbilia. Tunaishauri Serikali izingatie na kuyafanyia kazi mapungufu tuliyoyaainisha hapo juu ili mifumo ya malipo iwe ya ufanisi kwa wateja na watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nina wachangiaji wengi lakini nitaanza na Mheshimiwa Zungu atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Msolla na Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru sana lakini vilevile niipongeze Serikali kwa Muswada huu ambao ni mzuri na unaendana na dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, sina tatizo na muswada nilitaka nitoe tahadhari ya namna dunia inavyokwenda na tahadhari ya *disaster* ambapo Muswada huu ukipita na kama Serikali haikuwa na *plan B* ya kudhibiti *disaster* hizi itakuwa tatizo. Nimeona kwenye Muswada huu Serikali imechukua tahadhari ya maeneo ya *disaster centre, of course* kunakuwa na *disaster recovery sites* lakini vilevile lazima Serikali ijue *Electronic Magnetic Pulse*. Kitu hiki ni hujuma kubwa sana inayofanywa na nchi kwa nchi na athari hii inaweza ikatupata sisi hata kama kutakuwa na matatizo kwenye maeneo mengine lakini hizi *Electronic Magnetic Pulse* ambayo kwa kifupi inaitwa *EMP* zikaathiri *system* nzima ya mtandao huu, ika-*melt system* nzima, ika-*melt* matumizi ya mtandao huu na ikaleta *destruction* kubwa sana kwa huduma na *facilities* hizi ambayo nia njema Serikali ambayo inayo ikashindwa kuwafanya watu waweze kuhudumiwa sababu the *whole system* ita-*collapse* sababu hizi *Electronic Magnetic Pulse* zina-*create radiation* ya *gamma* na hii *gamma* ina-*melt insulators*, ina-*melt* kila kitu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali lazima iwe na *plan B* kwenye *issue* kama hizi ili zisiweze ku-*disrupt* huduma. Naomba Mungu atujalie kisitokee kitu kama hicho lakini nchi nyingi zinachukua tahadhari. Hujuma hizi ni ndogo tu unaweza ukafanya hujuma hapa Dodoma tu uka-*create gamma radiation* sisi wote humu ndani hata magari yetu yasitembee, simu zikafa, mitandao ya benki *system* zote za nchi zika-*collapse*. Kwa hiyo, lazima kuwe na *backup plan B* ya kuwa ikitokea jambo kama hili *there is another system* ambayo ita-*take over* ili kusaidia jamii iweze kupata huduma zake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni suala la je, *server* hizi *ownership* ni nani? Ni Serikali yetu, ni Wizara yetu au *ownership* itabaki tena Afrika Kusini kama kawaida? Tunaona sasa hivi mitandao ya benki, unakwenda benki *system* iko *down* sababu mtandao ukiharibika huko Afrika Kusini au popote pale basi na huku vilevile huduma zinakuwa hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine hatutaki watu wa-*suffer,* tunataka *comfort* ya kuwa sheria hii ikipita na Serikali iwe na hiyo *plan B* kwa sababu kuna *issue* ya *firewall* katika *system* hii, Serikali imejiandaa vipi na *firewall* ya *hackers,* watu kuingia kwenye mitandao, watu kuibiwa sasa hivi ni tatizo kubwa sana kimataifa kwa wizi unaofanywa kwenye mitandao. Kwa hiyo, Serikali lazima iwe makini na *firewall system* itakayowafanya hawa *hackers* wasiweze kuiba. Kuna *computer crime syndicate* ambazo sasa hivi ndiyo biashara hapa Tanzania tunapigwa sana. Unakwenda kwenye hizi *ATM,* kuna watu wanatoka nchi za nje sitaki kuzifanya siyo vizuri lakini wanaiba sana, mabenki hayasemi tu yanaogopa *embarrassment* ya pesa zinazoibiwa. Kwa hiyo, mimi naongelea sana tahadhari, Muswada ni mzuri *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna *issue* nyingine Muswada huu u-*add value,* twende *an extra mile,* kuwe na *networking* kati ya Muswada huu na vyombo vya dola kama *TRA* tuweze kuona *transactions* zinavyokwenda hizi, *TRA* wawe na *feeder window* ya kuona hizi *transaction* ili iweze kupata mapato. Muswada huu usione kama ni urahisi tu wa masuala ya kielektroniki, nchi nyingi ndiyo unaisaidia Serikali ku-*capture* mapato yao kupitia mitandao kama hii.

Mheshimiwa Spika, nitakupa mfano mdogo kwenye hizi *credit card,* lazima kuwe na *monitoring system* ya chombo cha Serikali kama vile *TRA*. Wakiona leo Zungu anatoa pesa kwenye kadi yake Dodoma *TRA* wanajua, nikienda hotelini nikilipia bili kwa kadi yangu *TRA* wanajua lazima i-*add value* haina maana ya kuona tu *transaction* huyu anatoa huku anapeleka huku lazima Serikali iwe ina-*monitor transactions* zozote zinazofanywa na mtu yeyote ndani ya nchi au nje ya nchi atakayetumia *server* yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mfano mdogo na siku zote namwambia Waziri wa Fedha na Waziri wa Mawasiliano, Muswada huu vilevile uisaidie Serikali kupata mapato yake kwenye simu.

*Corporate tax* ambazo makampuni ya simu mengi wanababaisha hapa na pale iko *excise duty* na *VAT* 30% ya Serikali ambayo wewe na mimi na Watanzania unapoponunua kadi yako ya simu ya *top up* ya dola kumi au shilingi elfu kumi, elfu tatu ni *automatically* mali ya Serikali. Hizi nazo wakati mwingine kuna mgogoro haziendi Serikalini, kodi ambayo mimi nalipa na wananchi wanalipa sababu *mechanism* iliyokuwepo bado siyo *water tight* ya kujua miamala hii ya *transaction*, kwa hiyo, Muswada huu usaidie Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukienda nchi nyingine uki-*top up* tuseme unaweka dola kumi palepale ina-*display* dola tatu ni mali ya *TRA*, *immediately,* kwa hiyo wewe unabakia na dola saba na *operator*. Kwa hiyo, Muswada huu ufanye *networking* na vyombo vingine vya dola kusaidia Serikali iweze kupata mapato na iwe na *comfort* ya kujua pesa halali. Najua kwenye kodi kuna mambo mengi *management fees*, wakati mwingine mnakubali tu *declaration* za *statement of accounts* za makampuni haya lakini huu ndiyo mwarobaini sasa wa ninyi kuweza kujua *transaction* zilizofanywa na haya makampuni, *transaction* zinazofanywa na watu binafsi lazima kuwe na *feed window* katika chombo cha *TRA* na wao waweze ku-*monitor transaction* za pesa hizi tunazopitisha, *we are losing a lot of money* kwenye vitu kama hivi.

Mheshimiwa Spika, nenda Uingereza, watu wote hapa wamesafiri uki-*change pound* yako 13% *commission* ya Serikali na vitu kama hivi vikiwa hapa kwenye sheria kila mtu awe kwenye mtandao vitasaidia mapato. *It is not only about business* ya kutuma pesa kwa ma-*wire* na nakadhalika, *we have to go an extra mile* ili Serikali iweze ku-*capture* mapato kutokana na *system* kama hii *and we can do it.* Mimi naamini sana Mheshimiwa Waziri uwezo anao, Serikali ina uwezo jaribuni ku-*interact* na hawa watu wa *software* hii ku-*imply* hizi *input* ambazo nazieleza hapa ili sasa tupate mapato mengi sana.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu kubwa na kitu ambacho kinatuuma hata ile kodi ya kawaida ya *excise duty* na *VAT* tunayolipia makampuni haya haiwi-*captured* na Serikali vizuri sababu wale wana-*declare* tu basi hakuna *monitoring system* ya kujua *top up* kadi hizi au *air time* hizi hata zikiingizwa nchini hakuna *mechanism* zikiwa *cleared* pale bandarini wana-*clear* kama *consignment* hawa-*clear* kama *air time*. Wanatakiwa wai-*clear* kama *air time, Zungu Telephone Company* imeingiza *air time* ya *ten billion,* 30% palepale anaambiwa muingizaji hii ni mali ya umma. Nenda kauze kadi zako au palepale anatakiwa ailipie ile *excise duty* na *VAT immediately* lakini *this things are not done* sababu ile *mechanism* bado hawajaweza kui-*capture*. Kwa hiyo, naomba Serikali itazame maeneo ambayo yanaweza kuendelea kupata mapato kwa kutumia Muswada huu ili ku-*capture revenue* ya Serikali kwa kutumia Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi sana nilitaka nitoe tahadhari tu ya vitu ambavyo Serikali inaweza baada ya Muswada huu kupita wakatumia Muswada huu kuongeza hizi *added value in put* ambazo zitaisaidia Serikali kupata mapato yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo naunga mkono na napongeza sana Wizara na Serikali kwa kuleta Muswada kama huu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Nilisema nitamuita Mheshimiwa Profesa Msolla atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Muswada huu wa Sheria ya Mifumo ya Malipo wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, vilevile nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati huu. Hata hivyo, sisi pamoja na kwamba tunaleta Muswada huu wakati huu kwa kweli tumechelewa ukilinganisha na nchi jirani kama ilivyosemwa na Waziri mwenye dhamana kwamba wenzetu kama Kenya, Zimbabwe, Botswana, Rwanda walianza kutumia sheria hii muda mrefu kidogo. Hata hivyo, nafikiri katika kuleta Muswada huu lazima tutakuwa tumejifunza na uzoefu wa wenzetu katika nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Muswada huu ambao ni Muswada mzuri ni pamoja na kuweza kuanzisha chombo kimoja cha kusimamia malipo lakini zaidi kudhibiti changamoto za malipo. Katika changamoto za malipo zipo ambazo zinatuathiri sisi Wabunge na wananchi kwa ujumla. Changamoto hizo ni utaratibu unaotumika kutoa malipo kufikia katika maeneo yanayolengwa. Hapa nazungumzia juu ya Halmashauri zetu mbalimbali kuna utaratibu ambao unatumika kwa sasa hivi ambapo Hazina hutoa fedha ziende kwenye Halmashauri lakini haziendi kule moja kwa moja zinapitia Benki Kuu kama *a clearing house* lakini *process* hiyo huchukua muda mrefu kwa sababu kutoka *BOT* fedha hizo zinaweza kuchukua hata miezi miwili, mitatu kabla hazijafika kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi ukifuatilia unakuta kwamba hizi fedha zinaonekana kwenye mtandao lakini hazishuki kule kwenda kufanya kazi inayotegemewa. Jambo hili kwa sababu ni pamoja na kuangalia changamoto za malipo, hili kwangu mimi naona ni changamoto kubwa sana. Isitoshe baada ta fedha kufika kwenye Halmashauri lazima tena upate kibali kwa Mwanasheria Mkuu, nchi nzima wapate vibali vya kuanza kutekeleza hiyo miradi kutoka kwa Mwanasheria Mkuu. Kwa hiyo, utaratibu huu wa malipo kwa kweli umekuwa ukicheleweshа sana miradi mingi hata pale ambapo fedha zimepatikana. Tunajiuliza, je, utaratibu ambao tunaujadili leo utasaidia kuondoa hili tatizo kwa sababu limekuwa ni kero na limechukua muda mrefu sana kuweza kukamilisha miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kama alivyozungumza mzungumzaji wa kwanza, kumekuwa na matatizo makubwa sana ya wizi kwenye mitandao na najua kuna sheria inayokuja ya *cyber crime,* mimi ningekuwa nimefurahi sana kama sheria hizi mbili zingekuwa zimejadiliwa kwa ukaribu karibu ili kusudi tuweze kuunganisha matatizo yaliyoko katika sehemu zote mbili kwa sababu kuna mwingiliano mkubwa. Imezunguzwa juu ya wizi wa fedha kupitia hata kwenye *ATM* na simu za mkononi. Nashauri Serikali iangalie ili iweze kuziba mianya hiyo ambako fedha nyingi zinaibiwa katika *transactions* mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini hata huko nyuma, hapa imezungumzwa juu ya Sheria ya *Electronic and Postal*, 2010. Katika sheria hii kulikuwa na pendekezo, ili kuweza kukusanya ushuru wa kutosha kutoka makampuni ya simu makampuni yote haya yaingie kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange* ili kuweza kufuatilia mapato yao na waweze kulipa kodi za uhakika lakini badala yake tumeacha makampuni haya yawe yana-*declare* yenyewe kwamba sisi tulichopata wakati huu ni hiki, kwa hiyo, kodi ambayo inatakiwa kutozwa ni hii. Nafikiri huu ni upungufu mkubwa. Ningeomba katika sheria hii iboreshwe zaidi ili kusudi makusanyo ya mapato ya makampuni kuhusu *transactions* zote zinazofanywa kama alivyozungumza msemaji wa kwanza ziweze kupatikana na Serikali iweze kukusanya mapato yake kiurahisi.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi sana juu ya wizi kwenye mitandao na imetolewa mifano mingi. Sasa hivi watu wanaanza kuwa na uwoga hata kuchukua fedha kwenye *ATM*, kuna watu wamegundua njia mbalimbali za kuweza kutoa fedha na hata mabenki yenyewe yamekuwa yakiibiwa. Kwa hiyo, sheria hii tungeomba iwe na utaratibu wa kuweza ku-*monitor* vizuri na iwekwe namna ambayo inaweza kuzuia wizi ambao umeanza kuenea sana kwa njia ya mtandao.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa huo mfupi na hasa hili la utekelezaji wa miradi namna fedha zinavyotoka Hazina kupitia Benki Kuu na kuchukua muda mrefu kabla hazijawafikia wananchi na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi mbalimbali. *Otherwise* mimi naunga mkono hii sheria inayopendekezwa ili kusudi iweze kutusaidia zaidi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Christowaja atafuatiwa na Mheshimiwa Chomboh.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache katika Muswada huu wa Sheria ambao umeletwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nianze kwa kuunga mkono huu Muswada, na niunge mkono maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja ya maoni ya Kamati pamoja na haya ya Serikali kwa kutuletea huu Muswada ambao una manufaa makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi na Mheshimiwa Zungu kwa kweli amezungumza mambo ya msingi sana, mimi nitakachoongea ni kusisitiza tu na kutoa mifano jinsi ambavyo nchi yetu imekuwa haipati mapato kutokana na hii mitandao ambayo inatumika katika nchi yetu. Kwa mfano, Mheshimiwa Zungu ametolea mfano wa jinsi ambavyo nchi yetu au Serikali inashindwa ku-*monitor* yale mapato yanayopatikana katika mitandao mbalimbali ya simu.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi kwamba mitandao mbalimbali ya simu au yote imekuwa ikianzisha *promotion* mbalimbali kwa mfano sasa hivi *Airtel* ina *promotion* ambayo inasema 'Yatosha Ushinde Gari' na tukipita pale *Airtel* tunaona magari yako pale. Hata hivyo, ukijiuliza hivi haya magari ambayo yamenunuliwa pale na kutoa zawadi, Serikali yenyewe imepata kiasi gani unashindwa kuelewa. Haya magari ya mamilioni ya fedha utakuta Serikali haiambulii hata kiasi ambacho ni robo ya hiyo faida ambayo mitandao inapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana Muswada huu sasa utaifanya Serikali iweze kubana mitandao ya simu ambayo inapata faida kubwa na hapohapo Serikali haipati. Sasa Serikali tunaomba muweke wazi vipengele ambavyo vitabana mitandao ya simu ili kile kiasi ambacho kitapatikana *TRA* iweze kunufaika na sisi wananchi tuweze kujipatia maendeleo kwa sababu ndiyo watumiaji wakubwa wa mitandao na ndiyo wawekaji wakubwa wa hizi pesa ambazo mitandao inatumia kutoa zawadi mbalimbali za magari na zinginezo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye wizi wa mitandao hasa *ATM* wamezungumza wenzangu, mimi mwenyewe ni muathirika wa kuibiwa kwenye *ATM* katika benki ya *NBC*. Ukiuliza ni Wabunge wangapi wameibiwa Bunge lililopita watanyoosha mikono karibu nusu. Cha kujiuliza hivi kama kweli kuna *monitoring system,* nifahamu itakuwa ipo, inakuwajekuwaje hawa wezi wanaenda wana-*hijack ATM* kadi za watum anachukua *PIN number* yako, anatengeza kadi ileile na namba ileile wakati wafanyakazi wa benki wapo wana mitambo wanaangalia hapa kuna nini. Tumeibiwa sana, unapata *emergency* ni Jumamosi jioni unauguliwa unakimbia ukachukue pesa *ATM, card* inakuwa *captured* hela hakuna kwenda kuuliza ni mpaka Jumatatu, mimi ilinitokea. Jumatatu nakwenda naambiwa Mheshimiwa hebu leta akaunti namba yako. Wanacheki akaunti namba wanakuta hela zote zimeibiwa nina *balance* ya Sh.39,000 hapo nina *emergency*. Huu Muswada tunaomba uweke wazi jinsi ambavyo mteja atashtaki benki Mahakamani fedha zake zile zilizoibiwa wakati uleule na riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapo-*process* kurudishiwa zile pesa inaweza kuchukua wiki moja mpaka mbili ndiyo zinarudishwa, hapo wewe mteja huna cha kusema, huna pa kulalamika kwa

sababu sheria haikuruhusu. Sasa kama ni mgonjwa ameshakufa, umeshazika ndiyo fedha zinarudishwa tena wakati mwingine zisitimie kwa sababu huwezi kujua watarudishaje. Tunaomba turuhusiwe wateja kushtaki benki na wafanyakazi wake kwa sababu si busara kuonyesha kwamba hawa wafanyakazi wa mabenki hawahusiki, wanahusika kwa sababu wanajua mitandao inavyofanya kazi. Muswada huu utatusaidia sana na naipongeza sana Serikali kwa hili kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wizi wa mitandao ya simu, unanunua kifurushi, tunaomba sheria itamke wazi, unaambiwa kifurushi chako ni cha mwezi mzima. Huo mwezi unaisha pengine hujatumia unaambiwa imekwisha, sasa kinaishaje, wakati mmeniambia mimi kiasi hiki. Hii sheria iweke wazi, kama nimenunua shilingi 20,000 basi nizitumie mpaka zimalizike na nipate *service* inavyotakikana. Wakati mwingine nikinunua kifurushi wajanja sana hawa mitandao hupati hiyo simu unayotaka, ukipiga unaambiwa simu haipatikani au simu imezimwa, hela zinakwenda na siku zinapita, ukienda vijijini simu hakuna, hujatumia pesa yako mtandao unakata unarudi mjini bado siku moja kifurushi kimekwisha, hizo pesa zinakwenda wapi? Huu Muswada wa Sheria utusaidie wateja pesa yetu itumike kikamilifu, huo ni wizi mdogo mdogo.

Mheshimiwa Spika, wizi mwingine kwenye mitandao ya simu unanunua huduma, kwa mfano, siku hizi tunanunua Luku tunalipia maji, unatuma hela imekwenda huduma huipati, huna pa kushtaki na huwezi kurudishiwa pesa zako wakati mwingine mpaka uje kukumbuka, uje kufanya *process* umeme umezimika, huna mahali pa kununua na hajapata hiyo *service*. Huu Muswada utatusaidia kuweza kushtaki haya makampuni yanayotuibia vilevile tuweze kupata haki zetu kwa wakati unaokubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kupata haki vizuri, kifungu cha 51(2)(b) kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imependekeza kinasema kwamba utatuzi wa migogoro umhusishe mteja na mtoa huduma. Mimi naunga mkono mawazo ya Kambi ya Upinzani kwamba awepo na mtu wa tatu ili haki itendeke. Kama ambavyo tuna-*solve* matatizo ya kijamii, wewe mtu kakukosea lazima kuwepo na mtu mwingine wa tatu kusikiliza ile kesi ili haki yako iweze kutendeka. Wamependekeza wenzetu wawe Benki Kuu au taasisi nyingine ya kifedha na mimi naunga mkono ili utatuzi wa migogoro ufanyike kwa haki na usawa.

Mheshimiwa Spika, pia Kambi Rasmi ya Upinzani imependekeza kwamba kile kifungu ambacho kinatoa faini muwe na kiwango cha kuanzia na kiwango cha kuishia, kifungu cha 20(a)na (b) mmesema tu *not exceeding,* kuna *ten million* hapa na milioni hizo nyingine mlizotaja. Tunaomba muweke kiwango cha kuanzia na cha kuishia ili ionekane. Kosa hili kiwango chake kinaanzia kiasi fulani na kuishia kiasi fulani kuwa na mipaka. Kwa sababu ukisema kisichopungua tu hata kama ni kosa kubwa kiasi gani analipa ileile uliyomwekea, kiwe cha kuanzia na cha kuishia.

Mheshimiwa Spika, sina mengi, nawashukuru sana na huu Muswada kwa kweli tunaupongeza na tunauunga mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Muhammad Chomboh.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie katika mada iliyokuwa mbele yetu ya Muswada huu wa Malipo kwa njia ya *electronic*.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuleta Muswada huu, Muswada ambao ni muhimu sana kwa wakati tuliokuwa nao lakini kwa wakati ambao tunakwenda nao kwa sasa.

Kiujumla naweza kusema kweli tumechelewa kwa sababu tulianza ku-*practice* kabla hatujaweka sheria. Pia ni vizuri kwamba sheria imekuja na imeshabainisha mambo mengi ambayo tumeyaona kwa vitendo kwa sababu kama waliotangulia kuzungumza walivyosema kuna mambo ambayo yamejitokeza, yamejitokeza kwa sababu tu wakati mwingine ni kwa makusudi tu au kwa makosa fulani lakini kwa kuwa kuna sheria sasa hata wale watekelezaji au ma-*operators* au vile vyombo ambavyo vinahusiana na malipo ya fedha watakuwa wako makini sasa hivi katika utendaji wao au kutoa huduma kwa wananchi kwa sababu na wao kwa upande mwingine inawezekana ikaja sheria hii ikawapa mtihani mkubwa kama siyo kulipa hasara ambayo mteja anaipata.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kusema ni kwamba sheria hii au Serikali kitu kikubwa katika mambo mengi ambayo yanakwenda ndivyo sivyo ni kwa sababu sheria tunazipanga vizuri lakini usimamizi wa sheria zetu, utekelezaji wa sheria zetu wakati mwingine ndiyo vikwazo na unarudisha nyuma yale maendeleo tuliyoyakusudia. Sasa basi hii sheria ni vizuri wale wasimamizi au wale ambao walikuwa wanahusika na mambo haya inabidi wajengewe uwezo kwa sababu haya mambo yanahitaji ujuzi, ujuzi wa kielektronikia. Kwa mfano, watu wa *TRA*, Wizara ya Fedha au watu wa Benki Kuu ni muhimu zaidi kuwa na watu ambao wana uwezo wa kuweza kuisimamia sheria hii kwa vitendo wakati linapotokea tatizo. Kwa sababu hawa watu ambao wanaendesha haya makampuni ambayo yanahusiana na mambo haya ya malipo kwa njia ya *electronic,* ni wajuzi ambao wanajua ni namna gani ya kucheza, sasa wale watu ambao watakwenda kuwahoji na wenyewe pia wawe na ujuzi zaidi ya wao kusimamia suala hili. Vinginevyo utakuwa wewe umetunga sheria lakini kuisimamia sheria huwezi kwa sababu huna uwezo wa kuweza kusimamia kivitendo kile ambacho kinatokea kwa upande mwingine. Kwa hiyo, Serikali inaleta Muswada huu, Muswada ambao ni mzuri na ni muhimu sana kwa kweli kwa sababu miamala inatendeka kila siku lakini sasa watu wanapata hasara na watu wengine wanapoteza fedha yao chungu mzima kama walivyotangulia kusema ni muhimu zaidi sasa Serikali iwajengee uwezo wasimamizi wa Serikali hii na Serikali isimamie kikweli kweli kwa sababu suala hili linahusu mahitaji ya wananchi na maisha ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa naitaka Serikali ni kuwa-*encourage* wafanyabiashara kwamba badala ya kutumia *debt* kadi watu wengi sana wawe na uzoefu wa kutumia *credit card.* Kwa sababu hiyo itakuwa inawapa usalama kwanza kwa pesa zao lakini pia na taasisi zile ambazo zinakwepa kodi wakati unakwenda kulipa *credit card* na ku-*swap* inakwenda moja kwa moja mpaka mfuko wa *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili linatendeka nchi zote duniani, ni sisi tu ndiyo tunatembea sana *cash.* Basi tujaribu kuwa-*encourage* wafanyabiashara hasa wa maduka makubwa kwa mfano *supper market, malls* na kadhalika wawe na wenyewe pia wana mpangilio fulani na kuzungumza na mabenki fulani, kwa sasa hivi wananchi wengi sana mishahara yao inapita benki kwa hiyo, wana uhakika kabisa kwanza fedha fulani za mfanyakazi fulani zinafikia mahali fulani, kuwe na mikataba baina ya maduka na maduka ili watu wawe wanatumia zaidi *credit card* kuliko kuwa wanatumia pesa *cash*. Hii itaongeza zaidi mapato kwa Serikali lakini pia kwa usalama wa fedha kuibiana humo mitaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu ulikuwa huo, naunga mkono hoja hii na nawaambia Serikali ijitahidi kuwajengea uwezo wasimamizi na Serikali isimamie kwa dhati sheria hii ndiyo, tutapata mafanikio tuliyokusudia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilimuita Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatia Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia kwenye Muswada huu muhimu sana kwa ajili ya maisha ya Watanzania na maendeleo ya Watanzania na uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Muswada huu umechelewa lakini pamoja na kuchelewa niipongeze sana Serikali kwa kuweza kutuletea kwa sababu kwa kweli wananchi wamekuwa wakiteseka, wananchi wamekuwa wakiibiwa sana, naamini kabisa kwamba sheria hii kwa kiasi kikubwa inaenda kumlinda mteja na mteja ni Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa mengi na nashukuru sana kwa semina ya jana imetusaidia lakini kubwa zaidi natambua kwamba wiki hii tutakuwa vilevile na Muswada wa Sheria ya *Cybercrime* ambayo kimsingi inaendana sana Muswada wa leo. Kwa hiyo, nilikuwa nategemea kwamba kama zingefanywa kwa pamoja watu wangepata wigo mpana wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba dunia sasa hivi kutokana na kukua kwa TEHAMA imekuwa kama kijiji na kwa maana hiyo jambo lolote linalotokea mahali popote tunakuwa na *effect* hapa Tanzania. Kwa hiyo, niseme kwamba Muswada huu ni mzuri pamoja na kwamba una upungufu lakini nadhani hayo yatakuja kwenye *amendments*.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tukiangalia huu Muswada umeleta mambo mazuri kama nilivyosema na kubwa ni hili la kuzibana taasisi za fedha, tunajua kumekuwa na miamala mingi. Nianze kwa kusema utakumbuka hivi karibuni watumiaji wa umeme wanaotumia Luku walipata matatizo makubwa kwa sababu ya watu wanaoitwa *hackers,* kumekuwa na *hacking* hapa Tanzania na hili ni tatizo la kimataifa lakini naamini kabisa hii sheria vilevile itasaidia. Wote tunajua sasa hivi masomo ya *IT* yamekuwepo hapa Tanzania lakini vilevile kwa sababu ya ukosefu wa ajira inawezekana kabisa vijana hawa wanatumia hiyo teknolojia vibaya. Kwa hiyo, nadhani hii sheria itaweza kuwabana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu pamoja na kwamba yameongelewa mengi, ni lazima basi sheria hii pia iangalie. Kwa mfano, unaweza ukaenda benki ukakuta hakuna mtandao, unaambiwa *server* iko *down.* Kwa hiyo, naishauri Serikali pamoja *servers* hizi kuwa *down* wahakikishe wanakuwa na *backup system* ambayo itaweza kusaidia Watanzania au wateja wasipate matatizo, kwa sababu haiwezekani unaenda kwenye *shopping mall*, umeshanunua vitu unafika pale hela hakuna. Kwa hiyo, naomba Serikali vilevile iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuwa Muswada huu nia na madhumuni ni kumsaidia mteja tunatambua kwamba sasa hivi Watanzania zaidi ya asilimia 65 wanatumia M*-Pesa, Tigo Pesa* kwa ajili ya kutumia ndugu zao fedha lakini makampuni haya yamekuwa yakichaji hela nyingi sana. Sijaona ni kwa jinsi gani Muswada huu vilevile unasimamia makampuni haya, unaweza ukawa unatuma shilingi 50,000 tu lakini unakatwa shilingi 2000 mpaka 3000. Katika benki unakuta utaratibu wao ni tofauti kidogo, unaweza ukatuma hata shilingi milioni moja lakini ukachajiwa shilingi labda 500 mpaka 1000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali ione ni jinsi gani inaweza kusimamia vilevile miamala ya haya makampuni hasa ukizingatia kwamba wananchi wetu ni maskini na wanategemea sana mtiririko huu kwa sababu ni vigumu sana kwenda kufungua akaunti kwenda benki kwa hiyo tunatumia zaidi *M-pesa, Tigo Pesa*, *Airtel Money* lakini bado gharama zao kwa kweli ni kubwa sana ukilinganisha na benki. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iweze kuliangalia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizingumzie suala *hackers,* naomba sana Serikali ijaribu kuliangalia. Kwa kweli kama walivyosema wenzangu watu wameibiwa, kama Wabunge wameibiwa, Mawaziri wameibiwa maana yake wananchi tunaowawakilisha wameibiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pia ni mwathirika, haiwezekani una simu yako mkononi lakini namba yako ikawa inatumika na mtu mwingine na hilo limetokea. Halafu wanavyochukua hizo namba wanaandika *message* za kuomba fedha watu. Mimi kuna watu wengi wameambiwa naomba hela milioni, watu wameibiwa sana na nimeenda *Airtel* na nashukuru jana nimeongea na mtu *TCRA* na ameniambia kwamba wana kitengo na nitakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inaonekana wazi wafanyakazi wa makampuni siyo waaminifu kwa sababu haiwezekani mtu a-*swap* namba ya mtu ambaye ni mtu wa nje lazima ni mfanyakazi wa haya makampuni. Kwa hiyo, naiomba Serikali vilevile ihakikishe sheria hii inazibana taasisi za kifedha ili na wao washtakiwe. Kwa sababu haiwezekani mtu uwe na simu yako mkononi lakini simu ileile inatumiwa na mtu mwingine. Hivyo, naomba vilevile hilo waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuzungumza ni suala la adhabu. Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri naomba niwaambie kwamba adhabu mnayotoa kwa kweli ni ndogo mno tena mnaweka ukomo. Ukiangalia hicho kifungu cha 20 anasema tu kwamba, "*a natural person to a fine not exceeding ten million*". Hivi kama mtu ameiba zaidi ya shilingi bilioni moja halafu unamwambia atalipa *not exceeding ten million*! Mimi nadhani ingekuwa "*not less*" ili sasa Mahakama ndiyo iangalie ukubwa wa tatizo. Unapomfunga mtu wa mabilioni halafu unasema *ten million* Mheshimiwa Waziri naombeni hapa kwa kweli pawe na *amendment* ili hawa watu wajue tatizo ni kubwa na kwamba wakifanya kosa kama hilo wajue madhara yake ni nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na nilivyosema ni kweli hii sheria inasaidia mteja, lakini vilevile naomba watuambie. Kwa mfano, unaweza ukaenda nje na kadi yako ya *ATM* au *Visa Card* lakini unapofika nje ya nchi unatumia wakati labda unataka kuondoka, mara kadi yako imenasa kwenye mashine. Je, utaipataje wakati siku hiyohiyo ndiyo unasafiri au kesho yake? Nilikuwa naomba kujua, kama kweli hii sheria nia yake ni kumlinda mteja, ni kwa kiasi gani basi tunapoenda nje au Watanzania wanapoenda nje wanalindwa na hii sheria ili hata *ATM* zao zinaponasa kule wajue ni jinsi gani wanaweza kuzipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu pamoja na kwamba wengi wanasema tumechelewa na hii sheria ni kweli teknolojia inaenda haraka sana lakini naamini kabisa huu ni mwanzo na kama kutakuwa na chochote kinacholeta mabadiliko basi yataboreshwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kumekuwa na utaratibu wa Serikali tunapitisha sheria hapa lakini tatizo linakuja kwenye kanuni. Nakuomba Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba kanuni zinatungwa haraka ili tuweze kuwahakikishia wananchi maisha yao. Kwa kweli fedha zao zinapotea sana, tunarudisha maendeleo nyuma, wananchi wanajitahidi sana, ni kweli teknolojia imekuja ni nzuri lakini basi tunaomba tupitishe sheria lakini vilevile hizo kanuni zitoke mapema ili tuweze kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan ahsante. Nilisema nitamuita Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa atafuatiwa na Mheshimiwa Sulemani Jafo halafu atakuja Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Muswada kimantinki ni mzuri sana na tuseme tu ni kweli umechelewaa kidogo ikiwa kuna nchi ambazo Muswada kama huu wamepitisha miaka 17 iliyopita na nchi ndogo za jirani nyingine kama miaka mitano, sita iliyopita kwa hivyo tumechelewa. Sasa kuchelewa huku kulipaswa kutumike kujifunza na matatizo yaliyotokea katika nchi za wenzetu. Inawezekana Mheshimiwa Waziri amechukua baadhi ya mambo lakini mengi sana inaonekana hatujajifunza katika nchi za jirani ambazo wameshapitisha Muswada kama huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu wenye vipengele 57 na vile vitatu vilivyomo katika sheria ya *Bill of Exchange, Cap*.125 ambavyo zinafanyiwa *amendment* unaweza ukasema una vipengele 60. Katika vipengele hivyo 60 au vifungu 60 vya Muswada huu, ni vifungu vinne tu vilivyomgusa mteja moja kwa moja ambaye anatumia miamala hii ambavyo ni kifungu cha 47 kinachozungumzia *protection of customer transfer* kwa maana ya uhifadhi wa taarifa za mteja. Kifungu cha 48 kinachozungumzia *time to effect transfer* yaani muda wa kuingiza zile fedha kwenye *account,* kifungu cha 52 kinachozungumzia *availability of fund and services* yaani upatikanaji wa huduma yenyewe ya fedha na kifungu cha 53 kinachozungumzia makosa ya kimtandao. Ni vifungu vinne tu kwa ujumla vifungu vyote vilivyobakia ni udhibiti, usimamizi baina ya Benki Kuu na hayo makampuni yanayotoa huduma za fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, wazungumzaji wengi walivyozungumza humu ndani ulikuwa unasikia yale malalamiko na maudhi na matatizo wanayopata wananchi katika matumizi ya miamala hii ya kieletroniki. Sasa ukitizama upande mmoja labda wananchi hawajatendewa haki vizuri kwamba, pamezungumzwa maeneo machache. Kuna baadhi ya mifano Mheshimiwa aliyemaliza sasa hivi ametoa, yeye katoa mfano wa kwamba kadi yako labda imechukuliwa kwenye *ATM* ukiwa safarini nje, lakini siyo nje tu hata Mikoani, umetumbukiza kadi yako imechukuliwa na wakati huo unaondoka, utaipataje na namna gani?

Mheshimiwa Spika, lakini watu wengi mpaka hivi sasa wakisafiri wanabadilisha fedha kupata dola, wanachukua maburungutu ya fedha mfukoni kiasi ambacho tukienda katika hiyo dunia nyingine anajulikana tu yule Mtanzania, kila kitu analipa kwa fedha ya mfukoni, wenyewe sasa hivi kila kitu malipo yote wanatumia hizi kadi. Hata hivyo, malipo haya ya kadi *fees* zake na ile *exchange rate* yake inakuwa taabu kui-*determine* kiasi kwamba ukifika hapa kuna kama *double fees* ya kule ulikochukulia ile fedha na hapa nchini sasa zile gharama zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, si rahisi kwa mtu ambaye si mpelelezi sana kuweza kujua nilipokuwa nje nimetumia kitu gani kutokana na *bank statement* inavyoonyesha akachambua vizuri. Kwa hivyo, inafaa sheria hii iweke wazi na ihamisishe watu kutumia hizi kadi wakisafiri kuepuka kuibiwa fedha na kusafiri na pesa *cash*. Ilikuwa vizuri Muswada ufahamishe hivyo na kutoa vielelezo au maelekezo kwa mabenki yetu ili mtu ajue kwa umakini *exchange rate* gani iliyotumiwa katika miamala aliyofanya wakati yuko safarini. Muswada huu hauja *cover* vizuri masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kuna michezo hii ya bahati nasibu ambayo kwa wengine ni kamari. Kuna watu wengine kwa dini zetu kamari ni dhambi, hapaswi mtu kucheza kamari, wengine wanacheza kamari yaani ni hiari ya mtu. Sasa hivi wewe ukinunua vocha tayari umeshatumbukizwa katika huo mtandao wa kamali na ikitokezea siku umeambiwa Mnyaa ameshinda shilingi milioni mia moja utazikataaje, itakuwa ngumu sana na huku umeingizwa katika lazima. Huu Muswada ueleze kwamba haya makampuni yasilazimishe watu kucheza

kamari, iwe ni kitu cha hiari, huyu anahitaji huyu hahitaji. Isiwe wewe pesa yako inatumika katika masuala ya kamari wakati tu unaponunua vocha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia huu mchezo wa hizi kamari katika mitandao hii ya simu kwa hapa Tanzania kuna kitengo kile cha mambo ya kamari kinachoongozwa na Ndugu yetu Abasi Tarimba, kodi zake zinajulikana, je, hii mitandao kodi zake zinajulikana? Wanafanya vipi, Serikali inapata mapato kiasi gani kwa kamari hizi? Muswada huu hauja-*address* masuala kama haya. Wananchi wanapata shida na Muswada haujazungumzia masuala haya.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu haujahusisha masuala ya risiti au kielelezo mara utumapo pesa. Mara nyingi unapotuma fedha katika maeneo mengi unahitaji kuwa na kielelezo kwamba fedha niliyomtumia Mheshimiwa Spika imefika na kielelezo changu ni hiki. Ushahidi uwepo wa risiti yoyote au stakabadhi ya kwamba umetuma fedha. Sasa mitandao ya simu hii wanaandika tu pahali lakini wewe uliyetuma laki tano, laki sita, milioni huna *evidence*, huna kidhibiti chochote cha kwamba nimetuma fedha hii yaani ukawa nacho *incase* kikihitajika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia Muswada haujahusisha *TCRA* moja kwa moja wakati hili suala la fedha ni baina ya makampuni yanayojihusisha na miamala hii, *BOT* na *TCRA,* hawawezi kukwepa *TCRA* katika masuala kama haya. Kwa sababu mengine una ushahidi wa *message* tu, ikipotea yaani huna uthibitisho tena. Iwepo njia unataka *evidence* yako *TCRA* waweze kukupa kirahisi na siyo ufuate mlolongo mkubwa. Kwa hivyo, Muswada pia ulikuwa uhusishe vizuri baina ya *TCRA*, haya makampuni ya simu au wanatoa miamala ya fedha pamoja na Benki Kuu, ni masuala ambayo yanahitaji kufuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hii mitandao inagharama tofauti na hizi gharama zimekuwa kubwa na wote kila mmoja anajivutia utumie mtandao wake tu. *Fees* zile kama umetuma laki tano, milioni moja zinatofautiana baina ya mtandao huu na mtandao huu. Muswadaa unafaa uzungumzie kuwe na *synchronization,* kuwe na uwiano wa hizi gharama na siyo kila mmoja ajipige anavyotaka tu na mwingine kwa vile anavutia awe upande wake atafanya rahisi ukitumia mtandao wake lakini ukitumia mtandao wake kwenda mtandao mwingine unapigwa kigogongo kikubwa sana kiasi kana kwamba unaambiwa usifanye hivyo hasa utumie wa kwake yeye tu. Sasa Muswada ulikuwa u-*address* masuala kama hayo angalau kuwe na uwiano wa zile gharama, vinginevyo kila mtu atajifanyia vile anavyotaka mwenyewe, sasa hili kidogo linaonekana ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla yapo mambo ambayo amezungumzia Mheshimiwa Zungu ambayo kwa ujumla ni muhimu sana lakini inawezekana pengine hapa siyo pahali sahihi, labda katika huo Muswada wa *ICT* utakaoletwa labda ndiyo pahali madhubuti ambao utazungumzia mambo hayo kwa ujumla. Kwa ufupi Muswada ni mzuri, tumechelewa kidogo lakini tujifunze na makosa ya wenzetu sisi tuliochelewa isipokuwa mambo ambayo yanawagusa wananchi ni machache kuliko yanayogusa Benki Kuu na haya makampuni.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Sulemani Jafo halafu baadaye Mheshimiwa Mnyika na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, napenda kushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia katika Muswada huu na nadhani mjadala wetu unapokwenda ni kwamba kila mtu anaafiki kwamba Muswada huu ni muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mantinki ya Muswada huu, mimi nasema haujachelewa umekuja katika kipindi muafaka ambacho sasa teknolojia imekuja kwa kasi sana, kipindi ambacho sasa tunatakiwa tuyashughulikie matatizo ya kifedha kwa ajili ya kulikomboa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, navyofikiri Muswada huu una maana kubwa sana kwa sababu kuna uwezekano mkubwa kwamba Watanzania usiku wakalala asubuhi wakaamuka halafu watu katika suala zima la miamala ya simu makampuni huko ukasikia mambo yameparaganyika *data base* zote zimeharibika. Hilo likitokea maana yake ni janga kubwa sana katika Taifa letu hili. Kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba Muswada huu sasa japo sijaupitia kwa ndani zaidi, ninaamini kwamba utakwenda kusaidia Taifa letu hili liwe katika wakati mzuri maana kama jambo hili la kifedha lisiposimamiwa vizuri kwa mfano, muda mrefu umepita bila kuwa na sheria maalum katika jambo hili maana yake tulikuwa tunaenda katika janga la hatari sana kwa sababu kuna siku lingetokea jambo la hatari kubwa kwelikweli. Makampuni ya simu yanayokuja na kufanya *transaction* za kifedha ambapo hakuna sheria maalum ya kuweza kuyabana, bahati mbaya wananchi ambao wanapesa zao katika mifumo hiyo ya simu, asubuhi wanaamka wanaambiwa *data base* hizo zimeharibika bila ya kuwa na sheria ya kuwalinda, naamini inawezekana ingekuwa ni hatari kubwa sana. Kwani hiyo, kwa mimi kwa kupitia haraka haraka ndiyo maana nimesema sijausoma kwa kina Muswada huu lakini najua mantiki yake ni Muswada ambao unakuja kulikomboa Taifa letu hili na hasa kulinda haki za nchi yetu, haki za wananchi wetu lakini vilevile haki za uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naiomba sana Wizara, wenzangu wengine wamesema ni kwamba wakati mwingine tunapitisha Miswada hapa utekelezaji wake unachukua muda zaidi. Mimi niombe sana Wizara yetu kwamba tunapoleta Muswada huu wengine wanasikiliza huko nje wanaona kwamba wamebanwa katika maeneo fulani. Kwa hiyo, ina maana kwamba tukichelewa kutengeneza kanuni, watu hao wataweza kutumia fursa hiyo kufanya hujuma kubwa sana katika nchi hii. Mheshimiwa Waziri niombe sana kwamba mara baada ya Muswada huu ukishasainiwa na Mheshimiwa Rais, tuhakikishe kwamba tunaandaa kanuni haraka sana na kanuni hizo zipite katika Kamati zetu za Bunge zinazohusika ili mradi wale ambao wanataka kutumia mwanya wa kuhujumu uchumi wa nchi hii tuweze kuhakikisha kwamba tunazuia janga hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niiombe Wizara, sasa umefika muda, mimi ninaamini kupitia michakato hiyo, inawezekana kuna wanjanja wengine wanasababisha hatupati makusanyo vizuri. Sasa naomba Muswada huu usaidie, kuna upungufu kwenye baadhi ya maeneo ambayo saa nyingine mapato yetu kama Serikali hatuwezi kuyakusanya vizuri basi tuweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mnyaa hapa kwamba jambo hili nadhani ni jambo mtambuka, niombe sana kuangalia *TCRA* japokuwa Muswada huu tunasema ni wa suala zima la mambo ya kifedha benki huko lakini jinsi gani *TCRA* tutafanya kazi kwa ushirikiano wa karibu zaidi, ili mradi tuhakikishe kwamba siyo kwamba mtu anasema jambo hili halinihusu hapana, jambo hili kila mtu linamhusu kwa sababu ni suala zima la Taifa letu hili. Lazima tuangalie kuna kipengele gani ambacho moja kwa moja kitahusiana kwa sababu miamala hii yote inapita katika mitandao ya simu ambayo mwenye mamlaka na mitandao ya simu nadhani ni *TCRA* ambaye kazi yake ana ratibu katika eneo hilo. Niombe tuangalie ni jinsi gani tutafanya kama Muswada huu utagusa moja kwa moja au kuna jambo lingine ambalo tutaweza kuliingiza tuweze ku-*link* vizuri ili mradi Muswada huu uweze kuleta tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni jambo moja lakini elimu ni jambo lingine. Kwa sababu Muswada huu unazungumzia haki za wananchi, inawezekana wakati leo Wabunge

wengi wanasema kwamba pesa zao nyingi sana zimeibiwa katika mabenki, kwa mfano siku moja nilimuona Mheshimiwa Kisangi hapa akilalamika kwamba siku moja alikuwa anaona kila wakati analetewa *message* na *NMB* kwamba ametoa kiasi fulani wakati mwenyewe kumbe hahusiki na hilo. Tuangalie tutafanya jinsi gani tutoe elimu ya kutosha kwa wananchi kwamba pale wanapodhulumiwa haki zao watafanya vipi kuzipata haki zao, hilo ndiyo litakuwa jambo la msingi.

Mheshimiwa Spika, kikubwa zaidi nipende kuishukuru Serikali yetu kwamba jambo hili sasa limekuja katika muda muafaka lengo kubwa ni kuwalinda wananchi lakini lengo lingine nina imani ni kulinda uchumi wa nchi yetu ambao kwa muda wa dakika chache ungeweza kuparaganyika endapo tusingekuwa na sheria madhubuti ya kusimamia mambo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa John Mnyika atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi niungane na wote waliosema kwamba Muswada huu umechelewa kuletwa kwa sababu majirani zetu ndani ya Jumuiya ya Uchumi wa Kusini mwa Afrika, Afrika ya Kusini wametunga Sheria hii ya *National Payment System* mwaka 1998, ninayo nakala yake hapa. Tunaweza kusema pengine Afrika Kusini kiteknolojia imekuwa kwa haraka kuliko nchi nyingi za Afrika lakini jirani zetu kabisa Zambia ambao ngazi na hadhi ya kiteknolojia tuko katika ligi moja, walitunga sheria mwaka 2007. Kwa vyovyote vile Tanzania kwa kutunga sheria mwaka 2015 tumechelewa lakini wanasema kawia ufike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa tunasema kawia ufike, nina mashaka iwapo kutungwa kwa sheria hii kutaweza kutatua matatizo ya udhibiti ambayo yamezungumzwa. Kwa sababu mwaka 2006 Bunge hili lilitunga sheria mbili muhimu sana.

Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya 2006 na Sheria ya Benki Kuu ya 2006, ambazo kama zingesimamiwa kwa uthabiti, bila udhaifu wowote, ni wazi baadhi ya matatizo katika miamala yangeweza kudhibitiwa kabla hata hatujafikia hatua ya kutunga sheria hii. Kwa hiyo, nina mashaka, kama hatutajadili juu ya namna gani tunasimamia utawala wa sheria, kutunga sheria peke yake kunaweza kusiwe suluhu ya matatizo yanayowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu katika ukurasa wa nne wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameeleza kwamba mifumo hii ya malipo ipo katika viwango vya aina mbili. Kuna mifumo ya viwango vya juu kwa maana ya *high end* na kuna ambayo ni zaidi ya shilingi milioni 10 au dola 10,000. Aina ya pili ya mifumo ni ile ya malipo ya viwango vya chini *(low value)* ambayo haizidi shilingi milioni 10 au dola za Kimarekani 10,000.

Mheshimiwa Waziri akaendelea mbele na naomba nimnukuu: "Mfumo wa malipo ya viwango vya juu unaotumika Tanzania, ni *Tanzania Interbank Settlement System (TISS)* ambao ulianza kutumika mwaka 2004. Mfumo huu ni mfumo wa kielektroniki unaounganisha benki za kibiashara na Benki Kuu ya Tanzania kwa njia ya mtandao ili kuwezesha uhaulishaji wa fedha kwa uharaka."

Kwa hiyo, kwa sheria hizi mfumo wa kielektroniki kwa viwango vikubwa vya fedha ulikwishakuwepo na udhibiti uko mikononi mwa Gavana. Sasa tujiulize kwa kuwa na mfumo wa namna hii, hivi ilikuwaje ikaruhusiwa kutolewa kwa fedha kutoka benki ya *STANBIC*, dola milioni

122, sawasawa na bilioni zaidi ya 200 kwenda kwenye akaunti zisizoeleweka zenye mashaka juu ya vielelezo vyake *Australia* na Afrika Kusini, kwenye kashfa ya *Tegeta Escrow. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi mfumo wetu huu ulikuwa wapi, udhibiti wa Gavana ulikuwa wapi, wakati haya yanatokea? Tunatunga sheria hapa, kumpa Gavana mamlaka ya juu kweli kweli, kwa hadhi yake kwa mamlaka yake ya udhibiti, ya usimamizi. Tujiulize, mamlaka ambayo yamekuwepo kwenye sheria, yametumika namna gani kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Spika, tunayo mifumo, lakini tujiulize, hivi ilikuwaje, ukiondoa fedha hizi zilizopita kupitia mfumo huu wa kuhamishwa kupelekwa nje. Hivi ilikuwaje, fedha taslimu, bilioni 73, zikatoka katika akaunti ya *STANBIC* nje ya mifumo hii ambayo sheria tayari iliweka kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira haya, pamoja na kutunga sheria, bado Wizara ina wajibu wa kutueleza jambo hili uchunguzi wake umefikia wapi ili tuamini hata haya mamlaka tunayoyatoa na mifumo tunayoweka chini ya Sheria mpya za Malipo, matatizo yakitokea ya watu kuibiwa kwenye *ATM*, watu kuibiwa kwenye *M-pesa*, watu kuibiwa kwenye mambo mbalimbali, hatua zitachukuliwa! Tutaamini vipi, kama kwenye mambo ambayo yako wazi kabisa, hakuna uwajibikaji, kwa maana kutoa maelezo, ilikuwepo yakatokea haya, hakuna uwajibikaji kwa maana ya kuelezwa, hivi waliogawiwa bilioni 73 ni akina nani, kwa nini wao hawatajwi na hawachukuliwi hatua? Hakuna uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU ilimhoji mtumishi wa Benki ya *STANBIC*, Paulo Owala na hatimaye akasimamishwa kazi, aliwekwa rumande Mganda huyu baadaye akasimamishwa kazi. Kama TAKUKURU ilimhoji, maana yake TAKUKURU sasa ieleze, kama ilifikia hatua mpaka kumweka rumande, matokeo ya uchunguzi wa TAKUKURU ni yapi ili tuamini, kama kukiwa na watumishi wengine wa benki, wakaingia katika mkondo wa ku-*syndicate* na baadhi ya watu, kuiba si tu fedha za umma, bali hata fedha za wananchi kwenye *ATM*, watachukluliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatua hazichukuliwi kwenye mambo kama haya, tuna mashaka kwamba sheria zetu, bado hazina mfumo thabiti zaidi wa kuwezesha uwajibikaji. Ni wazi katika hatua ya kufika Bunge kukaa kama Kamati, tutapendekeza kwenye majedwali ya marekebisho maeneo ambayo yanastahili marekebisho ili kuongeza nguvu zaidi katika kuwezesha utekelezaji wa sheria ili mifumo hii ya malipo kweli iweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili au ugonjwa huu ni wa muda mrefu sana. Haukuanzia kwenye kashfa ya *Tegeta Escrow* ya mwaka 2013, wala haukuanzia kwenye kashfa ya *IPTL* ya miaka ya 1990/1993. Mambo haya yameanza muda mrefu, yameanza kwa sura za namna nyingi sana.

Kwenye orodha ya mafisadi iliyosomwa Septemba, 15 pale Mwembeyanga, kuna nukuu kutoka kwenye ripoti…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnyika, nilifikiri unatoa kama mfano, lakini utunge sheria hii, tufanyeje!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo nasema, tunatunga sheria, nazungumzia mamlaka na majukumu ya Gavana wa Benki Kuu katika kusimamia Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha, Sheria ya Benki Kuu, lakini zaidi mamlaka hayo sasa yanakuja kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo na nazungumzia hapa malipo makubwa, miamala inayofanyika kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, tuna rekodi ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ikisema kwamba, aliyekuwa Gavana kipindi cha nyuma, katika kashfa ya Meremeta, aliruhusu fedha zikapita kwa mfumo huu huu, kwenda kwenye benki isiyojulikana *Nedbank* ya Afrika Kusini, dola milioni laki moja na kumi na nane, zaidi ya bilioni 20!

Mheshimiwa Spika, sasa niache kutoa mifano hii kwa sababu mifano ni mingi, kuna mifano ya *TANGOLD*, kuna mifano *Deep Green,* kuna mifano ya Kagoda…

**SPIKA:** Tufanyeje sasa!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, niseme hivi, Sheria hii ya Mifumo ya Malipo, ambayo tukishapiga hatua ya Bunge kukaa kama Kamati, nitaleta mapendekezo ya vifungu ambavyo kama vikirekebishwa, Sheria hii ya Mifumo ya Malipo, itakuwa bora zaidi kwa maana ya kuongeza udhibiti, siyo tu katika masuala yanayohusu miamala mikubwa, bali masuala yanayohusu miamala inayotumia nyenzo nyingine za malipo kama kwenye *ATM*, kama ving'amuzi vya ununuzi yaani *POs*, kama kwenye maeneo yanayohusiana na ulipaji wa kwenye mitandao wa kibenki na malipo kama *Maxcom*, malipo kama *Selcom*, malipo kama *Maxmalipo* na mifumo yote hii.

Mheshimiwa Spika, tutapendekeza kupitia majedwali ya marekebisho kwa sababu kwa dakika hizi 10 ni vigumu kuweza kwa Muswada wenye vifungu vingi namna hii kusema kifungu hiki kiwe hivi, kifungu hiki kiwe hivi na ikaeleweka kwa Serikali kuweza kuzingatia kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie eneo lingine ambalo naungana na Kambi ya Upinzani katika kuhakikisha kwamba marekebisho ya msingi yanafanyika. Nayo ni masuala yanayohusiana na viwango vya adhabu. Natambua kwamba Serikali imekwishakusudia kuleta marekebisho ya kuongeza viwango vya adhabu zaidi kama ambavyo Serikali imekubaliana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika kuyatafakari haya mambo yote mawili, ni vizuri Serikali ikazingatia vile vile pendekezo la Kambi ya Upinzani, kwamba pamoja na kuweka adhabu ya juu, kuna haja vile vile ya kuweka adhabu ya chini, kwamba kwa vyovyote vile, kiwango cha adhabu kisipungue hivi, kiwango cha adhabu kisizidi hivi. Haya ni marekebisho ya msingi ambayo yanahitajika kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kukubaliana vilevile na Wabunge wenzangu waliosema kwamba Sheria hii ya Mifumo ya Malipo, tungeijadili vyema zaidi kama tungehusisha na Sheria nyingine inayohusiana na Malipo ya Kielektroniki, Miamala ya Kielektroniki ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo, Sheria hii iliyoletwa kwa hati ya dharura,…

**SPIKA:** Muda wako umekwisha.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, *amendments* hizo ni vizuri zikafika mapema, kusudi tuweze kuona mahali pake pa kuingia. Umenisikia Mheshimiwa Mnyika, nasema *amendments*, , mtu yeyote mwenye *amendments* alete mapema kusudi watu wote wazione kwa wakati, siyo tuanze kupambana humu ndani, itakuwa si vizuri.

Nilisema Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sikuwepo kidogo, naomba nitumie nafasi hii pia kuungana na wananchi wa Jimbo la Mbinga Magharibi, lakini Mkoa wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla, kuomboleza kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa John Damiano Komba.

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono Muswada huu na naona umefika wakati muafaka. Hata hivyo, niombe kwamba, Muswada huu ili uweze kueleweka kwa wananchi wengi zaidi, naomba uandikwe kwa lugha ya Kiswahili, kama ambavyo wengi sasa hivi tumekuwa tukilisemea hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba niende katika kifungu cha 15 na 16, ambacho kinazungumzia namna ya kupata vifaa vitakavyoweza kufanya kazi hii ya kutoa malipo ya kielektroniki. Nimejaribu kuoanisha na mfumo wa ulipaji wa kodi ambao sasa hivi unaendelea nchini na malalamiko ambayo wananchi hasa wajasiriamali wadogo wadogo wamekuwa wakiyazungumzia.

Mheshimiwa Spika, suala langu hapa ni kwamba, nahitaji ufafanuzi au angalizo, ni kwamba, kumejitokeza hii hali ya kwamba, tunasema mashine ziagizwe au ziletwe na kundi la aina fulani au watu fulani. Matokeo yake, bei za kuagizia mashine hizo zinakuwa ni kubwa, kiasi cha kushindwa kufikika kiurahisi kwa watumiaji wengi.

Mheshimiwa Spika, hilo limelalamikiwa sana, juzi tarehe 19 Machi, 2015, nilikuwa na mkutano na wajasiriamali wadogo pale Sumbawanga, wamelalamika sana juu ya hilo, ikianzia kwamba mashine ziliuzwa kuanzia milioni moja la laki nane na zikashuka mpaka kufikia laki sita. Kwa hiyo, naomba nitoe angalizo, hasa kwa kuangalia hawa wajasirimali wadogo, ambao wanajihusisha na shughuli hizi za malipo ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, naomba pia niseme kwamba, kwa muda mrefu, makampuni haya makubwa ambayo yanahusika na malipo haya ya kielektroniki, yamekuwa hayajashikwa moja kwa moja katika ulipaji wa kodi na hawa wananchi wadogo wadogo wamekuwa wakisema kwamba wao wanalipa kodi nyingi zaidi kuliko hawa wakubwa. Kwa hiyo, kutokana na mfumo huu, naamini kuwa itakuwa sasa tumekidhi haja ya kuona kwamba makampuni yanalipa kodi zinazostahili ikizingatiwa kwamba mzunguko wa fedha kwa kutumia miamala hii ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sijui kwa nini leo napenda kukuita Mwenyekiti, lakini ni Mwenyekiti wa kikao, naomba niulize kifungu hiki cha 24 ambacho kinazungumzia kwamba mtu hataruhusiwa kufanya kazi hii ya malipo ya kielektroniki endapo hana leseni.

Mheshimiwa Spika, wote mashahidi, mfumo huu hasa wa kutumia miamala ya simu katika kufanya ulipaji wa fedha umesaidia sana kukua kwa biashara na kukua kwa huduma za kibenki hasa kwa wananchi wanaoishi vijijini. Kule wanaohudumiana ni wenyewe kwa wenyewe. Mabenki haya makubwa hayapo katika maeneo haya ya vijiji.

Mheshimiwa Spika, watu walikuwa wanapata shida, yaani anatumia nauli kubwa kwenda kuitafuta benki iliyoko katika Wilaya, anatumia nauli kubwa kwenda kuhakikisha ni namna gani analipa ada ya mtoto wake, lakini kwa kutumia utaratibu huu, umewezesha wananchi wengi wawe ni wa kijijini kuweza kupata huduma hizi za kibenki.

Sasa hofu yangu ni kwamba, ni kweli tunasema kwamba wote wawe na leseni, lakini, yule mwananchi ambaye yeye ameamua kufungua ka sehemu kake kadogo ambako

anahudumia watu wake wawili watatu, naye ataingia kwenye mfumo huu. Kwa hiyo, naona kwamba kama masharti yatakuwa makali sana, yatafanya hawa wananchi wa vijijini, ambao hawana hizi huduma za kibenki, ambazo ziko rasmi katika maeneo hayo, warudi tena kwenye ile ile hali ya unyonge wao ambayo kwa muda mrefu walikuwa wakiipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyo, naomba hili sharti lililowekwa hapa na faini zilizowekwa lazima ziwajali hawa watu ambao ni wa *informal* ambao hawajawa rasmi, lakini ni muhimu sana katika mfumo wa maisha yetu ya kila siku, kwa sababu mtu hatokei moja kwa moja akawa ni mjasirimali au mfanyabiashara mkubwa, anaanzia na eneo hili dogo na hasa katika maeneo hayo ninayoyasema ni ya kijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana, isije ikafikia mahali sasa mwananchi huyu wa kawaida, akadaiwa kulipa faini hii kubwa ambayo tunasema sasa, tuseme isiwe *not less than*, ikawa milioni tano, kumbe alikuwa anafanya biashara ya shilingi elfu tano au elfu 60 kwa mwezi mzima.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kwamba, ili ufanisi wa mashine hizi uweze kuwa mzuri, pia lazima tuangalie suala la *maintenance*, katika maeneo yale ambayo yako mbali na huko ambako hizo mashine zinatoka, inapotokea zimeharibika na kwa sababu lazima zihakikiwe na ziweze kufanya kazi yake ipasavyo, hao mafundi wa kutengeneza hizo mashine, kama ilivyo kwa mashine zile za kodi, wako wapi? Kwa sababu hali iliyoko sasa hivi katika baadhi ya maeneo, tunahamashisha sana wananchi wote watumie mashine hizo katika kukokotoa hesabu zao na katika kufanya malipo yoyote, lakini sasa mashine ikiharibika, inakuta kunakuwa na tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni rai yangu kuona kwamba, kunakuwa na vituo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu ili kuhakiksiha kwamba, hawa watumiaji wa hizo mashine, hasa hawa wadogowadogo ninaowazungumzia, wanaweza kupata huduma za matengenezo mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, lile zoezi la kufikisha umeme vijijini, tafadhali liendelee kupewa kasi ili wananchi wengi wanaoishi vijijini waweze kupata huduma kama hizo na wao waweze kufaidika na hizi ajira zitakazotokana na kupitishwa kwa sheria ambayo leo hii tutaipitisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Martha Mlata halafu baadaye Magdalena Sakaya!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nitoe mchango wangu kidogo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, napongeza, pamoja na kwamba Muswada huu umechelewa, lakini wengi wamesema, kawia ufike, naamini tutaziba angalau mapengo ambayo yametokea kule nyuma kabla ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba ruhusa yako ninukuu *message* moja ili mchango wangu uweze kukamilika. *Message* hii imetumwa kwa Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa *DC* wangu, karibu sana Iramba, Iramba tunasema Iramba Nkulu kuliko Tanzania, kwa hiyo, karibu sana. *Massage* hii imetoka *Airtel* inasema "mpendwa mteja, huduma ya kusikiliza miziki ya bure kutoka *airtel flavour* itakwisha baada ya siku tatu, utakatwa shilingi 35 kwa siku, kujitoa tuma sms kwenda namba 0901000000"

Mheshimiwa Spika, *message* hii ukitaka kujitoa kama alivyosema, ukiandika ili ujitoe usikatwe fedha hiyo, *message* haiendi, hapo ndipo ninapotaka kuanzia.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wizi mkubwa sana kutoka kwenye haya makampuni. Wametuibia sana, sasa nataka niunganishe kwamba, je, sheria hii inakwenda pia kudhibiti wizi wa namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, ninazo *messages* nyingi sana kutoka kwenye simu yangu nikikatwa sh. 400, ama kila baada ya siku mbili, ama wiki moja, ama wiki mbili, kwamba, umewekewa upya wimbo fulani na umekatwa sh. 400 kwa siku 30, lakini baada ya siku mbili tatu unawekewa tena upya, lakini bila ridhaa yangu mimi na wengi wamefanyiwa hivyo.

Mheshimiwa Spika, wizi huu unaofanywa ningependa kujua, sheria hii kama, maana nimeona makampuni mengi yaliitwa; ya simu yaliitwa, *TCRA* waliitwa. Je, inakwenda kudhibiti hali hii? Pia hiyo sh. 400 inapokatwa, piga hesabu watu milioni moja, ni shilingi karibu milioni 400. Mwenye wimbo ule, anapata haki yake?

Mheshimiwa Spika, pia ninachotaka kujua je inakwenda kuweka *record* na kudhibiti kwanza kama nchi, kama *TRA* inahusika katika fedha hizi? Je, *TRA* inapata chochote kwa ajili ya Taifa? Ningependa kujua, je, Msanii mwenye wimbo wake ni nani anasimamia ili na yeye apate haki yake kutoka kwenye mauzo hayo ambayo nayaona ni haramu, nani anakwenda kuyahalalisha? Sheria hii inakwenda kuhalalisha?

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kama ni kweli Muswada huu umekuja, wa Sheria hii utakwenda kudhibiti hali kama hii, nitaunga mkono, lakini vinginevyo sioni hata sababu ya kuunga kwa sababu ya wizi huu unaofanywa wa kiwazi wazi, Watanzania karibu milioni arobaini ni wangapi wametumiwa meseji moja ya kukatwa shilingi hiyo mia nne au hii wanayosema, hii shilingi thelathini na tano ambayo unalazimiswa tu kukatwa, jitoe, hujitoi, kwa nini wasibadilishe mfumo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hilo na naomba ku-*declare interest* kwa sababu hata mimi ni mmoja wa wale ambao wana miziki yao na mimi ni mwimbaji wa nyimbo za Injili ambapo nyimbo zetu zinatumika, zinauzwa. Naomba nitoe mfano mmoja, kuna watu wanawekewa miziki hajaomba; kwa mfano, nina babu yangu ambaye ni Shekhe pale nyumbani. Ukimpigia simu unakuta wimbo uliowekwa, 'hakuna Mungu kama wewe *Yahwe* aaa...' Shekhe huyo, lakini bado.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilimpigia Mchungaji Kadiva nikakuta, 'alikasema alikasema, sijui wa nini wa nini! Siyo kweli kwamba ameomba ule wimbo, watu wanawekewa. Mimi mwenyewe ukinipigia sasa hivi utasikia oooh, nabembelezwa! Mimi sijaweka huo wimbo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini wanatufanyia hivyo? Wabadilishe mfumo. Sasa kama sheria hii inakwenda kudhibiti, kama unataka mimi niweke wimbo niambie ninunue kama vile ninavyonunua vocha kuweka kwenye simu, niweke *password* yangu nichague wimbo. Lakini bado ningeshauri, sina mengi ya kusema nataka nishauri kwamba *COSOTA, TCRA* wapewe jukumu, pamoja na *TRA* ya kusimamia miamala hii ya kuuzwa kwa nyimbo za wasanii. Kama *percent* itakwenda *TRA*, *percent* iende kwa muuzaji, *percent* iende kwa mwenye wimbo wake, lakini *percent* iende *TCRA*, kila mtu aweze kupata kile anachostahili. Naomba nishauri hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, wengi wamesema, wafanyabiashara wengi wanapokwenda, hata sisi unaposafiri, tukienda nje ile posho yako unapewa tu unaiweka mfukoni, sawa ni ndogo, lakini wafanyabiashara wengi wanaondoka na fedha zao nyingi, Dola labda laki moja au zaidi, hasa wanaokwenda labda Hong Kong, Guangzhou, sijui wapi, wanakwenda kununua bidhaa na wanarudi, zile fedha haziendi kibenki, wanazibeba mkononi. Kwanza ni hatari, lakini naona huo ndiyo mwanya wa watu kutorosha fedha hapa nchini, huo ndiyo ukweli. Naomba nijue, sheria hii inakwenda kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, labda niishie hapa, ili tudhibiti huo utoroshwaji wa hayo mabilioni na mabilioni, nchi unakuta haina hela tu eti kwa sababu watu wametorosha fedha zao, watu wamehamisha fedha, wanahamishaje? Serikali inafaidika, wanahamisha kupitia njia ipi, je, mfumo huu unakwenda sasa kudhibiti?

Mheshimiwa Spika, naomba sana hasa kwenye masuala ya kazi za sanaa nipate majibu labda nitaunga mkono; lakini kama hii haipo sioni sababu ya kuunga mkono Muswada huu wakati mabilioni yanapotea kwanza kwenye Taifa, lakini bado na kwa msanii mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante. Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumza kwamba kawia ufike, lakini naona kabisa kwamba ni makosa makubwa kwa nchi kama Tanzania kuweza kukubali mifumo ya fedha ndani ya miaka 15 kufanya miamala mbalimbali bila kuwa na sheria. Hatuwezi kusema kwamba tukawie tufike kwa sababu hasara iliyopatikana kwa Watanzania katika maeneo mbalimbali kwa kuweza kukubali mifumo, tumeipokea kwenye *technology* mpya bila kuweka kwanza sheria za udhibiti, tulifanya makosa makubwa sana na naiomba Serikali ijifunze hili kutokana na makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi tunayazungumza kutokana na matatizo ambayo tumepata kutokana na miamala ambayo imefanywa na nina imani kabisa kama tungetanguliza sheria tangu huko nyuma, pengine haya mengi yanayochangiwa hapa Bungeni leo yasingekuwepo, ingekuwa ni kuboresha Muswada, lakini tunaanza kuelezea machungu ambayo tumepata kutokana na kwamba Serikali haikuliona hili mwanzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika naomba nianze na alilomalizia Mheshimiwa Mlata. Kwa kweli tumekuwa tunachangia hapa Bungeni kwenye bajeti karibu bajeti za miaka mitano iliyopita. Tunawekewa nyimbo ambazo hatuzitaki, tunawekewa vitu kwenye simu ambavyo hatuvitaki, lakini kwa nini halifanyiwi kazi? Leo Mheshimiwa Mlata pale anasema lililotumwa leo kwenye simu, lakini miaka mitano hapa tunazungumza, hata kama kulikuwa hakuna sheria, hata kuongea na makampuni tu kwamba wateja wenu hawataki haya mmeshindwa? Kwa nini tuzungumze mambo yale yale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hii inauma sana, kama anavyosema, mimi ni Mkristo nawekewa wimbo wa Kiislam, Muislam anawekewa wimbo wa Kikristo. Wanaingilia mpaka masuala ya dini zetu, hatutaki kwa nini Serikali haifuatilii haya? Pia ni wizi, nina imani kabisa Serikali haipati pesa kwa sababu sijaamua kwamba niwekewe huo wimbo. Naomba hili lifanyiwe kazi.

Mheshimwia Spika, suala lingine, ni suala la uwiano wa gharama kwenye fedha zinazotumwa kwa njia ya makampuni mbalimbali, makampuni yote kuanzia *Money Gram*, kuanzia *Western Union, Money Fax* mpaka Makampuni ya Simu. Sheria hii sijaona itaweka udhibiti gani kuwepo na uwiano, si kila kampuni iamue tu kwamba inajiwekea utaratibu wake wa kuchaji tozo fulani au makato fulani; lazima sheria iweke uwiano kwamba makampuni yawekewe viwango au uwekwe na uwiano fulani, kwamba makato yawe yanaendana na si kila kampuni kuweka jinsi ambavyo inaona.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye kila tozo zinazotolewa, kwenye *transaction* ya fedha, aidha ni Kampuni ya Simu, ni *Money Gram*, kuwepo na tozo ya Serikali inufaike kutokana na *transaction* ambazo zinafanyika kwenye miamala hiyo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kuwepo na kumbukumbu na hasa suala la kutuma fedha kwenye simu. Tunatuma fedha haina kumbukumbu ya aina yoyote, naomba sheria iweke utaratibu wa kuwepo na *documentation*. Unapotuma fedha uweze kupata chochote kwa yule ambaye unampa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunatuma fedha aidha kwenye *M-Pesa* au kwenye *Tigo-Pesa*. Ukiangalia kwenye simu yako aidha inakuja namba ya unayemtumia au jina la unayemtumia, pale ni basi. Nataka nitoe mfano mmoja, Niliwahi kutuma pesa kwenye *M-Pesa*, tena ilikuwa Shilingi laki tatu; baada ya kumtumia ananiambia tayari Mheshimiwa hela yako itaingia baadaye.

Mheshimiwa Spika, namwambia jina gani limetokea kwenye simu, ooh! Sikumbuki jina gani, kumbe pale nilitaka kuibiwa, nisingemuuliza angeniibia kwa sababu ni utaratibu ambao umekuwepo. Kungekuwa na ki-*documentation* au kumbukumbu angenipa kwamba umetuma laki tatu *documentation* yako hiyo hapo. Kwa hiyo, naomba sheria iangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, suala la kulinda fedha za wateja kwenye miamala ya simu. Siku hizi wafanyabiashara wakubwa na hata wadogo wanatumia sana *M-Pesa* kwa njia ya kuuza na kununua. Kumekuwepo na utaratibu, aidha mnunuzi ananunua bidhaa kwenye maduka makubwa makubwa, anamwambia nakutumia kwa kutumia *M-Pesa*. Kweli anatuma na ana-*confirm* kwenye simu kwamba hela imeingia, baada ya muda anakwenda kuitoa. Ni wizi ambao umefanyika sana.

Mheshimiwa Spika, tayari kama nimepokea nakubali kwamba, jina lako limetokea umeingiziwa *one million* au laki tano, baada ya nusu saa, kwa sababu una uhakika imeshaingia huna wasiwasi una-*keep on* na biashara zako na *business* zako. Baada ya muda ukija kuangalia kumbe yule anapiga kule anasema nilikosea kutuma ile fedha, kwa hiyo, hela inarudi kwa aliyetuma. Kwa hiyo, wewe umeshakula hasara, matatizo ni mengi, naomba na hii sheria ihakikishe kwamba na hili inabana. Kama fedha ikishatumwa kwa mteja uwezekano wa kurudi kwa yule lazima kuwepo na angalau taratibu za kufuata ili kuondoa wizi kama huu.

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo, jinsi gani fedha zinalindwa kwenye benki zetu, fedha za wateja. Naomba hili liwe wazi tulijue. Mwaka wa jana mwezi wa Kumi kulikuwepo na heka heka kwa wateja kwenye benki ya *NBC*. Tulisikia kwa ndani ndani kwamba benki inafilisika, walikuwa ni heka heka watu wanakimbizana kwenda kutafuta jinsi ya kuhamisha fedha kule.

Mheshimiwa Spika, lazima sheria ituambie, sijui kama ipo, jinsi gani fedha iliyoko benki mbalimbali zinalindwa, aidha, zinaibiwa, tunapataje fedha zetu, aidha kuna majanga yametokea, tunalipwaje, au aidha benki imefilisika, fedha inalipwaje, vinginevyo watu

watakuwa wanaweka fedha zao benki, lakini wanakaa kwa mashaka kwa kuwa hawana uhakika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia, ni suala la makato yanayofanyika. Kuna makato yanayofanywa ndani ya benki kwa kuhamisha fedha kutoka kwenye benki hiyo hiyo kwenye akaunti moja kwenda kwenye akaunti nyingine. *May be* labda nina akaunti mbili kwenye akaunti moja, nina akaunti ya malengo ya mtoto wa shule na akaunti yangu *(current account)*. Nataka nitoe fedha kwenye *current account* naingiza kwenye akaunti ya mtoto ya shule, kuna fedha inakatwa pale.

Mheshimiwa Spika, naona huu ni wizi mtupu, haiwezekani kama *NMB,* natoa fedha kwenye akaunti yangu napeleka kwenye akaunti ya mtoto benki hiyo hiyo wananikata fedha kwenye benki moja akaunti moja. Huu ni wizi. Kwa kweli huwa inakera sana; naomba pia sheria iweke utaratibu, benki moja hiyo hiyo, akaunti tofauti kwa nini kuwepo na makato ambayo hayana maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ucheleweshaji wa fedha. Fedha hazifiki kwa wakati, fedha zinaokoa maisha ya watu, fedha mtu yuko dukani anataka umtumie fedha kwa *M-Pesa*, umetuma fedha haifiki kwa wakati. Naomba sheria iweke pale fedha inapochelewa yule ambaye amekosa huduma, au mtu ni hospitali amekosa huduma, nini kifanyike na adhabu ipewe kwa wale ambao wamechelewesha kufikisha ile fedha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kati ya kitu ambacho naona tumeshindwa Tanzania na Wizara ya Fedha imeshindwa na Benki Kuu imeshindwa, Gavana ameshindwa ni jinsi ya kusimamia miamala ya fedha kwenye suala la kutumia Dola. Bado nchi yetu shilingi imeendelea kuporomoka kwa kuwa tumeshindwa kusimamia shilingi yetu kabisa. Ni aibu! Nchi nyingine huwezi kununua hata peremende kwa kutumia Dola, nchi yetu tumeshindwa kutumia Dola.

Mheshimiwa Spika, leo na napenda kabisa angalau uje Muswada wa jinsi gani ya kudhibiti matumizi ya Dola ndani ya nchi yetu. Leo tunavyo vioski mbalimbali, vimekuwa vioski, kila mahali unabadilisha pesa. Tunakobadilishia pesa kule Serikali haipati hata *VAT*. Juzi nilikuwa Pretoria, nimezunguka masaa mawili natafuta benki ya kubadilisha Dola upate hela yao hakuna, hata benki za kubadilisha zimetengwa, vioski hakuna.

Mheshimiwa Spika, umekwenda kubadilisha Dola, *VAT*, *you have to pay VAT* kabla ya kubadilisha pesa yako. Nimetembea siwezi kupanda *taxi* kwa sababu sina fedha yao ninayo Dola. Angalia jinsi ambavyo hata wenzetu wa jirani wanadhibiti fedha yao, South Africa hapa, Tanzania tumeshindwa. Leo tunafanya manunuzi wka Dola, tunalipa kwa Dola, kodi za nyumba zinalipwa kwa Dola, vioski vimejaa kila mahali kama vioski vya kuuza juisi na maji, hii ni aibu kwa nchi kama hii.

Kwa kweli kwa hili Serikali mmeshindwa, Gavana Mkuu kwa hili umeshindwa. Naomba Serikali ifanye kazi tutunze shilingi ya Tanzania, tutunze uimara wa shilingi yetu kwa kuweka taratibu ambazo zitahakikisha kwamba tunasimamia udhibiti wa matumizi ya Dola ndani ya nchi yetu ili shilingi yetu ipande thamani.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naona muda uliobaki hautoshi, dakika kumi kwa mchangiaji anayefuata. Ningependa kutoa tangazo kwamba, baada ya Mheshimiwa Kabwe Zitto kujiuzulu Kamati ya Hesabu za Serikali wamefanya Uchaguzi wakiwa Dar es Salaam kabla ya kwenda safari yao Afrika ya Kusini, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau ndiye Mwenyekiti Mpya wa Kamati ya

Hesabu za Serikali. Akinamama hamumpigii hata makofi mwanamke, maana hiyo Kamati kubwa, eti, yaani hamumshangilii eeh! *(Makofi/Vigelegele)*

Kwa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC,* sasa ni Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau.

Baada ya kusema hivyo, Waheshimiwa tutarudi mchana, tutatoa nafasi ya wachangiaji wachache labda niwataje; atakuwa Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Josephine Gezabuke, Mheshimiwa Omar Nundu na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

Kwa hiyo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 6.54 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, wakati nasitisha shughuli za Bunge nilikuwa nimewataja wachangiaji ambao ni Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Mheshimiwa Agripina!

**MHE. AGRIPINA A. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niipongeze hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa mchango wao ambao umewasilishwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nadhani leo ni siku ambayo hata wewe unapumua, kwamba Serikali imeleta Muswada ambao leo tunakaa kama Wabunge wote bila kuvutana kwa maslahi ya Watanzania.

**SPIKA:** Si huwa mnataka tu kuvutana! *(Kicheko)*

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, naomba name niungane na wenzangu kusema kwamba Muswada huu ni muhimu kwa Watanzania, lakini pia naomba niungane na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwenye kifungu cha 7(9) kwenye utoaji wa leseni.

Mheshimiwa Spika, anayetoa huduma kama hatapewa au hatakubaliwa maombi yake, amepewa siku 30 kupeleka malalamiko yake kwa Gavana. Sasa sheria ni msumeno, naomba Muswada huu useme wazi kwamba, Gavana akipelekewa maombi, atachukua muda gani kutoa maamuzi ili kupunguza urasimu. Kwa sababu mtu anaweza akakataliwa maombi yake, suluhu ya mwisho ni kwa Gavana, matokeo yake anapeleka malalamiko kwa Gavana na Gavana anaweka kwenye droo anatulia. Kwa hiyo, ni lazima sheria iseme Gavana atachukua siku ngapi kutoa maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye sheria hii kifungu cha tisa (9), 10, 11 hadi cha 12, vifungu vyote hivi vinamgusa mlaji ambaye ni mwananchi, lakini bado sheria hii haijasema

kwamba mwananchi atakapokuwa amekosa huduma atatumia njia gani kufikisha taarifa zake za ucheleweshwaji wa huduma. Ni lazima sheria iseme kwamba kama unatunga sheria umempa mamlaka makubwa Gavana kwamba ndiye mwamuzi wa mwisho lazima na huyu mlaji apewe utaratibu na apate mwongozo, mahali ambapo amekosa haki yake ya msingi atachukua utaratibu gani ili kufikisha malalamiko yake mahali panapohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, leo tunasema kwamba mwombaji wa leseni kama vigezo havitakidhi, ikaonekana kwamba maombi yake hayakupokelewa, anatakiwa kwenda kukata rufaa yaani tuseme kama rufaa kwa Gavana, kwenda kupeleka malalamiko yake kwa Gavana ili ayapitie upya. Sasa najiuliza, haya malalamiko ili huyu mwananchi akiona kwamba hakuridhika, atachukua utaratibu gani wa kwenda kutoa hayo maelezo au atapitia wapi ili kufikisha hayo maelezo?

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi, Wabunge wengi wameongea, tuna malalamiko mengi kuhusu utoaji wa huduma kupitia *ATM, M-Pesa* na mambo mengine mengi, lakini wananchi wengi wanashindwa. Je, ukipata matatizo hayo unakwenda kwa nani? Kwa hiyo, sheria hii lazima itoe mwongozo kwamba mwananchi yeyote atakapoona anapewa huduma au ananyimwa stahiki yake wakati ni haki yake kupata huduma hiyo, anatakiwa achukue utaratibu fulani ili huyu Gavana au wahusika waweze kutatua tatizo lile mapema kabla ya malalamiko makubwa kama haya waliyokuwa wanazungumza Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye kifungu cha 17(7), hapa amepewa mamlaka tena Gavana. Narudia kusema kitu kinachowaumiza Watanzania wengi wanapinga urasimu. Walaji ambao ni wananchi na wawekezaji hakuna kitu kinachosumbua katika nchi yetu kama urasimu. Mtu ana haki ya kufanya shughuli Fulani, anapitia taratibu zote zinazostahili ambazo zimewekwa na sheria, lakini unamkuta kiongozi anapokea taarifa yako anaiweka pembeni. Urasimu unachelewesha maendeleo ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kifungu cha saba nacho ni lazima kiseme kwamba Gavana atachukua muda gani kutoa maamuzi hayo.

Mheshimiwa Spika, tuna mifano mingi na ndiyo maana unaona sheria hii inaungwa mkono na Wabunge wote, tumekumbana na matatizo mengi. Jana tulipata semina, tunawashukuru sana kwa kutufumbua macho, lakini kuna malalamiko makubwa sana ambayo yanatolewa kwa taasisi mbalimbali za Serikali, kwa mfano, Wakandarasi wa wananchi wetu, wanafanya biashara na Halmashauri au taasisi mbalimbali. Mtu akidai malipo yake kwa muda mrefu anaandikiwa *cheque*, akiipeleka benki anakuta akaunti aliyoandikiwa *cheque* ile hakuna fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini jana wataalam wetu wametupa semina kwamba sheria ipo ilitungwa tangu mwaka 1992. Sasa kama sheria hii ipo na watu wa Benki mnaielewa, ni kwa nini Mtanzania apewe *cheque* ambayo hela kwenye akaunti ile hakuna, ile *cheque* watu wa benki kwa nini wasiikamate, kisha wakamtafuta kama ni taasisi au Mkurugenzi akaenda kutoa maelezo, ni kwa nini anatoa *cheque* ambayo anajua kabisa kwenye akaunti ile hakuna fedha? Sheria ipo lakini haitekelezwi!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Wizara ya Fedha, sheria hii tunaipitisha wote kwa mikono miwili, inapopita wachukue hatua za haraka, kama ni kanuni zitengenezwe, ziletwe na zipitishwe ili sheria ianze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, tunapata shida sana sisi Wabunge wa vijijini, ukienda vijijini wananchi wamekuwa maskini kwa ajili ya taasisi za fedha ambazo zinatoa fedha bila utaratibu. Kwa mfano, tumekuwa na mgogoro wa muda mrefu wa *DECI*. Tuna Watanzania wengi sana ambao wamekuwa maskini kwa sababu ya *DECI*, ina maana sheria hii kama ingekuwepo, *DECI*

ingeweza kushughulikiwa mapema, lakini hakukuwa na sheria watu wanafanya kazi kwa namna wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, nimeongea mengi, kwa kweli Muswada huu siyo wa kukaza msuli sana, bali ni Muswada wa kufagilia. Naomba sheria hii ikafanye kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na iondoe ukandamizaji. Tunataka itumike kama ilivyopitishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ahsanteni kwa kusinikiliza na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa nashangaa unavyokaza misuli na Miswada, unakaza misuli tena!

Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Omar Nundu wajiandae!

**MHE. CECILIA D. PARESO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada ulio mbele yetu ambao ni Muswada unaopendekezwa kuwa na Sheria itakayodhibiti na kusimamia mifumo ya malipo ya aina mbalimbali nchini na mifumo kwa malipo ya elektroniki. Pia Muswada huu utaweka sheria ambayo itatoa uhalali na nguvu ya kisheria kuhusiana na malipo yote nchini.

Mheshimiwa Spika, kuwa na sheria ni jambo moja na ni rahisi sana kuitunga na kuiweka kwenye makaratasi, ikawa Muswada na kisha ikapitishwa kuwa sheria, lakini utekelezaji na usimamiaji wa Sheria ni kitu muhimu sana kuliko hata *process* ya awali ya upitishaji wa Muswada na hatimaye kupelekea kuwa sheria. Maana yake ni kwamba, tunaweza kuwa na Miswada mizuri, yenye maslahi mapana kwa masuala yote ya fedha na malipo mbalimbali nchini, lakini kama hakutakuwa na usimamizi thabiti wa mamlaka zinazohusika ambazo zimeainishwa katika Muswada huu, maana yake mwisho wa siku hata kama tunaunga mkono Muswada huu inakuwa haina maana yoyote kwa sababu umekosekana usimamizi na utekelezaji bora wa sheria husika.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe rai kwa Wizara husika lakini kwa Benki Kuu pia, ni muhimu sana wakasimamia sheria hii ipasavyo ili kutoa kabisa uhalali na nguvu ya kisheria kwa mamlaka zinazohusika nchini katika masuala yote ya uhamishaji fedha kutoka taasisi moja kwenye nyingine ama kutoka kwa mtu binafsi kwenda kwa mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Muswada huu pia kuna mambo ambayo yameainishwa ikiwemo hatua zote za maombi ya leseni, utoaji wa leseni, ku-*renew* leseni ama kufutwa kwa leseni. Yameainishwa katika vifungu mbalimbali yaani kifungu cha (9), (8) pamoja na vifungu vidogo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba imeoneshwa humu, lakini tutarajie na tuone kama Wabunge tunasisitiza ni lazima kuwepo na ufanisi na uharaka wa mlipaji na mlipwaji katika *transactions* zote za fedha nchini. Maana yake tutarajie kuona kwamba huduma inaboreka, inakuwa ya uharaka na ufanisi kwa sababu inapata nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, mfano tu, *process* ya kuhamisha fedha kutoka eneo moja kwenda lingine kwa kutumia mfumo wa *TISS*, unaweza ukachukua muda mrefu sana. Kuna wakati nahamisha fedha kutoka *account* ya *CRDB* kwenda *account* ya *NMB* kwa *TISS,* inachukua wiki nzima mpaka wiki mbili, ukiwauliza pale ambapo umeandika maombi yako ya *TISS* kwenda benki nyingine ambayo ni *CRDB,* wanasema tunafuatilia, hawakupi majibu ya uhakika. Sasa unajiuliza ni kwa nini? Ni udhaifu wa utendaji ama tatizo ni sheria ambayo haikuwekwa au ni

nini? Lakini hatutarajii hivyo, tunatarajia kwamba sasa tukipitisha Muswada huu kasoro hizi zote kwamba mlipaji na mlipwaji apate huduma kwa haraka na kwa ufanisi ambayo inawekwa na nguvu ya sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Muswada huu umeanisha mfumo wa ulipaji wa hundi kwa njia ya elektroniki. Tumeona na Wabunge wengi waliochangia kuanzia asubuhi wamelalamika, kuna wizi sana kupitia mitandao. Wengi wanaibiwa fedha au fedha zinahamishwa bila wao wenyewe wahusika kufahamu. Kwa hiyo, tunatarajia kama nchi ni lazima muangalie, kuwe na sheria ya namna gani tunakwenda kudhibiti wizi wa aina mbalimbali katika mitandao.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameeleza na kuna *crisis* kubwa sana *NBC* sijui kama Benki Kuu na Wizara husika wanafahamu. Watu wenye akaunti *NBC* wanalalamika ama ni *NBC* kwenda kufilisika hatujui, sababu hatujui! Kuna watu fedha zao zinahamishwa bila kujua, mtu yupo Arusha lakini akienda kuchukua *bank statement* inaonekana *ATM* yake ilitoa fedha Kenya au Oysterbay wakati yeye yuko Arusha. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa sana na ni muhimu sana mkaliangalia kupatia ufumbuzi lakini mkaja na mikakati ya namna ya kudhibiti wizi kupitia mitandao katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, dunia ya leo kuna kukua kwa teknolojia, ni vizuri sana kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania tukajifunza kwa nchi ambazo zimekuwa kiteknolojia katika kuimarisha na kudhibiti mifumo ya wizi wa kupitia mitandao. Kwa hiyo, tunatarajia pia pamoja na kupitisha sheria hii lakini mtakwenda kuliangalia suala hilo kwa umakini na kudhibiti wizi unaotokea kwa namna moja ama nyingine.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada pia inaonesha mfumo wa malipo na katika ulipaji kupitia simu za kiganja. Pamoja na kwamba mfumo huu ambao unatumiwa na watu wengi sana nchini sasa hivi, lakini kila kampuni inakuwa na kiwango chake, kama unahamisha 50,000/= kutoka *Voda, M-Pesa, Airtel Money au Tigo Pesa* kila kampuni inakuja na makato yake kulingana na ushindani wa makampuni ambavyo unakwenda sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ifike mahali kama mnaweza ku-*harmonies* hizi bei kuliko huyu anajiamulia na huyu mwingine anajiamulia kwa sababu mwisho wa siku anayebeba mzigo ni mwananchi anayetuma fedha na siyo makampuni kwa sababu kama unatuma kwa *M-Pesa* kumhamishia mtu mwingine wa *Tigo Pesa* au wa *Airtel Money* ambaye utakwenda kukatwa makato ya kusafirisha fedha ni wewe mtumiaji. Kwa hiyo, ni vizuri mkalitazama hili kitaalam zaidi, mkaona namna gani ya ku–*harmonies* hizi *price* ili ziwe ambazo hazimuumizi mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, pia ni muhimu kupitia *TRA* mkaangalia namna gani mtahakikisha kwamba makampuni haya yanalipa kodi ipasavyo. Katika bajeti zetu tulisema na Wabunge wengi walichangia sana, ni namna gani mnasimamia Makampuni ya Simu yanalipa kodi stahiki kupitia *TRA*, lakini pia ni namna gani TRA na yenyewe inafanya *monitoring* kwenye makampuni husika ili kujua je, kodi wanazolipa ama wanazotakiwa kulipa ndizo halali kulingana na huduma wanazotoa na mambo kadha wa kadha kulingana na uwekezaji katika makampuni husika. Kwa hiyo, ni muhimu sana kupitia *TRA* wakayasimamia haya ili makampuni yote yalipe kodi stahiki kwa manufaa ya Watanzania na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nyenzo za malipo kwa mujibu wa semina ambayo tumeipata jana kama Wabunge zipo za aina mbalimbali ikiwemo fedha *cash*, hundi, kupitia *Visa Card* au Mitandao, simu za kiganjani na mambo kadha wa kadha. Hata hivyo, walituambia kuwa nyezo zote hizi za kufanya malipo kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine zote zina

changamoto na ni muhimu sasa mkaangalia na kutatua changamoto zote kulingana na mfumo wa nyenzo za malipo nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana mkasimamia sheria hii, lakini kama kuna sheria nyingine ambazo zinahitaji ama kutungwa ama kurekebisha ili kuufanya mfumo huu uwe imara ni muhimu sana Serikali mkaleta kama ni Miswada hiyo, lakini pia mkaisimamia sheria kwa jinsi ambavyo inatakiwa. Pia ni muhimu mkajenga na kupanua uelewa wa teknolojia kwa watendaji wetu ambao wanasimamia sheria hii. Kama nilivyosema, sheria ni nzuri, Muswada ni mzuri, lakini ni namna gani unakwenda kujenga uelewa wa watendaji wetu ili tuendane na ulimwengu wa sasa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kuna wizi kwenye mitandao, lakini kuna nchi nyingine ambazo inaweza kuwa ni *best practice* kwa sisi kwenda kujifunza na kuangalia ni namna gani tunakabiliana na changamoto zilizopo mbele yetu katika suala zima la wizi kupitia mitandao hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu na naunga mkono pia hotuba ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Josephine Genzabuke na baadaye Mheshimiwa Omar Nundu na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir ajiandae!

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Muswada huu wa Mifumo ya Malipo nchini, 2015.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu wa Sheria ya Mifumo ya Malipo Nchini wa mwaka 2015, naipongeza sana Serikali. Serikali imefanya jambo la maana sana kwa sababu sheria hii imechelewa, imeletwa wakati huduma za fedha zimekuwa zikifanyika na hivyo wananchi wengi wameumizwa na wamedhulumika kupitia mitandao hii ya fedha.

Mheshimiwa Spika, naamini sasa kupitia Muswada huu tutakapokuwa tumeupitisha na Kanuni zikaandaliwa zikaletwa, ni lazima zitumike ili wananchi sasa waweze kufaidika kupitia Muswada huu kwa sababu wamedhulumika kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo faida nyingi zitakazopatikana kupitia Muswada huu utakapokuwa umepita. Kwanza, Muswada huu utakapokuwa umepita, kutaongezeka fursa za kijamii na kiuchumi, hivyo, kuleta maendeleo endelevu kwa wananchi. Mfumo huu utaongeza usalama wa fedha katika taasisi mbalimbali ikiwa ni katika Benki, Makampuni ya Simu, mfano *Tigo Pesa, M-pesa* na *Airtel Money*. Wananchi wengi wamepoteza na kuibiwa fedha kutokana na kwamba hakukuwa na sheria yoyote, lakini sheria itakapokuwa imepitishwa wananchi hawatadhulumika tena.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine ya mfumo huu ni kwamba, itapunguza msongamano katika benki na kampuni za watu binafsi zinazotoa huduma kwa njia ya mtandao. Pia mfumo huu utawawezesha wananchi kurahisishiwa huduma mbalimbali kwa sababu wakati mwingine wanapokuwa wanakwenda kwenye benki wanakutana na adha kubwa sana kama vile foleni kubwa, wakati mwingine wakiwa pale wanaibiwa, lakini huduma hii itakapokuwa imeboreshwa wananchi wataweza kunufaika kupitia huduma hii.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu utatusaidia kutuma fedha kwa urahisi. Kwa mfano, kulipia ada za magari yetu, ankara za maji na umeme na hata kununua bidhaa kwa njia ya mtandao. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kuweza kuliona hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida ambazo zimekuwa zikipatikana hata kabla ya Muswada huu kuletwa humu Bungeni, ziko changamoto mbalimbali ambazo wananchi wamekuwa wakikutana nazo. Kwa mfano, wananchi wakati mwingine wamekuwa wakituma fedha kwa njia ya *M-pesa*, akikosea namba moja tu badala ya fedha kwenda kwa mlengwa, inahamia kwa mtu mwingine. Ikiishahamia kwa mtu mwingine kupata fedha ile inakuwa shida.

Mheshimiwa Spika, mwanzo watu wa *M-Pesa* waliwaambia watu kwamba, ukihamisha fedha na bahati mbaya ikaenda kwa mtu mwingine unatakiwa kupiga namba 15366. Hata hivyo, wananchi wamekuwa wakidhulumiwa, wakipiga simu kwenye namba hiyo waliyoelekezwa na *Vodacom* badala ya kupata huduma wanawekewa muziki. Muziki unalia na matokeo yake akija kupiga simu ili apatiwe huduma fedha ile inakuwa imeshahamishwa imepelekwa sehemu nyingine. Kwa hiyo, wananchi wamekuwa wakipata hasara sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara, tumekuwa tukiuliza maswali wakati mwingine tunapokuwa kwenye Kamati ili ufumbuzi uweze kupatikana, lakini mpaka sasa hivi ufumbuzi haujapatikana na wananchi wameendelea kupoteza fedha zao, pale tu inapotokea bahati mbaya wamekosea namna moja tu, ambapo kwa binadamu kukosea ni kitu cha kawaida, lakini wamekuwa wakipata hasara.

Mheshimiwa Spika, mwanzo ilikuwa ni kwamba, yule mwenye akaunti aliyepokea fedha, akaunti yake inafungiwa, lakini baadaye walisema mwenye akaunti hawezi kufungiwa akaunti yake kwa sababu anaweza akashtaki na kampuni ikapata hasara. Sasa nauliza hili tatizo la wananchi kupoteza fedha kwa kukosea namba moja na wakiomba kupata huduma wanaambiwa kwamba, ni kwa nini wamekosea, hili tatizo Serikali italitatuaje?

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa sana kwa sababu watu wanapoteza fedha kwa kukosea namba, fedha zinakwenda sehemu nyingine, wakiomba huduma wanawekewa mlio kwenye simu na matokeo yake wakija kupata huduma fedha zimeshahamishiwa sehemu nyingine, wanakosa pa kulalamikia. Mwanzo akaunti zilikuwa zikifungwa, lakini walishasema hawawezi kufunga. Je, ni kwa nini tatizo hili Serikali isilishughulikie?

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichotaka kuzungumza ni kwamba, kumekuwa na wizi kupitia mitandao. Hili kila mtu analifahamu, wapo watu ambao wametekwa na wakachukuliwa na baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu, wananyang'anywa kadi zao na wanaambiwa sasa waende kutoa fedha kwa njia ya *M-Pesa*. Mtu anakuwa amenyang'anywa simu yake, labda simu yake inakuwa na shilingi milioni moja, anapelekwa anaambiwa tunaomba ututajie namba yako ya siri ili tuweze kutoa fedha. Wananchi wengi wamepoteza fedha kwa kupitia njia hiyo, lakini bado ufumbuzi haujapatikana. Kwa hiyo, nafikiri sheria hii itakapokuwa imepitishwa wananchi hawataibiwa. Ni wakati muafaka Waheshimiwa Wabunge wote kwa pamoja tuipitishe sheria hii ili wananchi wetu wasiendelee kudhulumika.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho, niseme kwamba, ni kweli sheria ilichelewa, lakini sasa umefikia muda wake, naomba Waheshimiwa Wabunge tuipitishe. Ikiishapitishwa ni lazima Kanuni za Sheria hii ziletwe mapema ili wananchi waweze kunufaika kupitia Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muswada ukipita Kanuni zinatungwa na Serikali, hawaleti huku. Hilo watafanya wenyewe, lakini hawataleta huku.

Mheshimiwa Omari Nundu na Mheshimiwa Zubeir jiandae!

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie katika Muswada huu. Awali ya yote niipongeze Serikali kwa kuleta Muswada huu wakati huu muafaka. Mwanzo kabisa niseme naunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Muswada huu iko wazi, kuna taratibu na tahadhari. Sasa Muswada tunao hapa, kazi tuliyonayo ni kuuboresha hii leo na hali kadhalika baadaye kwani leo ni mwanzo tu. Wachangiaji wamekuwa wengi, wamechangia vizuri na nisingependa kurudia yale ambayo wameyasema, lakini nataka kusisitiza baadhi ya mambo, kwanza ni Kanuni. Muswada huu ukiishapita na kuwa Sheria, Serikali itayarishe Kanuni ili sheria iweze kutumika mara moja.

Mheshimiwa Spika, yaliyomo katika Muswada yanahitaji ufuatiliaji wa kudumu (*continuous monitoring*) wa karibu sana. Hivyo, basi Benki Kuu tuwe na Kitengo Maalum chenye wataalam waliobobea kwenye fani hii ili wafuatilie yafuatayo:

Utendaji wa wahusika, utaalam unaoibuka duniani na pia taratibu na Sheria za Kimataifa kwenye mambo haya, ili tuweze kudhibiti na pia twende sambamba na dunia. Sheria hii ni muhimu kutuwezesha tufanye miamala kwa kujiamini. Hicho ndicho cha muhimu, tumekuwa tunaifanya lakini hatukuwa na sheria ambayo inatulinda kwa hilo. Sasa wakati umefika tunayo sheria, hivyo tuongeze utumiaji wa miamala ya kielektroniki.

Mheshimiwa Spika, tuwe na tahadhari na si uoga ili tuendelee kwa kasi kubwa kushiriki kwenye utandawazi wa dunia na hatuna jinsi ni lazima tufanye hivyo. Taarifa za *World Bank* na *FinScope* za 2010 ziliainisha hivi kuhusu Tanzania, kuwa ni asilimia 14 tu ya watu wazima Tanzania ndiyo wanaotumia huduma za benki, lakini asilimia 43.5 wanafanya miamala yao kwa simu. Kwa hiyo, njia hii imekubalika, inatumiwa, tuna uzoefu na sasa inabidi tuendelee nayo. Kwa hiyo, hii sheria ni njia ya kuongeza ufanisi na usalama wa kitu ambacho kimeshakubalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo matatizo yaliyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na mimi nimeona matatizo ya aina mbili; la kwanza ni wizi, Wabunge wengi wameongelea aina mbalimbali za wizi. Pia kuna tatizo la mwenendo wa miamala hasa pale ambapo malipo hayafiki sehemu ambazo zinatakiwa kwa wakati. Serikali hili imeliangalia hili la pili na Sheria imeweka kwamba, kuwe na faini kwa wale watu ambao watakuwa wanachelewesha.

Mheshimiwa Spika, tunajihami vipi na akina *Western Union, Money Grams* na kadhalika, kwenye masuala ya wizi ambao sasa hivi huduma zao zinatumika duniani kote? Pia tunajihami vipi na hizi huduma nyingine ambazo zinatolewa nyuma ya sheria, kama *PayPal***,** *Scams* za aina mbalimbali ambazo sasa hivi ziko 419 kama *Ponzi Schemes* ambazo zimeenea duniani. Itabidi tufanye jitihada za kuhakikisha kuwa tunaweka vitu katika sheria hii ili tujihami na hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunalindaje kampuni zetu za simu? Desemba mwaka 2014 Nairobi, *Safaricom* ambayo inahusiana sana na *Vodacom* waliibiwa shilingi za Kenya milioni 600 moja kwa moja na ukienda kiujumla inaonekana fedha ambazo zimeibiwa ni takribani shilingi bilioni tatu. Sasa kwanza *Vodacom* imeathirika vipi kwa fedha ambazo zimeibiwa huko *Safaricom* ambao wanashirikiana nao?

Mheshimiwa Spika, pia *Safaricom* imewaachisha kazi wafanyakazi 41 ambao sasa watatafuta ajira sehemu nyingine. Huku tumesema watu ambao wanahusika kwenye vitu hivyo wasiajiriwe popote, lakini tutafanyaje ili watu ambao wanatoka nchi nyingine hasa za jirani ambao watakuja kutafuta ajira hizi hapa ili kuhakikisha tunafanya utafiti wa kina kuhusu anakotoka ili nao pia sheria ile ya kwamba wasipate ajira kwenye huduma hizi tena iwe inatumika?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka niende moja kwa moja kwenye sheria husika niangalie vipengele ambavyo naomba viboreshwe. Jambo la kwanza nataka kusisitiza kuwa katika kufuatilia haya ambayo yako katika sheria hatuhitaji kwenda kufanya *inspection* tu kama ambavyo imeelekezwa kwenye sehemu hapa. Tunahitaji tuwe na *continuous monitoring* hata kama itabidi ufanyike *electronically* bila ya mtu kwenda kule ambako kunahusika ili wakati wowote likitokea tatizo tuwe tuko tayari kukabiliana nao.

Mheshimiwa Spika, katika aya za rufaa, aya ya (7) mpaka ya (9), tumeona hizi aya ni *closed systems* kwani zinaongelea ndani ya Benki Kuu tu mpaka mtu wa mwisho wa kufanyiwa rufaa ni Gavana, halafu hakuna mwelekeo, yaani ni *end closed,* Gavana atatoa uamuzi gani haisemwi. Sasa kama Gavana siyo *end closed,* hii haina tatizo kwa sababu bila shaka kuna mfumo wa kwenda ku-*appeal* mahali pengine, lakini kama Gavana ndiyo mtu wa mwisho, hiyo inanipa shida kidogo. Tutafute njia ambayo itawezesha kuwa na mtu mwingine wa kuwasaidia hawa ambao wanakata rufaa kupata haki yao.

Mheshimiwa Spika, katika adhabu zilizotolewa na nawasifu sana Serikali kwa kubadilisha na kuweka mfumo ambao wameweka adhabu kubwa na wameweka adhabu kubwa pale ambapo tulisema adhabu zilizowekwa mwanzo ni ndogo, lakini adhabu kubwa wanazosema ni kiwango kisichozidi kiasi fulani, ukiacha wazi hivyo ni kuonesha kuwa, inawezekana kabisa Mahakama ikatoa adhabu ambayo ni ndogo kuliko ile iliyokuwepo pale mwanzo.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba zile adhabu za kwanza zirekebishwe labda kwa kuongezwa shilingi milioni tano kwa kila moja, ziwe ndiyo adhabu za kuanzia, halafu hizi zilizoletwa baadaye ambazo ni kubwa ziwe ndiyo adhabu za juu kwa maana ya faini.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 23 kinaongelea kwamba, panapokwenda Mahakamani utolewe ushahidi kukiwepo na *essential details* za *cheque*. Ushauri wangu ni kuwa kusiwe na *essential details* tu kwa sababu zinaweza zikapelekwa namba tu, lakini pia kuweko na *electronic picture image* ya hiyo *cheque* ili kila kitu kiwe kimekaa wazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 48, kuna neno "*immediately*" au mapema iwezekanavyo na hii inaendana na faini ambayo watatozwa wale ambao hawakulipa zile fedha kwa wakati unaotakiwa. Ningeomba kipengele hiki kipewe sifa ili iwe wazi ni siku gani zile fedha za faini za ziada zitakuwa zinaanza.

Kifungu cha 50 kinasema atajumuisha kwa kupokea fedha kutoka kwa mtu huyo na ni Gavana na mtu aliyemteua. Najiuliza ni kwa nini mfumo wa kulipa fedha hizo usifuate mfumo uliopo benki ili fedha hizo kama nimeelewa sawasawa kifungu hiki kinasema akabidhiwe mtu mmoja?

Mheshimiwa Spika, niipongeze na kuishukuru tena Serikali kwa kuleta Muswada. Watu wanasema umechelewa, haukuchelewa, lakini nasema hiyo kwangu si hoja, hoja ni kwamba Muswada sasa uko hapa tuurekebishe twende mbele. Nilikuwa najiuliza hapa, Nabii Musa alipopewa *Ten Commandments* angeweza kusema zimechelewa wakati *commandment* ya sita inamwambia asiue na yeye ameshaua, sijui tungekuwa tuko wapi sasa?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante. Mheshimiwa Said Musa Zubeir!

**MHE. SAID MUSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili kuweza kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Mifumo ya Malipo. Kwanza na mimi niwe kama wenzangu niunge mkono kwa asilimia mia moja. Hili jambo limekuja nasema kutokana na kawaida yetu Watanzania kusubiri mambo na kuyafanya kwa uhakika, nasema huu ni wakati muafaka. Tumepata fursa ya kusoma changamoto nyingi za wenzetu ambazo zimewakumba wakati walipoanzisha hii mifumo. Kwa hivyo, kuja kwetu tutakuwa na marekebisho mengi ambayo yataufanya huu Muswada uweze kufanya kazi vizuri kwa upande wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme njia hii ya kutuma fedha kwa elektroniki kuanzia mwaka 2014 mwishoni mpaka Februari, 2015 kwa tathmini tulizonazo kuna *transactions* karibu mia mbili na kidogo hivi, lakini kuna wingi wa fedha takribani shilingi trilioni 12.5 au 13 kwa kipindi hiki kifupi.

Mheshimiwa Spika, nimesema nizungumze hili lengo langu kubwa likiwa ni kuitanabahisha Serikali kwamba, ni lazima tuwe na *plan B* iwapo hii tuliyonayo, aidha, kwa bahati mbaya au makusudi inaweza ika–*collapse*. Si jambo la kutegemea, lakini ufanisi ulio mzuri kwenye kazi na ukishaona kuna jambo ambalo linafanya kazi vizuri na lina *demand* kubwa kwa watu basi ni lazima ulitazame mara tatu tatu, siyo mara mbili.

Mheshimiwa Spika, pia ni lazima tuwe na mfumo unaofanana na huu ambapo pindi likitokezea tatizo basi tunajua kwamba, ni wapi tuna–*recover* bila ya kubabaika na kwa wakati muafaka. Hili naiomba sana Serikali ilichukue, ilijue tusije tukabakia tu kwenye eneo moja, tusije tukapata matatizo tukawa sasa hatuna pa kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine tuje kwenye faida za huu mfumo yaani baina ya anayelipwa na mlipaji. Ni matumaini yangu kwamba, Sheria hii ya Mifumo ya Malipo itaondoa kero nyingi zikiwemo za mabenki ambazo wenzangu wamezizungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukapata *cheque* leo na hasa watu hawa, watu wa kati ambao hawana kipato kikubwa, mtu anakwenda benki amelipwa *cheque* yake leo, ameichukua na kuipeleka benki lakini anatakiwa alipwe na benki nyingine, anapokwenda aka–*submit* ile *cheque* kwenye ile benki yake yeye anaambiwa subiri siku nne.

Mheshimiwa Spika, anapoambiwa hivyo ni kwamba, pengine amepeleka *cheque* ile saa saba siku ya Jumatatu anaambiwa subiri Jumanne, Jumatano, Alhamis, Ijumaa na Ijumaa yenyewe pengine ataambiwa aende mchana saa tisa. Hii ni sawa sawa na mtu huyu kuambiwa kwamba, fedha zake atazipata baada ya wiki moja.

Mheshimiwa Spika, sasa ni matumaini yangu kwamba huko tunaweza tukaondoka na sasa ikawa mtu yuko *up todate* na akaweza kujipangilia na biashara zake kwa uhakika ambao yeye mwenyewe alikuwa tayari alishapanga kwamba nilikuwa na shida ya kiasi fulani na nimepata cheki yangu ni hii, sasa nitakachokifanya ni hiki.

Mheshimiwa Spika, lingine, kuna suala la faini. Nilipata wasiwasi kidogo, lakini baada ya kuona *amendment* ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kidogo imenipa matumaini. Ukweli ni kwamba mzunguko wa fedha ni mkubwa, makampuni yanayofanya, ni tajiri yenye fedha zao lakini tulipokuwa tunasoma hii Sheria yenyewe tulipoletewa, faini zilikuwa ndogo. Lakini kwa

marekebisho haya ya kutoka angalau kwenye hii 50 ikaja mpaka 500, hata nami nimeridhika kidogo.

Mheshimiwa Spika, kubwa nitakalosema ni kwamba kuwe kuna faini pamoja na angalau kuwazuia kama kwa miaka miwili. Mtu anapigwa faini, kwa mfano milioni 500 au na zaidi lakini *atleast* kuwe na kuambiwa, Bwana tuna ku-*suspend* kwa kipindi cha *atleast* miaka miwili au mitatu usifanye hii kazi, utakuwa uko chini ya uangalizi. Hii inaweza kusaidia, tofauti na vile ilivyokuwa mwanzo, Shilingi milioni 50; na kwa *individual cases* hizi za mtu mmoja mmoja ilikuwa kwenye Shilingi milioni 10. Hii kidogo ilikuwa haionyeshi kwamba kweli tunataka tuwe na Sheria nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa viwango hivi vilivyowekwa sasa hivi, hata mimi nimeweza kuvutika nikajua kwamba sasa tunaweza kufanya kazi vizuri. Hili nimelisemea kwasababu kuna tofauti ya makampuni makubwa na watumiaji wadogo.

Kuna *transaction* ya karibuni yenye thamani ya Shilingi trilioni tatu mpaka nne, ambazo hizi ndani ya kipindi cha miezi mitatu au minne huwa zinafanywa na watumiaji, yaani wananchi wenye kipato cha hali ya chini. Hata Wabunge hapa wamelizungumzia hili kwamba wanapata matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, ukweli kampuni kuiwekea *amount* ndogo kama ile iliyokuwa mwanzo ilikuwa ni kuendelea kuwaumiza hawa wananchi. Lakini kidogo kwa kupandishwa huku watakuwa na wao wana umakini wa kukaa na kufikiria kwasababu mwananchi anachoona ni kwamba anatuma pesa zake, anapeleka kwenye M-Pesa halafu anampigia simu mwenzie kule anamwambia kuwa nimeshakutumia, yeye anakwenda upande wa pili, anatoa. Lakini kilichokuwepo nyuma ya pazia ingekuwa wananchi wanakijua, halafu mfano wangejua kwamba hata Sheria ilikuwa hakuna, wasingeweza kuifanya hii biashara. Kwasababu kuna mlolongo mrefu na kama una uelewa nini kinachoendelea huko nyuma ya pazia, palikuwa pana uzito mkubwa sana

Mheshimiwa Spika, kwa ujio wa Sheria hii, pamoja na marekebisho haya yanayofanywa, inaonekana dhahiri kwamba kweli tunataka kuwasaidia wananchi wenye kipato cha chini waweze kufikisha fedha zao mahali husika kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, hili limethibitika baada ya kuonekana kwenye Ibara ya 4(2) ambacho kimefanyiwa marekebisho kuachiliwa nafasi Gavana angalau kufanya maamuzi kuondoa ukiritimba au urasimu ambao uko Serikalini. Hapa Serikali imejionyesha kwamba inao uwezo wa kujisahihisha yenyewe na matatizo ambayo yanaweza tukayakabili na tuna uwezo wa kuyatatua sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nami niseme kwamba nimefurahi, hili bado halijachelewa, isipokuwa ni matumaini yangu kwamba tutakuwa tuna marekebisho madogo madogo kufuatana na ukuaji wa TEHAMA siku za usoni. Lakini kwa sasa hivi hii iko *reasonable* na inaweza ikatumika vizuri.

Sasa tuwaombe tu, kama alivyozungumza Mheshimiwa Spika, kwamba kanuni hatuletewi hapa, tunajua kuwa Kanuni hatuletewi hapa, lakini basi wakitoka hapa wasije wakageuka kama Wakenya. Walipitisha Sheria halafu wakakaa zaidi ya miaka minne, mitano bila ya Kanuni na iliwapa shida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiondoka hapa, kwasababu kuna watu pengine huko nyuma walikuwa hawajui kama tulikuwa hatuna hii Sheria, pengine hii kuzungumza yetu ndiyo

wanafahamu kwamba kumbe hii miaka yote sisi tunafanya tu. Kwa hiyo, kuna majambazi wamekaa *standby* kutafuta njia ya kuweza kunanii. Wanaweza kwa kipindi hiki kifupi, baada ya kuwatanabahisha kuwa ndiyo Sheria tunaifanya, wao sasa ndio wakaanza ujambazi wa kuwaibia watu fedha nyingi badala ya huo uliokuwa nyuma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Sayansi na Teknolojia na TEHAMA! Wewe nakupa dakika 15.

**WAZIRI WA SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Sawasawa Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Muswada huu wa Sheria iliyopo mbele yetu, kwanza tukubali kwamba Sekta ya Mawasiliano imekua kwa kasi kubwa. Mwaka 2010 wakati naingia Wizara hii tulikuwa na watumiaji wa simu kama milioni 10 na leo hii tunazungumzia watumiaji wa simu karibuni milioni 32. Mwaka 2010 watumiaji wa *internet* walikuwa kama milioni tano, na leo hii tuna watumiaji milioni 11.3. Mwaka 2010 kwa upande wa pesa watumiaji wa pesa walikuwa ni kidogo sana lakini leo hii tuna Watanzania karibuni milioni 12.3 wanatuma pesa kwa kutumia mitandao mbalimbali ya simu.

Mheshimiwa Spika, nataka kuchukua fursa hii kushukuru Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kwa kuanza kulifanyia kazi jambo hili na leo hii tumefika hapa tulipo, hata mama yangu aliyeko Kijijini anaweza kutuma pesa kumpelekea ndugu yake mwingine, nami naweza kumtumia na kupokea. Zamani hasa kwa sisi tuliokuwa tunatoka vijijini ilikuwa ni vigumu kutuma pesa kwa wazazi wetu, lakini leo hii tuna bahati kwamba tunaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mbali ya kukua Sekta ya Mawasiliano lakini kumetokea changamoto nyingi sana. Ndani ya Bunge, kila mmoja wetu amekutwa na kadhia pengine ya kuibiwa au kudanganywa. Kuna watu wamenyanyaswa kwa kutumia mitandao, kwa vile sisi tunakubali kama Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Technolojia kuna changamoto nyingi na watu wengi wameathirika.

Mheshimiwa Spika, waathirika wa uhalifu wa mitandao ni pamoja na sekta binafsi, watu binafsi, sisi Waheshimiwa Wabunge pamoja na wazazi wetu na ndugu zetu na pia pamoja na jamii yote na wananchi wote kwa ujumla. Aidha, katika kipindi cha hivi karibuni, kumekuwepo na ongezeko kubwa la uhalifu katika mitandao katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ambalo uhalifu umeongezeka ni wizi wa fedha kwa kutumia mitandao, yaani kwenye M-Pesa, *Tigo Pesa, Airtel Money* na Z-Pesa ya *Zantel* kumetokea ongezeko kubwa la uhalifu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni wizi wa taarifa binafsi za kwenye mitandao. Watu wameibiwa taarifa zao na zimepelekwa huku na huku ambalo ni jambo baya.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo limekuwa na changamoto kubwa ni uchochezi, udhalilishaji na vitisho kwa kutumia mitandao. Wengi kati yetu hapa wamepokea *messagei* na maneno ya uchochezi na vitisho kupitia mitandao.

Mheshimiwa Spika, pia kumetokea udanganyifu wa kutumia *computer,* tumepata *message* kutoka sehemu mbalimbali nje kwamba Baba yangu alikuwa tajiri, nitume pesa hapa na pale yote haya ni kupitia kwenye kompyuta.

Mheshimiwa Spika, kumetokea tatizo lingine ambalo ni kughushi nyaraka mbalimbali kwa kutumia kompyuta. Leo umepata *document,* kesho imeghushiwa, hujui imetoka wapi, ni *same document* lakini ni *document* ya uongo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la upangaji wa utekelezaji wa matukio ya ugaidi kwa kutumia mtandao. Haya tumeyaona katika baadhi ya nchi za jirani, watu wametumia mitandao katika kutekeleza hizo hujuma za ugaidi. Nchi nyingi hapa na nchi nyingine mbalimbali kumetokea wizi kwenye *ATM,* watalaamu wanaita *ATM Scheming,* yaani unakwenda na kadi yako halafu unaibiwa pesa zako kwa kutumia mitandao ya *ATM*.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kwamba katika mwaka 2012 kulikuwa na matukio 444, mwaka 2013 kulikuwa na matukio ya uhalifu kupitia mitandao 355 na mwaka 2014 kulitokea matukio 215. Matukio haya siyo kwasababu yanashuka, isipokuwa pengine hayakuripotiwa vilivyo. Aidha, jumla ya kesi 212 zenye watuhumiwa 132 zilishafikishwa Mahakamani na sasa hivi zinafanyiwa kazi na kesi 787 ziko katika hatua mbalimbali za upelelezi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wizi wa fedha kupitia mitandao ya simu, yaani M-Pesa, Tigo Pesa, *Airtel Money* na Z-Pesa ya *Zantel*, kinachotokea ni kwamba wezi au wahalifu wanapata taarifa ya mwenye akaunti au kutoka kwa mwenye akaunti mwenyewe au kwa njia nyingine. Wanapata taarifa ya siri na wakishapata taarifa ya siri hiyo wanaitumia kukuibia au kuhamisha hizo fedha kutoka sehemu moja kupeleka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwaasa Watanzania wanaotumia huduma za aina yoyote ya mtandao kujiepusha na kutoa taarifa zao za siri. Ni muhimu kwamba wahakikishe hata kama ni ndugu yako, tafadhali usimpe taarifa yako ya siri kwasababu hujui ana nia gani katika kuangalia akaunti yako.

Pia nachukua nafasi hii kuwafahamisha Watanzania na Waheshimiwa Wabunge ya kuwa vilevile msitoe taarifa zenu binafsi, kwasababu ukitoa taarifa binafsi watu wanaweza kutumia taarifa hizo kuweza kuingia katika mtandao wako na kuweza kufanya hujuma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wale wanaotumia kompyuta, hii ni muhimu sana kutengeneza *password* ambayo siyo rahisi mtu mwingine kuweza kuighushi.

Kwa mfano, mimi kwenye kompyuta nikitumia *password* "Makame" mtu anaweza kuja mara moja akaingia tu. Anatumia jina langu, anajaribu jina la Babangu, anajaribu jina watoto wangu na mke wangu, anaweza kuingia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi kutayarisha *password* ambayo mtu kughushi inakuwa ni vigumu, *then* hapo pesa zako ama habari zako katika mtandao zitakuwa salama. Aidha, kwa lengo la kuongeza usalama wa matumizi ya huduma za kimtandao, Wizara imekamilisha Miswada miwili ambao wa kwanza utakuwa ni Sheria ya Udhibiti wa Uhalifu wa Mtandao *(Syber Crime Act)* mwaka 2015 na Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, *(Electronic Transaction Act)* ya Mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, Jumapili hii inayofuata tutaanza Semina kwa ajili ya Miswada hiyo na Jumatatu Miswada hii italetwa hapa Bungeni. Nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, wakati wa semina mje kwa wingi na mchangie kwenye Miswada hii kwasababu ni muhimu katika kulinda huduma hizi za mitandao. Sheria hizi zitazingatia mambo mbalimbali ikiwemo kuainisha makosa na adhabu dhidi ya makosa ya uhalifu ya mtandao, kuainisha Kanuni na taratibu za upelelezi na uendeshaji mashtaka ya makosa ya uhalifu wa mtandao na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, Sheria hizi zitakapokuwa tayari tunaamini kwamba kwa asilimia kubwa ya uhalifu tunaoona leo utapungua na tunaamini kwamba tutajengea uwezo vyombo vyetu vya usalama kama Polisi na vyombo vyote vya Serikali ili kupambana na uhalifu unaowakabili wananchi wetu kupitia kwenye mitandao.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kuhusu *policy* ya vifurushi au Sera ya vifurushi. Naomba nichangie kwamba vifurushi vilianza mwaka 2013. Vifurushi hivi havikuja kwa bahati mbaya, sisi Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Technolojia tulileta Sera ya kuanzisha vifurushi kwasababu bei ya upigaji simu kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine ilikuwa ni kubwa mwaka 2013 kwa dakika moja kuunganisha kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine. Kwa mfano, kutoka *Zantel* kwenda *Airtel* ilikuwa ni Sh. 115/=. Baada ya kuteremsha bei hiyo, sasa imekuwa ni takribani Sh. 35/= kwa dakika. Matokeo yake ni kwamba makampuni mengi yakaanzisha vifurushi na leo hii tunaona faida kubwa ya vifurushi.

Mheshimiwa Spika, nikikupa mfano tu, mwaka 2006 kupiga simu kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine, kwa mfano kutoka *Airtel* kwenda *Zantel* kwa dakika 175 ilikuwa ni Sh. 49,000/=. Mwaka 2010, kupiga mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine kwa wastani ilikuwa ni Sh. 46,000/=. Leo hii kupiga mtandao mmoja, kwa mfano kwa mfano *Airtel* kwenda *Zantel* kwa kutumia vifurushi, unatumia karibu Sh. 10,000/=, ambalo ni pungizo la takriban la asilimia 87.

Mheshimiwa Spika, hii yote isingepatikana isipokuwa kwa kuingiza vifurushi. Vifurushi vimeleta faida kubwa, lakini vilevile vimeleta changamoto, tunajua. Kuna malalamiko mengi kwamba watu wengi wanaibiwa kwenye vifurushi. Kwa hili tunaweka Kanuni nzuri kuhakikisha kwamba hujuma kama hii ama wizi kama huo usiweze kutokea tena.

Mheshimiwa Spika, kuna suala vilevile lilihusu milio ya simu. Suala hili limeletwa kwenye Bunge lako na Wizara yangu sasa iko katika hatua za kuhakikisha kwamba tunatayarisha Kanuni ambazo zitasimamia milio ya simu. Watu wengi wanaibiwa na tunajua kwa vile sisi Wizara ya Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania tunatayarisha Kanuni ambazo mtu mwenyewe atapewa haki ya kuamua *wheather* anataka mlio wa simu au hapana, kwasababu bila kufanya hivyo tunaona watu wengi wanaibiwa sana.

Kulikuwa na suala lingine kuhusu kuibiwa kwenye mitandao kupitia *Electronic Magnatic Pulse*. Hili suala litazungumzwa vizuri kwenye sheria yetu inayokuja Jumatatu. Tunachukua fursa hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge tushirikiane kuhakikisha sheria hizo zinapita kwasababu ni muhimu sana. Huko tunakoelekea kwenye Uchaguzi kutakuwa na *message* nyingi za uchochezi, za vitisho. Kwa hiyo, nachukua fursa hii ili kuhakikisha kwamba tushirikiane kupitisha sheria hizo mbili ambazo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo machache, naomba nami niwapongeze wenzangu wa Wizara ya Fedha kwa kuleta Muswada huu muhimu ambao utaleta maendeleo makubwa katika Sekta yetu ya Fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha! Ni sehemu ya kujibu sasa, unatakiwa ukae hapa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha sijui mligawana dakika ngapi?

**WAZIRI WA FEDHA:** Dakika 15.

**SPIKA:** Dakika 15!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa niaba ya Waziri wa Fedha katika Muswada huu muhimu sana kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia kwa upana suala hili na nianze pia kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao waliyotoa katika ngazi ya Kamati na mpaka kwenye semina jana na maeneo mengine mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kimoja kilichojitokeza sana katika michango hii wakati wa mjadala…

**SPIKA:** Wewe! Mimi naitwa Spika. Umekazana tu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa!

**SPIKA:** Mimi naitwa Spika. Wewe unaniita Naibu Spika, nimekunyamazia, nimeona tena unaendelea tu. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuliweka sawa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu kama alivyosema Mheshimiwa Jafo ni mtambuka. Kwa hali ya maendeleo ya kijaamii na ya kiuchumi tuliyofikia sasa hivi, Muswada huu unakata kwenye maeneo mbalimbali ya jamii yetu na maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamesema kwamba Muswada huu umechelewa, ni kweli. Lakini Muswada unavyoandikwa sasa hivi mwaka 2015, sivyo ambavyo ungeandikwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wamesema Muswada huu umechelewa, ni kweli lakini Muswada unavyoandikwa sasa hivi mwaka 2015 siyo Muswada huu kama ambavyo ungeandikwa 2005, *it would have been totally different Bill.* Huu unavyoandikwa sasa hivi unazingatia hatua ya maendeleo ya sayansi na teknolojia tuliyofikia Watanzania leo, lakini pia Muswada huu umepata nafasi ya kuangalia maeneo waliyojikwaa wenzetu wote waliotangulia.

Mheshimiwa Mnyika amesema sisi na Zambia tunafanana na kadhalika. Siyo kweli! Sisi na Zambia hatufanani. *As a matter of fact,* katika matumizi ya sayansi na teknolojia Profesa Makame angenisaidia, lakini Tanzania kwa matumizi ya simu kama huduma kwa wananchi tupo mbali sana kuliko nchi nyingine nyingi za *Sub Saharan Africa*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme na ninawashukuru Mheshimiwa Zungu, Mheshimiwa Chomboh, Mheshimiwa Nundu, Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Mnyaa. Wamezungumzia suala la usimamizi wa ule mfumo wenyewe *(Networking),* kwamba mfumo huu unajioanisha vipi na mifumo mingine ya usimamizi kama *TRA, TCRA*, mabenki na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nundu nadhani na Mheshimiwa Chomboh wamelizungumzia na ni jambo muhimu sana tutakwenda kulifanyia kazi. Ni suala la kuongeza uwezo wa rasilimali watu *(human resource capacity*) ya kusimamia mfumo huu katika maeneo haya ya utandawazi na mambo yaliyopo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Zungu alizungumzia suala la *cyber crimes* na akatumia neno "*cybercrime syndicates*." Hivi ni vitu ambavyo sisi tunaviona hapa ni vidogo lakini kwa hiyo

dunia wanaita *developed world* huko kuna watu wa namna hii ambao wana-*penetrate* kwenye mifumo hii na wanatengeneza pesa za ajabu, lakini pia wanasababisha hasara za ajabu.

Wenzetu wamejitengenezea mifumo ya kujihami kwenye *data protections system* za *primary* sites na *secondary sites* na kadhalika na sisi tunakwenda huko na tumeshafika hatua hiyo ambayo mabenki mengi yameagizwa kwa sasa hivi kwamba *primary site* ya kumbukumbu zao ni lazima zote zihifadhiwe Tanzania ili na sisi tuwe tunajua kinachoendelea kwenye kila Benki. Bado kuna Benki kama mbili ambazo zimeomba muda ndani ya miezi mitatu minne nao watakuwa wamefikia kuwa na *sites* zao za msingi hapa nchini Tanzania. *In that way,* Benki Kuu, Wizara ya Fedha, *Financial Intelligence Unit* wote wanahusika katika kudhibiti mienendo ya kazi zinazoendelea humo.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia suala la Makampuni ya Simu. Haya makampuni ya simu ni lazima tukubali kwamba yanatoa huduma ambayo imebadilisha sana maisha ya kila siku ya Mtanzania. Tulikuwa tunagombana hapa miaka mitatu minne iliyopita kwenda kulipia Luku. Luku ikikuishia saa 4.00 usiku ni matatizo. Unakwenda unapanga foleni ya Luku pale, *it is inconveniencing!* Lakini sasa hivi unakaa nyumbani, unaambiwa Luku imebaki nusu *unit* au *unit* moja, unachukua simu yako, unatengeneza mambo, baada ya dakika mbili unajaza Luku yako. Maji, kulipia *Azam TV, DSTV* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye upungufu wa huduma hiyo, ndiyo sheria hii inapoingia. Kwa sababu ni lazima katika ile *human resource capacity building* tuwe tuna uwezo wa kusema kwamba hawa *Vodacom,* hili wanalofanya ni uzembe, hawa *Airtel* hili wanalofanya ni uzembe! M-PESA wamepoteza hela za watu, ni uzembe na kuitofautisha na *force majeure,* kwamba hili limetokea kama ni ajali isiyoepukika.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema katika hili, kwa mfano jambo ambalo wengi wamelizungumza ambalo ni la kweli; unanunua *bundle* la wiki nzima; katika hiyo wiki nzima ya siku saba, siku tatu *network* imeanguka. Lakini wao baada ya siku saba wamekata *bundle* yako, sasa pale umeliwa. Ndiyo tunasema yote haya yanakuja kwenye sheria hii ambayo matarajio yetu pia ni kwamba kwa matumizi ya sheria hii na maeneo yake mbalimbali, pia tutafikia sehemu ya kupanua ubora wa huduma zinazotolewa za *financial services* zinazotolewa kupitia mitandao na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Suzan Lyimo amezungumzia suala la *inconvenience* ya kwenda Benki na unakuta *server* iko *down.* Unahitaji *ATM*, unahitaji kufanya *money transfer* unaambiwa *network* ziko *down*. Katika kukosa huduma ile kwa wakati ule kuna hasara inapatikana, lakini hasara ile inakwenda kwa mlaji haiendi kwa makampuni ya simu. Sasa pale pana *balance* baina ya *fair competition policy* na nini ni haki ya mtumiaji na haki ya mlaji na haki ya mtoa huduma.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme wazi kwamba katika yote hayo yamezingatiwa na ni matarajio kwamba Muswada katika maeneo ya Kanuni za Waziri zitakwenda kufafanua kwa kina masuala haya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo limesemwa katika Muswada huu ni namna ambavyo *electronic transfer* zinavyoathiri hata utendaji mzuri wa *EFD's.* Ni kweli, amelisema Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya na namna ambavyo wafanyabiashara wengi nao wanapata hasara au wanajikuta wako kwenye mazingira ya kupigwa faini na *TRA* na ugomvi na *TRA* kwa sababu ya mifumo hii kutokufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ndiyo hayo tunayosema kwamba Muswada huu unachofanya siyo kuweka taratibu, sheria na kanuni na namna mambo yatakavyokwenda, hapana. Utaratibu na kanuni zilikuwepo. Watu wanasema aah, unajua mambo yalikuwa yanaenda kiholela, hapana. Mambo yalikuwa hayaendi kiholela, isipokuwa sasa yanatengenezewa sheria ili ufanisi wake uwe ni bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kitu kimoja kikubwa ni uwajibikaji, dhamana, *responsibilities*, *obligations,* ndiyo kinachofanywa hapa kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nadhani ni vizuri nikalitambua na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge hasa tulipokuwa kwenye ngazi ya Kamati, ni suala la adhabu. Adhabu ya awali iliyopendekezwa kwa mtu *(a natural person)* ilikuwa inasema isiyozidi Shilingi milioni 10, na kwa *a corporate body,* adhabu ilikuwa ya Shilingi milioni 50.

Sasa tulipofika pale kwenye Kamati, tukapata nafasi ya kukaa na Waheshimiwa Wabunge wenzetu na kuzungumza nao, tukakubaliana kwamba kimsingi *natural person* huyo, kumpa adhabu ya Shilingi milioni 10 wakati anaweza akawa kwa utendaji wake kazi kwa makusudi amesababisha mabilioni ya hasara ni kama kumzawadia, kumpa pensheni kwamba bwana eh, lipa hiyo Shilingi milioni 10 ondoka. Lakini *natural person* ilikuwa ina Shilingi milioni 10 na adhabu ya kifungo. *Corporate body,* haya makampuni makubwa ambayo yenyewe ndiyo yana dhamana kubwa katika mambo haya, adhabu ya kima cha chini ilikuwa Shilingi milioni 50. Tukasema kwenye *body corporate* kuwa na adhabu ya Shilingi milioni 50 ni ndogo mno.

Mheshimiwa Spika, kwa makubaliano ya pamoja, tukafika sehemu tukasema kwenye adhabu ya mtu binafsi, amefanya kosa la wazi kabisa la maksudi, umempa adhabu ya Shilingi milioni 10, tukasema hapana, Serikali ikaridhia, tumesema tuipeleke kwenye Shilingi milioni 100 kwa adhabu ya mtu *(natural person)*. *Body corporate* imetoka Shilingi milioni 50, imependekezwa na Kamati na tulikaa pale kwa pamoja tukaridhia tukasema iende kwenye Shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, adhabu zinaonekana kubwa, lakini pia kiasi cha kiwango cha fedha kinachopita humu kwenye mitandao hii kwa kila siku, ukiwachukulia Watanzania milioni 30 ambao *in one way or another* kuna *sim card* milioni 30 zinafanya kazi, ni hela ndogo sana. Lakini tunasema kwa sababu sheria hii tunaipeleka kwa wananchi, iende ikafanye kazi halafu itapata muda wa kuja kufanyiwa marekebisho kama tunaona hizi adhabu ni ndogo zinaweza zikaja zikafanyiwa marekebisho katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la utatuzi wa migogoro baina ya mtoa huduma na mteja, hili limezungumziwa katika Ibara ya 51 na kulikuwa na wasiwasi kwamba ikiwa suala lenyewe ni la Benki Kuu tu na mtoa huduma au na mteja, wigo ule wa kuweza kupata utetezi unaweza ukawa ni mdogo. Hilo limefanyiwa kazi kwa kina na sheria imeweka bayana kwamba hilo limekuwa *covered* vizuri tu.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 52 pia inazungumzia namna ambavyo mfumo huu wa malipo unajikinga dhidi ya majanga mbalimbali yanayoweza kutokea. Sheria hii inapendekeza kwamba hawa watoa huduma wahakikishe kwamba huduma inapatikana wakati wote. Hapo ndiyo nikasema ni suala la wajibu na dhamana *(obligations and responsibilities)* za kila mmoja ambazo hazikuwemo katika utaratibu wa awali na sasa unamwambia mtoa huduma kama utatoa huduma hii, basi uhakikishe inapatikana masaa 24.

Mheshimiwa Spika, wizi wa kimtandao katika mifumo ya malipo. Hiki ndiyo kile kipengele ambacho tumesema kwamba usimamizi, inabidi saa zote 24 wale wasimamizi nao wanakuwa

wanaenda sambamba, maana mnapokwenda ninyi na duniani watu wanakwenda wanabadilika. Tuna watu wanaitwa *hackers* wao kazi yao, mbinu yao, fani yao ni kuingia katika mifumo kwa kutumia njia za kompyuta na *internet*. Anaweza kuchukua mfumo mzima wa usalama wa Marekani. Sasa anaufanyia nini? Anaweza kuuza. Akiuuza kwa matarajio ya kupata fedha na kadhalika, hapo anaingia kwenye makosa ya upande wetu. Anapokuwa anafanya *hacking* kwa masuala ya usalama na nini, anaingia kwenye Sheria ile ya *cyber crimes* ambazo anatakuja kuziwasilisha Mheshimiwa Profesa Mnyaa wiki ijayo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la ulinzi wa mlaji katika mifumo ya malipo nchini. Nilitaka tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba vifungu vingi katika sheria hii vimezungumzia masuala ya *compliance* na *deterrence,* lakini siyo kwa vile vifungu vinne tu ambavyo vimemzungumzia mlaji.

Kwa upana wa tafsiri ya vifungu vingine, mlaji huyu amezungumziwa katika maeneo mengi sana na lengo hasa ni kuhakikisha siyo tu kwamba anatajwa lakini lengo ni kuboresha huduma hii kwa huyu mlaji ili kile kiwango cha kupata huduma hiyo kiongezeke.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo Ibara tu zile za 47, 48, 52, na 53, lakini yapo maeneo mengine mengi ambayo mlaji anazungumziwa.

Sheria inayopendekezwa inasomwa pamoja na sheria nyingine, kama nilivyosema inasomwa pamoja na *Fair Competition Act*, Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* na sheria nyingine kama Sheria ya Mawasiliano na Elektroniki na Posta, *(EPOCA)* 2010 na sheria nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunapoisoma sheria hii ukitaka kuipatia tafsiri nzuri inapaswa uiangalie kwa upana wake pamoja na sheria nyingine ambazo zinahusika nazo.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la mapato ya Serikali, Mheshimiwa Christowaja, Mheshimiwa Mohammed Chomboh, Mheshimiwa Martha Mlata Mheshimiwa Zungu pia amelisema; na Waheshimiwa wengi, wamelizungumzia hili suala na namna ambavyo mifumo hii ikitumika vizuri kwenye masuala ya *networking*, *TRA* na kadhalika. Lakini kuna *element* nyingine ambayo hatujaiona kwamba mfumo huu utatumika na *NIDA,* vitambulisho vya Taifa ambavyo navyo vina *biometric identity*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, matarajio ni kwamba kwa upana wa sheria hii inavyotumika na malengo yake itaboresha sana huduma za kifedha zinazopatikana kwa wananchi lakini kwa kiasi kikubwa matarajio ni kubadilisha maisha ya Mtanzania na kuyafanya bora zaidi na kuongeza kiwango cha maisha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, hiyo kengele ya kwanza au ya pili?

**SPIKA:** Ni ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtoa hoja!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi ninashukuru kupata nafasi hii ili kuweza kutoa maelezo, majibu pamoja na taarifa mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, tunawashukuru sana kwa *comment* zao lakini tunawashukuru sana kwa pamoja sote tumeweza kukubaliana kutokana na umuhimu wa Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, mengi ambayo yaliulizwa ama yalitaka kutolewa ufafanuzi, yametolewa ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri Makame Mbarawa lakini vilevile na Mheshimiwa Naibu Waziri. Mimi nitakwenda katika masuala yale ya kisera zaidi ili kuyatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala zima la kulinda mifumo ya malipo dhidi ya majanga mbalimbali, ambapo limeelezewa kwa kina na Mheshimiwa Zungu. Ushauri huu ni muhimu sana na tumeupokea. Kuna umuhimu mkubwa sasa wa kulinda mifumo ya malipo dhidi ya majanga mbalimbali.

Katika Ibara ya 52 ya sheria yetu inaeleza kwamba sharti moja la kupewa leseni ni lazima wale wanaotoa huduma kwanza wahakikishe huduma inapatikana wakati wote. Vilevile ibara hii tutakwenda kuihuisha na Kanuni ambazo tutabainisha mle kwamba taratibu za kuendesha biashara, yaani *business continuity* na mikakati ya kuzuia majanga *(Disaster Recovery Plan)*. Wakati watoa huduma wakapokuja ku-*apply* ili wapewe leseni, hivi vitu lazima viwepo. La muhimu, kubwa zaidi, ni lazima kuwe kuna hiyo *Disaster Recovery Plan.*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, hawa watu kwa mfano kama sasa hivi wanavyofanyakazi zao, *requirement* moja ni lazima wawe na *primary servers.* Tunachokitaka wao wenyewe wanajua na ndicho ambacho wana *implement,* ni kwamba zile *primary servers* ni lazima ziwepo hapa Tanzania. Kwanza, kwa zile Benki za Tanzania lakini hata zile Benki ambazo ziko nje, lazima kama wana-*operate within* Tanzania wawe vilevile na hizi *server* zao hapa ndani.

Kwa hiyo, hii ipo lakini kwa sababu hii mifumo imeimarika zaidi, imekwenda mbele kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, tutahakikisha kwamba hata zile kanuni zetu tunaziimarisha ili kuona kwamba hata *plan* yao wenyewe mbali ya kuwa na hizo *servers* lakini ni lazima wawe na ile *plan* kwa ajili ya kufanya hiyo *disaster recovery*.

Mheshimwia Spika, vilevile kulikuwa kuna suala ambalo limesemwa kwa wingi kuhusu wizi wa kimtandao katika mifumo ya malipo. Sisi tumebainisha, lakini vilevile sheria hizi za *cyber crime* pamoja na *electronic transactions,* zitakuja kubainisha zaidi kuhusiana na suala zima hili la jinsi ya kujikinga na wizi huu wa kimtandao. Lakini mengine mengi tayari yameshaelezewa na Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, eneo hili la kumlinda mlaji limeshaelezewa. Kuna maeneo mengi ambayo yanaelezea kuhusiana na mlaji anavyolindwa, na hii siyo sheria pekee ambayo inakwenda kumlinda mlaji. Sheria hizo zitakazokuja zote vilevile zinakwenda, zitaelezea kwa namna moja ama nyingine kuhusiana na kumlinda mlaji katika suala zima la matumizi haya ya hii mitandao.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu tu ya hili suala zima la kumlinda mlaji, hii sheria haisimami peke yake katika eneo hili. Sisi tuko tu katika lile eneo la fedha *(finances)* lakini vilevile Sheria ya *Fair Competition Act*, 2013; Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano (*TCRA Act),* 2003, vilevile Sheria ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta *(EPOCAR)* ya mwaka 2010 zote pamoja na kanuni zake zinaelezea kwa kina jinsi gani mlaji analindwa mle. Kwa hiyo, hii siyo sheria peke yake, hii sheria tumeangazia zaidi katika yale maeneo ya *transaction*.

Mheshimiwa Spika, kuna suala moja ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Peter Msolla, tunamshukuru sana kwa *concern* aliyoitoa, ambayo alikuwa akisema kwamba fedha huwa zinachelewa sana kutoka Hazina kwenda *BoT* na Halmashauri. Alizungumzia sana kuona huu utaratibu ambao unawekwa, vipi unakwenda ku-*address concern* hii ambayo yeye ameitolea.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchelewa kwa fedha kutoka Hazina kwenda BoT na kupelekwa kwenye Halmashauri, hizo fedha tayari unakuwa unaziona kwenye mtandao lakini hakuna *hard cash.* Ni suala ambalo siyo tu kwa sababu ya sheria hii, lakini ni suala mbalo tayari limekuwa likizungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge na Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya katika Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, kweli, utaratibu huu ni lazima tuufuate, yaani ni lazima Hazina ipeleke pesa *BoT*. *BoT* pale, ndipo kuna akaunti ile ya Serikali. Sasa tunasema kwamba, hii akaunti ya Serikali inavyo-*operate,* ni kama akaunti ambayo mtu binafsi anayo.

*Sometimes* kwa sababu ya *operation,* inakuwa ile *limit* ya kutumia inakuwa imekwisha, kwa hiyo, ni lazima tusubiri fedha ziingie ndipo matumizi yapelekwe. Lakini hata kama ile *limit* ya matumizi kwa siku itakuwa imefikia kikomo chake, haituzuwii sisi kama Serikali kutokufanya *procedures* nyingine kwa ajili ya matumizi. Kwa hiyo, fedha ukiziona kwenye mtandao, basi ujue hiyo ni hatua muhimu sana kwa ajili ya kufanya malipo. Wewe chukulia kwamba hiyo fedha tayari iko njiani na itafika wakati wowote.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu tu Serikali yetu inavyo-*operate* ama bajeti yetu tunavyoitekeleza, tunaitekeleza kutokana na utaratibu huu wa kukusanya mapato na kisha kwenda kule kutumia. Kwa hiyo, hili siyo tatizo la mtandao *as such,* lakini ni tatizo la *operation* nzima za bajeti yetu na *Government procedure* katika matumizi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala lingine kuona kwamba, Sheria hii iboreshwe ili kuona kuna *transaction* zinalipiwa kodi. Ni kweli, lakini kwa mantiki ya Sheria hii ni Sheria ambayo inatazama utaratibu mzima wa ile miamala inayofanyika. Lakini hili tumeendelea kuliboresha kama Serikali na kama tulivyokuwa tumesikia tokea mwaka juzi tumeanza ku-*operate* huu mfumo wa *TTMS* sisi na wenzetu wa mawasiliano kupitia *TCRA,* lakini vilevile ambapo tunaona sasa zile *international calls* zinazoingia, sasa pale *exactly* tunajua *calls* zilizoingia na *revenue* ya Serikali ni kiasi gani. *System* ya mfumo huu imeanza tayari kuleta matunda, kuna fedha ambazo zimekuwa zinaingia tokea tumeanza kuufunga.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu kwamba mwaka huu wa fedha tunaoendelea nao tumepitisha Sheria katika *Finance Bill,* kipengele cha kutoza *0.15%* kama *Excise Duty* kwa ajili ya *electronic transactions.* Hii Benki Kuu ina-*manage,* yaani inaweza kuziona zile *transactions* na kwa hiyo, *automatically* zile *0.15% Excise Duty* zinaweza zikapatikana. Kwa hiyo, bado katika mifumo mingine tunaweza kuboresha kuona ni jinsi gani Serikali inaweza kupata mapato yake hapo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo lilikuwa limezungumziwa ni kuhusiana na wizi kupitia matumizi ya nyimbo na michezo ya kubahatisha. Hili limeelezewa, ambalo tutakwenda kulisisitiza kwa sababu Serikali ni moja.

Huu Muswada wetu umezungumzia masuala zaidi ya ile mifumo ya kifedha, lakini kwa sababu wizi kupitia matumizi ya nyimbo na michezo ya kubahatisha mbalimbali ni masuala ambayo yanamgusa mwananchi moja kwa moja. Sisi Serikali tutalichukua, tutalisimamia pamoja na wenzetu wa *COSOTA* tuone kwamba hapa mwananchi hawezi kuibiwa.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kumlazimisha mtu aingie katika bahati nasibu, kwa sababu, bahati nasibu ni *optional.* Kwa hivyo, ni kweli kuna watu wengine hawapendi, ama tu misingi ya kidini, ya kiimani haituruhusu kuingia katika hii michezo ya kubahatisha, makampuni haya yaone haki ya mteja katika kukubali na kutokubaliana na huduma anazozitoa. Kwa hiyo, lenyewe tutalichukua, tutakwenda kulisimiamia kuona kwamba haki ya huyu mteja inalindwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine Mheshimiwa Chomboh alilizungumza vizuri, kuhusu Maafisa wetu ambao watakwenda kutekeleza hii Sheria kwamba wajengewe uwezo. Ni suala la msingi sana na tunalichukua. Sasa hivi tayari katika ile Idara yetu ya Mifumo ya Kifedha pale *BoT* tuna vijana weledi kweli ambao wana uwezo mkubwa.

Mheshimiwa Spika, jana wakati tulipokuwa tunafanya Semina, nadhani Waheshimiwa Wabunge wengi wamemwona kijana wetu alivyokuwa akitoa semina na kitu ambacho alikiteremsha ni kitu ambacho kinafahamika kabisa, ndio maana leo tuko hapa kwamba, sisi sote tumepata ufahamu mzuri wa Sheria hii. Alitupa semina nzuri, tumefahamu, lakini pia ni changamoto kuweza kutengeneza vijana wengine kama wale ili kusimamia Sheria hii muhimu sana kwa maslahi ya uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, kuna lingine ambalo Mheshimiwa Chomboh alilisitiza hususan la *credit card. Well,* hili ni jambo la kibiashara zaidi. Wengi sasa hivi wanatumia *debit card,* lakini nadhani kuna Benki moja au mbili tayari zina mifumo hii ya *credit card.* Suala hili ndilo ambalo wenzetu wa nchi zilizoendelea walilitilia mkazo. Kubeba pesa ukawa unasafiri nazo ni kitu ambacho ni *so 1990s,* tunaweza tukasema! Sasa hivi kuna namna mbalimbali. Wakati unabeba pesa tayari wewe mwenyewe unakuwa katika *risk zone* kwamba, uko *risking.*

Mheshimiwa Spika, tumeona, tumeshuhudia matokeo mbalimbali ya ujambazi! Mtu tu ameonekana ametoka pale, amekwenda kuchukua pesa *Bank* kwenye *hard cash,* amebeba, watu wamemfuata. Kuna tukio limetokea juzi juzi siyo zuri sana, watu wengi wameibiwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto kama hizo, ndiyo tunapopata sasa umuhimu wa kuweza kutumia hizi kadi. Hizi kadi tuwe tunazitumia na tuzishajihishe. Yaani hii sasa tuone kwamba ni changamoto ya kuweza kuwashajihisha wananchi waweze kutumia kadi zinazotolewa.

Mheshimiwa Spika, zenyewe zina changamoto zake, lakini tunaona kwamba, ile *risk* inapungua zaidi mtu ukiwa unatumia kadi kuliko kuwa unatembea na *cash.* Lakini wengine *it is just an attitude* kuona kwamba mkoba wake uwe umetunatuna, anachukua hela anapeleka, lakini siyo tabia nzuri hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana sasa kutokana na msingi huu, kwa mfano, kuna wafanyabiashara wengi sasa hivi wanakwenda China, wanarudi; ku-*facilitate* tu ile *trade,* tayari kuna Benki ya Kichina iko hapa, lakini vilevile *CRDB* imefungua tawi lake kule *Beijing* na tutashajihisha zaidi *CRDB* na Benki nyingine kutumia fursa hii ya wafanyabiashara wa Tanzania ili waweze kufungua matawi yao katika nchi mbalimbali kuweza ku-*facilitate trade.* Hii vilevile itajenga uchumi, lakini vilevile itapunguza ile *riskness* ya watu ambao wanabeba pesa mikononi.

Mheshimiwa Spika, adhabu inayotolewa, tumeambiwa ni ndogo mno. Hili tumeliona na katika ngazi ya Kamati tumelirekebisha. Lakini napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, suala la Kanuni limetiliwa mkazo. Kwa upande wetu natoa taarifa kwamba, hizi Kanuni ziko tayari, tulishaziandaa, ziko Hazina, tunasubiri marekebisho madogo madogo

ama mengine ya kimsingi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge ili twende tukaboreshe Kanuni. Kwa hiyo, kati ya mwezi mmoja na miezi miwili tunahakikisha kwamba hizi Sheria zinatoka. Kwa hiyo, suala la hizi Sheria na Kanuni zake zinatoka. Kwa hiyo, hilo halina mjadala, tutalifanya na Kanuni zitatoka kama vile ambavyo tumesema.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa gharama, limeelezwa, nadhani hili ni suala la msingi, lakini halielezwi katika sheria hii na hivyo basi, Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano amelichukua na bila shaka katika Miswada ya Sheria miwili itakayokuja atalielezea kwa kina suala hili.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya alitoa *concern* kuhusiana na matumizi ya *EFD* ambapo alisema zinaharibika mara kwa mara. Nadhani mashine zetu za *EFD* kama tulivyokuwa tumezungumza tokea tunawasilisha bajeti yetu ya mwaka 2014/2015 tumesema sasa mfumo huu utakuwa umeboreshwa zaidi. Mashine zetu za *EFD* sasa hivi zimeboreka. Suala la kuwa zinaharibika mara kwa mara, halipo! Zinaharibika, lakini siyo mara kwa mara kwa sababu kile ni kitu tu.

Mheshimiwa Spika, hili limekuwa ni sababu kubwa sana ya hao ambao tunawataka watumie hizi mashine, wamekuwa wakilalamika kwamba hizi mashine zinaharibika mara kwa mara! Kwa sasa hivi halipo kwa sababu mashine zetu, hizi *versions* ambazo tumetoa sasa hivi ni *versions* ambazo ziko *more modern* na zinaweza zikahimili mazingira yoyote. Kwa hiyo, hiki siyo kikwazo. Lakini naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya kwamba, kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania, tutaendelea kulisimamia hili, tutaendelea kutoa huduma kwa wale ambao wanatumia, tutawasimamia wale *suppliers* wahakikishe kwamba zile huduma kama ilivyo katika Mkataba wetu tuliosaini nao; zile huduma za kuhakikisha kwamba mashine kama zinaharibika, tatizo linatatuliwa mara moja, hili tutaendelea kulisimamia na hawa *Suppliers.*

Mheshimiwa Spika, lakini kama ilivyo Sheria, Sheria inasimama pale pale, mashine za *EFD* hazijafutwa na zinatumika kama kawaida. Tutalifuatilia kwa wale ambao hawatumii mashine hizi, hatua za Kisheria tutachukua; suala la kuharibika tutali-*cover,* lakini isiwe sababu ya mtu kutokutumia mashine.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Agripina alieleza kuhusiana na muda huu wa kukamilisha leseni, katika sheria tumesema ni *30 days,* kweli, lakini tumesema *within 30 days.* Yaani katika siku 30, hata yeye mwenyewe Gavana awe tayari ameshatoa leseni! Yaani hiyo, haimpi yeye *option* kwamba anakaa tu anasubiri siku 30.

Kwenye Sheria tumesema *within 30 days Govenor* awe ametoa hizo leseni. Kwa sababu, tayari ile misingi ipo, hakuna sababu ya kukaa muda wote siku 30 kwamba ndiyo leseni inatolewa. Isipokuwa lazima kama ilivyo kwa Sheria, twende tukafanye *due diligence* kwa haya makampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, na hiyo ina-*require* vilevile kwenda. Wakati nyingine tunakwenda *site visit,* lakini *all in all with our capacity BoT within 14 days* kama kila kitu kitakuwa kimekamilika upande wa wale wanao-*apply* na upande wetu sisi na kwamba *facilitation* ile ya kwenda *site* na kwenda kufanya *inspection* imekamilika, basi *within 40 days* leseni inaweza kutolewa. Tumejipa ile *leeway* ya *30 days,* lakini ni *leeway* ambayo itakuwa inayotekelezeka. Haimpi *option* ya kuwa Gavana akae *and then after 30 days* ndiyo atoe hiyo leseni. Hakuna sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lingine Mheshimiwa Agripina alisisitiza kuhusiana na Kanuni, tunalichukua. Kama nilivyoelezea ni kwamba, hizi Kanuni kimsingi ziko tayari. Tutafanya marekebisho ya hapa na pale ili sasa tuwe tunazitoa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Nundu amelielezea suala zuri sana kuhusiana na *Safaricom* na *Vodacom* zimeathirika vipi? *More or less* hii *Vodacom* na *Safaricom* ni moja, kwa hivyo, labda tutakupa tu taarifa kutokana na *transaction* hiyo iliyopotea kwamba *Vodacom* kwa upande wake imeathirika vipi. Lakini kuhusiana na Watendaji ambao wamehusika na kadhia hii ya upotevu wa hizi karibu Shilingi bilioni 300, kipengele chetu kwenye sheria kinasema kabisa kwamba mtu yeyote ambaye atakuwepo katika *management* na ambaye amefanya makosa katika *previous payment system,* huyo mtu hatutamruhusu aingie katika *system* nyingine kabisa.

Kwa hiyo, hili tutalisisitiza, na kwa sababu hii taarifa tayari tunayo, tuhakikishe kwamba wale wote ambao walihusika na kadhia ya miamala hii, basi hawaingii katika *management level* ya hizi *payment system* za kwetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir alielezea kuhusiana na malipo kupitia *cheque* kwamba yanachelewa sana na hii ni *concern* ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kumekuwa kuna ucheleweshaji wa pale *electronic clearing house* kwamba, inaweza ikachukua hadi wiki kweli mtu hajapata pesa zake. Lakini ni suala la kwenda tu kulisimamia zaidi na sasa hivi karibu tunatoka katika huu mfumo wa *electronic clearing house* na kwenda katika mfumo bora zaidi ambapo itasababisha sasa *one, two or three days* tayari mtu amekwenda ku-*clear cheque* awe amepata fedha zake. Hili litakuwa ni jambo zuri kwa sababu, watu wengi wametapeliwa ama wamekosa pesa zao kutokana na malipo haya ya *cheque*. Lakini sisi tutaendelea kudumisha hizi *system* zetu, kuimarisha ili kuona kwamba, hawa watu nao hii *payment system* nayo inakuwa nzuri na inakuwa *relevant in terms of timing* kwa ajili ya kui-*clear.*

Kulikuwa kuna hoja nyingine ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani iliisisitiza, ni suala la msingi kuhusiana na mapitio ya malalamiko kuwasilishwa kwa Gavana badala ya Benki Kuu. Maoni yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani yako *valid* na kwamba, kwa sababu tu uamuzi wa Gavana ndio uamuzi wa Benki Kuu na kwa sababu yeye ndiye Mtendaji Mkuu. Ndiyo maana sasa pale ilikuwa siyo rufaa. Pale ni *reviews,* tunaangalia yale mapitio; mtu hajapewa leseni, lakini anapeleka maelezo yake ya kwa nini hajapewa leseni.

Kwa hiyo, Gavana atahusika na kufanya *review rather than* ku-*appeal.* Masuala ya *appeal* yako kwenye vyombo vya kisheria zaidi na sio Gavana. Lakini tukisema kwamba, Gavana maana yake ndio Benki Kuu. Kwa hiyo, iko *valid* kutokana na muono, lakini haya ni malalamiko tu ambayo ni ya mapitio *rather than* zile *appeals,* yaani siyo rufaa yenyewe.

Kulizungumzwa kuhusiana na kutangazwa *again* Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kuwa sheria ndogo ndogo na masharti, tunakubaliana na pendekezo mlilotoa, ndiyo maana tumeleta *Schedule of Amendments* kuangalia kwamba, hizo sheria pamoja na masharti na yenyewe yanakuwa *Gazetted.* Isipokuwa zile *administrative* ndizo ambazo tutakuwa tunazitoa kwa kutumia tu njia nyingine, lakini zile Sheria, Marekebisho ya Sheria Ndogo ndogo pamoja na masharti yatakuwa *Gazetted.* Tumeleta *Schedule of Amendment* na hili ni jambo la msingi na ni jambo la maana sana.

Mheshimiwa Spika, eneo kubwa lingine ambalo lilizungumziwa ni kuhusiana na wizi wa mitandao ambalo limeelezwa kwa kina zaidi kwenye vifungu vyetu, lakini vilevile Sheria ambazo zinakuja na zenyewe zitakuwa zimeelezewa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine, Mheshimiwa Mnyika alielezea kuhusiana na fedha zilizotolewa kutoka *Stanbic.*

Suala hili lilijadiliwa kwa kina wakati wa maazimio yale ya Bunge kuhusiana na hili sakata la *Escrow.* Labda kupitia Bunge lako Tukufu, tunataka kutoa taarifa kwamba, uchunguzi bado unaendelea kwa vyombo vinavyohusika na kwa sababu siyo uchunguzi wa leo na kesho.

Lakini ni uchunguzi ambao unahusisha mifumo, Benki za nje, vilevile unahusisha makampuni na *individuals* na kwamba vyombo vinavyohusika vinaendelea na uchunguzi, ninaamini kwamba kwa sababu ni *issue* ambayo iligusa *attention* ya wananchi, basi taarifa itakapokamilika itatolewa.

Mheshimiwa Spika, mengi mengine tayari yamezungumzwa na nadhani tumejitahidi kwa njia moja ama nyingine kutoa maelezo na ufafanuzi, sasa basi naomba Waheshimiwa naomba kutoa hoja kwamba Muswada huu ukubaliwe.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Tunaingia hatua inayofuata, Katibu!

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 4

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 8

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwangungu! Nadhani wote mmegawia marekebisho mbalimbali ee?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye ibara hiyo nimependekeza tuongeze kipengele ambacho kitaondoa hali ya makampuni kulalamikiwa kwa maana kwamba, pale kampuni ambapo itakuwa imelalamikiwa kwamba inatoa huduma zisizokidhi, basi itakuwepo fursa kwa Benki Kuu kukubali na kumnyima leseni au hatakubaliwa tena kuendelea na biashara hiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unabadilisha nini wewe?

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongeza kutoka vipengele vilivyokuwepo, kipengele cha 8(2)(b) na nimeongeza kipengele kipya cha 8(2)(c)

**MWENYEKITI:** Naomba usome ulichoongeza kwa sababu ni rekodi hizi.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) kwa maana kwamba itasomeka hivi;

"*on the receipt of an application under section one the bank may renew the license upon satisfaction that no justifiable and genuine complain has been lodged to the bank by consumers regarding service offered by the holder of the license*".

**MWENYEKITI:** Na ueleze sasa hii sasa inatusaidia nini sisi au inasaidia nini sheria hii.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hii itasaidia kwamba kama kutakuwa na makampuni ambayo yanalalamikiwa au wenye leseni wanaolalamikiwa, hawatakuwa na fursa ya kupewa tena kibali cha leseni mpya mpaka pale watakapokuwa wame-*comply* na hizo *complaints* ambazo zimekuwa *filed*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria au Waziri sijui! Waziri!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimemuelewa vizuri Mheshimiwa Mangungu, anasema kwamba, ikiwa tu yaani hakuna *complain* kutoka kwa watumiaji kwamba hiyo leseni itakuwa *granted*. Lakini kwa sababu sheria hii utekelezaji wake unakwenda kusimamiwa na Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kipengele cha 8(3), Benki Kuu inapoona, inawezekana hata hayo malalamiko yenyewe pia Benki Kuu wameyapata, kwa hiyo inapoona, hatuwezi ku-*renew* leseni kama itakuwa *satisfied* kwamba, huyo mtu ame-*fail* tu-*comply*. *Including the conditions* ambazo zilikuwemo katika leseni iliyopita, basi hatum-*grant*. *Otherwise* kama itaonekana kwamba huyo mtu ame-*comply* na hizo *conditions* ambazo zilikuwepo, basi kutakuwa hakuna haja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naona hiki cha 8(3) kinatosheleza pamoja na hilo ambalo amezungumza Mheshimiwa Mangungu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nitakubaliana na Mheshimiwa Waziri kwamba itabakia hivyo hivyo kama atanihakikishia kwenye *conditions* ambazo zimekuwa kwa kipengele cha (3) kinavyosema kwamba;

"*…the bank may refuse to renew a license if it is satisfied that applicant has failed to comply with conditions*".

Sasa hizi *conditions* ukiniambia *one of the conditions* kwamba hatakuwa na *complaints,* hapo tunakubaliana. Lakini kama ikiwa hizo *conditions* siyo moja kati ya hili nililolisema kwamba kukiwa na *complaints, then* itabidi kipengele hiki kibakie na nitabakia na msimamo wa *amendment* niliyoi-*move*.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anavyozungumza ni sahihi katika *context* yake. Lakini tumuachie Gavana aweze sasa kuangalia hizo *complaints* ziko *justifiable* kiasi gani. Haitakuwa vyema kwamba amekuja mtu, wamesema wawili, watatu, wane, halafu yeye hajapata fursa ya kuweza kufanya *analysis* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mangungu kwamba, katika kanuni zetu tutaliangalia suala hilo kwa mapana yake.

**MWENYEKITI:** Hapana! Ile *section* ya 8(2)(b) inasema hayo, inasema hivyo hivyo isipokuwa kwa maneno mengine, inasema hivyo hivyo!

*(Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 9

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeleta marekebisho katika kifungu cha 9(3) kwa msingi kwamba kifungu hicho cha 9 kwa ujumla wake kina maudhui ya kusimamishwa kwa leseni ya mfumo wa malipo; na hicho kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kwamba pale ambapo mwenye leseni ameshindwa kutoa sababu za kuridhisha, benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni hiyo au kutoa amri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naleta marekebisho kuondoa maneno "au kutoa amri nyingine kwa namna itakavyoona inafaa" na ibaki maneno yafuatayo kwamba pale ambapo mwenye leseni ameshindwa kutoa sababu za kuridhisha, "benki inaweza kusimamisha kwa muda leseni yake".

Mheshimiwa Mwenyekiti, naondoa haya maneno kwa msingi ule kwamba maudhui katika kifungu hiki ni kwamba pale ambapo mtoa huduma atakuwa hajakidhi vigezo na anapoenda ku-*renew* leseni yake na ikaonekana kwamba kuna upungufu ama nini, basi leseni yake inaweza kusimamishwa muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake unatoa mwanya wa kusimamisha leseni tu kwa muda na kuondoa haya maneno ambayo yanatoa mwanya mwingine kwamba kutakuwa kuna amri nyingine kwa namna itakavyoonekana inafaa. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni kutoa hayo maneno na kubaki kama ambavyo nimesoma hapo awali.

**MWENYEKITI:** Kwa sababu Muswada upo kwa Kiingereza, tunaomba utumie hicho Kiingereza kilichopo hapo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kiingereza ni kuondoa maneno "…*or make any other order as it may deemed appropriate*" na kwamba sasa kifungu kisomeke "…*where the license fails to show cause to the satisfaction of the bank, the bank may suspend the license*". Iishie hapo na kuondoa yale maneno yanayofuata.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tukiwa tunalielezea hivi nadhani hili neno linakuwa zuri, lakini hapa tuna *deal* na mifumo ya malipo ambayo tayari ni *operational,* lakini ni mifumo ambayo tayari inatoa huduma kwa watu katika siku zote.

Kwa hiyo, mantiki yetu kama Wizara kuweka kifungu hiki ni kuipa nafasi Benki Kuu kuweza ku-*determine other ways rather than* ku-*suspend* ile leseni ili kuhakikisha kwamba ile huduma kiuchumi kwanza inaendelea, siyo tu ku-*suspend,* lakini tukiona kuna haja ya kuwa huyu mtu usimpe *suspension* lakini umuangalie katika muono mwingine kwa ajili ya kuweza ku-*comply,* basi vile vile benki iweze kutoa hizo ili tusikatishe ule mzunguko mzima wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali ambapo Benki Kuu inaona kwamba hapa kabisa hii leseni itabidi iwe *suspended,* basi itakuwa *suspended.* Kwa hiyo, tunataka tuipe nafasi Benki Kuu kuweza kutekeleza hayo.

**MWENYEKITI:** Mimi sijaridhika na *justification* kwa nini yatoke hayo maneno!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi ambao Waziri ameeleza hapo nakubaliana kwamba ibaki kama ilivyo.

*(Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 10

*(Ibara Iliyotajwa Hapo Juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara Zilizotajwa Hapo Juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 14

**MWENYEKITI:** *Okay* tumeishasema.

**MHE. CHRISTINA M. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kifungu cha 14 kinatamka adhabu ambayo mtu atapewa ikiwa atavunja masharti ya kifungu hiki. Sasa adhabu ambayo inaletwa katika marekebisho ya Mheshimiwa Waziri, ni kwamba ana-*substitute a fine not exceeding ten million* ambayo na yenyewe tuliihoji, sasa inaletwa *a fine not less than fifty million.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hoja yangu ni kwamba Muswada au kifungu hiki hakijaeleza bayana mlengwa wa kifungu hiki ni nani, kwa sababu watoa huduma wa mifumo ya malipo kuna makampuni na kuna vikampuni na watoa huduma wadogo wadogo kama kwenye huduma hizi za kutoa pesa hizi.

Sasa, ingefaa kama marekebisho haya yangefanunua ni nani ambaye atatoa *fine* ya *not less than fifty million.* Je, ni kampuni au ni wafanyabiashara wadogo wadogo hawa wa huduma za malipo ya pesa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ufafanuzi!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 14 inazungumzia makosa yanayofanywa katika sehemu hii ya tatu ambayo inaanza Ibara ya 5 mpaka Ibara ya 15. Sasa makosa yote yanayofanywa katika kipande kile ndiyo yanasema hivi; "*a person who contravenes any provision of this part…* (katika sehemu hii ya tatu) *commits an offence and is liable on conviction…*" kwa haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yule mtu ni binadamu *(natural person)*, ndiyo tunasema hivi, mwanzoni tulivyokaa kwenye Kamati tukakubaliana kwamba, kama ni binadamu kumtoza unasema *not exceeding* milioni 10 ni adhabu ndogo sana kwa madhambi yanayokuwepo katika sehemu hii yote ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa makosa yenyewe unayachukua tangu Ibara ya 5 mpaka Ibara ya 13, makosa yote yaliyotajwa hapo awali. Tukasema basi katika hatua hii kima cha chini

cha faini kiwe ni milioni 50 kwa binadamu *(natural person)*. Lakini, inapohusu kampuni *(board corporate)* tukasema hivi, adhabu ile ambayo ilikuwa sasa kwa kampuni ambayo imesajiliwa kama *board corporate* ya kumuambia milioni 50 ni ndogo na ile ilikuwa *not exceeding 50 million*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa adhabu inayoenda sasa kwenye kampuni ni *not less than 500 million.* Adhabu haipungui *500 million.* Kwa hiyo binadamu haipungui 50, kwa kampuni haipungui milioni 500.

**MWENYEKITI:** Sasa, siyo kwa binadamu, kwa mtu mmoja mmoja.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtu mmoja mmoja.

**MWENYEKITI:** Lakini, wengine mlishahoji hata Mheshimiwa Mughwai nimempa nafasi kwa sababu tu, lakini hakuna ubishi katika hili. Ehe, Mheshimiwa Chambiri!

**MHE. KISYERI W. CHAMBIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya makosa tunayofanya ya kifedha kwamba tunasema faini au kifungo, yanafanya watu wasi-*comply* inavyotakiwa. Kusudi *compliance* iwe nzuri na watu wasidhulumiwe, hii sheria ingesoma kabisa kwamba atafungwa pamoja na kulipa faini, halafu watu wataogopa na kazi itafanywa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nashauri, hayo ni mawazo yangu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ukiisoma Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaeleza kwamba, Mahakama ndicho chombo cha juu kabisa cha mamlaka ya utoaji haki katika Jamhuri. *Trend* sasa ya *penal systems* duniani ni kwamba, Mahakama iachiwe fursa ya kuamua.

Kwa hiyo, tunachokifanya hapa sisi, tunatambua ukubwa na tatizo hili. Kwanza hawa watu juzi tu hata na mimi wameniingiza mjini, lakini bado tuache hii *option*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri Wabunge wenzangu kwamba, hivi ambavyo tumeileta sasa kwenye mapendekezo sisi Serikali ibaki jinsi ilivyo.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 18

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kifungu cha 18 hakitofautiani na kile kifungu cha awali na kwa msingi ambao Mheshimiwa Waziri ameusema, basi inabaki kama ilivyo.

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara ya Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 20

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba nikubaliane na marekebisho ya Serikali kwa maana kwamba yenyewe yamekaa vizuri, kwa maana *figure* ambayo wao wameanzia iko kwenye *higher side* kuliko ile ambayo mimi niliipendekeza. Mimi nilipendekeza milioni 10 wao wamependekeza milioni 50, kwa hiyo nakubaliana nao.

*(Ibara ya Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28

*(Ibara Zilizotajwa hapo juu Zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 29

*(Ibara Iliyotajwa hapo juu Ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 30

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki cha 30 kuna maelezo yanayomhusu mtoaji wa fedha za *electronic* aliyepewa leseni. Sasa yapo mambo pale ya kufanya. Mimi sipunguzi kitu lakini nataka kuongeza kitu katika kifungu hiki kwamba, ni kuongeza *paragraph* (e) itasomeka kwamba "*to provide a receipt equivalent to cash deposited or issued to a consumer or customer*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba hizi stakabadhi za kuwa huyu mtu ambaye anafanya hii miamala awe na kitu cha kumlinda kwamba hizi *message* hizi zinaweza zikafutika zinaweza zikapata matatizo kwa hivyo awe na *document* ya kuonesha kwamba ametuma idadi ya fedha fulani, hasa pale anapomtumia mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa sababu hizi simu tumeona kwamba unaweza ukarusha kwa nambari hii, akapokea mwingine, na kuna mambo kidogo, kwa hiyo *message* zinaweza zikafutika kwenye simu, mtu awe na stakabadhi ambayo itamhakikishia kwamba *message* ikifutika au kumetokea fedha hazikufika kulikokusudiwa, aweze kusema kwamba nilituma kwa wakala fulani, wakala namba fulani na stakabadhi hii ndio ushahidi huu. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Yaani hata wewe Waziri unaweza kujibu, ninyi wote mnaweza kujibu, hata wewe unaweza kujibu Profesa!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nadhani suala hili la utoaji wa risiti ni suala la msingi na tumelisisitiza hapa, lazima risiti ziwe zinatolewa. *In actual fact* tunasisitiza biashara zote ni lazima hizo risiti ziwe zinatolewa.

Kwa hiyo, tukiliweka hapa, kwa sababu kuna sheria yake ya *electronic transaction* yenyewe inapokuja, tunaomba tulichukue kule *rather than* kwenye kuliweka hapa, kwa sababu hii itakuwa tunabana zaidi katika mfumo mmoja, lakini hilo ni suala la msingi na tutaliangalia katika *electronic transaction* itakapokuja.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mahali pake sahihi ni hapa, ukivisoma vile vifungu vilivyoko katika Ibara ya 30 vya (a), (b), na (c) utakuta hapa ndipo mahali sahihi.

Sheria hiyo inayokuja anayoizungumzia Mheshimiwa Waziri itahusiana sana sana na wizi na mambo mengine yanayofanyika, lakini hapa utakuta ni sahihi kwamba hawa *service providers* wa mambo haya itakuwa wana-*issue* hizi risiti, na upande mmoja ndio sehemu ambayo Serikali inapata kuhakiki. Sasa kama wanasisitiza *receipt* sehemu nyingine, halafu wakaikataa hapa ambapo ndiyo mahali hasa, wala haipunguzi maana yoyote katika Ibara hii ya 30, lakini imezindisha tu majukumu kwa hawa *service providers* ambao wanashughulika na hii miamala ya kifedha.

Kwa hiyo, sioni kwa nini Waziri au Serikali ikatae kuongeza jambo hili ambalo watu wengi wanapata matatizo mambo haya ya simu meseji zile kufutika. Hii ni *document* ambayo mtu atakuwa nayo, stakabadhi ambayo itamsaidia *in case* kukitokezea matatizo yoyote. Kwa hiyo, haibadilishi maana, isipokuwa inajenga vizuri maana na inaongeza nguvu katika Muswada wa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kuna vitu viwili hapa inabidi tuweke vizuri. Hapa tunazungumza *National Payment System*, lakini Muswada unaokuja Jumatatu utazungumzia biashara mtandao na utaekeleza mambo haya yote kwenye Muswada huo.

**MWENYEKITI:** Nadhani Mheshimiwa *Engineer* tukubaliane hapo, siku hiyo tuangalie hilo suala kama linaingia.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niulize kitu kimoja na labda wanijibu kitu kimoja. Katika miamala hii na sheria hii, haitamhusu wakala huyu wa mitaani, hawa wakala wa huku, itahusiana na makampuni ya simu tu, wakala haimgusi? Leseni hizi hazihusiana na huyu wakala wa kawaida? Ikiwa haitahusiana na sheria hii na wakala huyu wa kawaida, nakubaliana na maelezo ya Profesa Mbarawa kwamba katika hiyo ndiyo iwemo. Lakini ikiwa wakala huyu wa kawaida hivi sasa inamhusu sheria hii kama alivyotajwa katika vipengele vya 47 na vingine vile, basi na hapa ndipo anapohusika.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inahusu mifumo ya malipo, wakala aliyepo mtaani tayari anakuwa ni wakala katika mfumo mzima wa malipo. Kwa mfano, kuna wakala wa M-pesa mtaani lakini *owner* wake ni ni nani, ni yule *VODACOM*.

Kwa hiyo, wale ambao wana-*operate* hizi *systems* ndio tunataka hizi sheria ziwe zina-*comply* na wao. Lakini haziondoshi, *again* tunasema, haziondoshi mtu kudai *receipt* akapewa *receipt* yake hata ya maandishi, na ndiyo maana nasema wakati tutakapokuja na sheria yake, itaweza kuelezea kwa sahihi zaidi hizo *transaction* ambazo zinafanyika.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 31

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge ZimaPamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila ya Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 34
Ibara ya 35

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Yaani hata kama kuna homa ya uchaguzi, mnashindwa hata kuitikia. *(Kicheko)*

Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 41

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 42

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 43

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuzingatia uendeshaji bora wa vikao, nakubaliana na mapendekezo ya Serikali.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 44

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 45

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

Ibara ya 46

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 47

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nakubaliana na marekebisho ya Serikali.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki nataka kiongezwe kifungu kingine (c) ambacho kitampa dhamana huyu anayetoa huduma za kibenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kifungu hiki ni kwamba, kuna hii miamala ambayo zinatumika kadi mbalimbali, *MasterCard, Gold, Visa Card*. Ukweli unapotoa hizi kadi, kwa mfano, kama hiki kitambulisho cha Taifa, huku nyuma ukikisoma kina maelezo kwamba kitambulisho hiki ni mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, huruhusiwi kukifanyia mabadiliko ya aina yoyote wala kumpatia mtu ambaye haruhusiwi kukitumia.

Kama kikipotea au kikiharibiwa taarifa kamili lazima itolewe Kituo cha Polisi na ofisi ya *NIDA*, kwa maana kwamba vitambulisho hivi vikitolewa *NIDA* unaweza kuona kwamba yule *owner* hasa ni *NIDA*. Kwa maana hiyo na hizi kadi za kutolea fedha *ATM owner* hasa ni ile benki iliyokupa ile kadi, kingepaswa pia kuwa na maelezo haya ya nyuma. Lakini hiki ndiyo kinachohifadhi siri zako, akaunti namba yako au namba zako na mambo yaliyomo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichoongeza hapa katika kifungu hiki cha 47 ni kwamba hii umekwenda mkoani, umeingiza, aidha kwa ubovu wa mashine au kwa kosa lolote ikatumbukia ndani, huipatani tena na wewe msafiri. Sasa wajibu wa kuirejesha ukaipata mwenyewe ni ile benki yako inayohusika ambayo ina mawasiliano na ile *ATM*, ndiyo maana ya kifungu hiki kwamba wao ndiyo wawe dhamana, asiachiwe *customer* au mteja kwamba yeye tena apate gharama ya kusafiri ya kufanya vipi ya kufuatilia jambo hili, haya mabenki yabebe dhamana hiyo, iwe miongoni mwa sheria, ndiyo maana ya kifungu hiki na nadhani hiki hakina ubishi na Waziri atakikubali, haina matatizo yoyote. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, analosema Mheshimiwa Mnyaa ndiyo utaratibu wa kawaida wa *bank operations* kama *ATM* yako imeingia ndani. Kwa sababu *ATM Card* inachukuliwa kwa mambo mengi, inaweza ikawa kwamba labda kwa mfano, ukienda pale ukaombwa *password* mara tatu, ukitumbukiza mara ya kwanza ikakosewa, ukitumbukiza mara ya pili ukikosea, ukitumbukiza mara ya tatu inaliwa. Sasa maana yake ni kwamba kama ikiliwa ile *ATM* yako…

**MWENYEKITI:** Inaliwa au inatumbukia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Inamezwa…

**MWENYEKITI:** Inamezwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Inamezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachosema ni kwamba ikimezwa ile kadi sasa inabaki mawasiliano baina ya wewe na benki yako. Mara nyingi kadi ikimezwa kwa sababu moja au nyingine, benki haitokupa kadi ile ile tena, itakuambia basi tutaku-*issue* kadi nyingine, na ndiyo utaratibu wa sasa. Kwa hiyo, ile itaondoka itakuwa *destroyed,* wataku-*issue* kadi nyingine na most *likely* hutoambiwa wewe uifuate huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi wao wenyewe watakuambia kwa nini hiyo kadi imemezwa, wala huna haja ya kuwaambia wewe. Kwa hiyo, utapewa hiyo kadi sehemu ambayo tena mara nyingi wewe mwenyewe ndiyo utasema niko Arusha, nileteeni *branch* ya *NMB* Arusha, watakuletea huko.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo, inaonekana Serikali imeshakubali. Na kwa kuwa haijajatajwa katika sheria hii na hapa ndiyo mahali pake penye kutunza siri ya miamala na nini, kwa hiyo, sasa iwepo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna kesi ya kupotea ukiwa ndani ya nchi, kuna kesi ya kupotea au ya kutumbukia kwenye mashine ukiwa nje ya nchi. Kwa hiyo, sasa tuiweke ili benki ijue ni dhamana yake kwa utaratibu. Kufanya kazi *business as usually* hii haitakuwa na maana, sasa tuiweke na Naibu Waziri ameishakubali kwamba ni utaratibu wa kawaida, sasa tuuweke kisheria pia. Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema nimekubali siyo kwamba sasa ndiyo aweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema ni kwamba haina haja ya kuwepo hapa kwenye sheria hii *principle legislation* kwa maana ya kwamba *ATM* ikiliwa au ikimezwa, basi lazima uende kwenye kituo chako, kama ilimezwa Biharamulo ukachukulie sijui wapi. Huwezi kuweka mambo hayo kwenye sheria. Hiyo ni haki yako kama mteja na imo kwenye maeneo mengine kwamba benki zitatoa huduma kwa mujibu wa makubaliano na kadhalika. Hayo yanaingia kwenye kanuni na taratibu na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo jambo halina nafasi hiyo. Ukishasema *protection of customer information* na unasema kadi yako ina taarifa zote hizo, ikishamezwa mle ndani mlinzi wa ile kadi sasa haiwezi kuchukuliwa hata na mtu yeyote, mlinzi wa ile kadi ni benki yenyewe ambayo tayari ina *information* yako, *anyway!*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa anachosema yeye kifungu hiki kina *deal* na *protection of customer information*. Sasa kadi yako ikishamezwa mle ndani mwenye dhamana ya *protection of customer information* ni benki yako na siyo lazima ile *customer information* benki iitoe kupitia kadi, inaweza ikatoka kwa njia nyingine na ndiyo maana tukasema dhamana ya *customer information* kwa hapa haihusu kadi tu inahusu mambo mengine mengi ambayo ujumla sheria inasema benki na taasisi nyingine yoyote ya fedha au taasisi yoyote inayotoa huduma kama hii iwe ina dhamana ya kulinda *information* yako ambayo ni *privilege information.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer,* mnasema kitu kimoja naomba tukubaliane.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema kitu kimoja, lakini tofauti yake wanakataa kuiweka hapa. Sasa ukisoma kifungu cha 47 bila kuathiri sheria nyingine yoyote, mtota huduma wa mfumo wa malipo atalinda usiri wa taarifa za mshiriki na taarifa za mteja wa mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi benki wanaofanya kazi ni binadamu, kuna wafanyakazi wengine wanakuwa *involved* na matatizo chungu nzima sote tunayajua. Sasa, imeingia kwenye mashine, yuko mfanyakazi ambaye atakwenda kuichukua mle. Zile siri yeye akiitumia vibaya je? Lakini benki ikilazimika kisheria kiutaratibu ndiyo utaweka *condition* vizuri kwa hawa watendaji ambao siyo waaminifu na hapa ndiyo sehemu yake tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongelea kitu kimoja, lakini tatizo dogo wao kuiweka ikawa *commitment* za benki ndiyo wanachokataa sijui wanakataa nini wanalinda nini! Kwa sababu hii inasaidia hawa Watanzania wako unaotaka upate kodi juu yao. Sasa kwa nini wanakataa sijui! *Almost* tunaongea kitu kimoja, lakini kwa nini isiweke, ndiyo siwalewi nini sasa.

**MWENYEKITI:** Mimi pia nadhani tusilivute sana hili suala. Benki zinataka biashara, wewe unataka kadi yako, kwa nini mtu akae na kadi yako na huwezi kuchukua benki nyingine isipokuwa benki yako ama tawi lako. *It is automatic* jamani tusibishane bila sababu.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 48

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nimeleta marekebisho kwenye Ibara ya 48, nikiomba neno au maneno "haraka iwezekanavyo" au "*immediately*" yaondoke. Yabadilishwe na "*within forty eight hour au* saa 48".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi…

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, nenda taratibu, kwa sababu tunarekebisha sheria, unaenda kifungu gani, unabadilisha wapi..

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Ibara ya 48 ambayo inasomeka hivi "*a payment* system..., kwanza, kwenye *marginal note* inaelezea "*time of effects to transfer of funds or customers account*". Katika hiyo ibara inasomeka; "*a payment system provider upon receipt of funds in the settlement account in receipt of its customer shall immediately transfer the funds to the customer's account*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo neno *immediately* ndilo ambalo lina ukakasi, kwa sababu ukiangalia na nimesoma *Guidelines, Rules and Regulations* ambazo zinasema ni *only two hour*. Na tunajua kama *provider* ameishapata hela anatakiwa ampelekee mteja, ni kwa nini kusiweke *fixed time* ili huyu mteja aweze kupata hela zake kwa wakati? Kwa sababu unaposema *immediately,* ni neno ambalo ni *very relative, immediately according to who?* Kwa sababu huyo *provider* anaweza akakaa nazo zaidi hata ya wiki moja.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana Serikali ituambie ni muda gani *specific* ili mteja awe na uhakika hela yake atalipwa lini?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru na tuna-*appreciate concern* ya Mheshimiwa Susan Lyimo. Labda mantiki mazima ya kuweka *immediately, immediately* maana yake ni haraka zaidi, na sasa hapa tunazungumzia kuhusiana na mifumo ya malipo.

Mifumo inatofautiana, kuna mengine inaweza ikachukua kweli siku moja na *it is very valid* kwamba siku moja, mbili. Lakini je, kama tukiiweka suala la saa, kuna mifumo ambayo tunaweza tuka-*transfer in a second,* mtu ameishapata pesa zake. Sasa tutasababisha tukiweka saa hapa, basi kampuni maadamu tumeweka *leeway* la *48 hours,* anaweza akachukua hata hizo *48 hours,* wakati ambapo kitu kilitakiwa kifanyike hapo hapo *in a matter of seconds*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaweka hii *simply* kwa sababu hii tunazungumzia kuhusiana na mifumo tofauti, *ECH,* mifumo ya *TISS* ambapo saa nyingine inawezekana kukawa na matatizo, lakini *all in all* tunaweka hapa kwa sababu tunaona teknolojia inaruhusu mifumo hii kufanya *transaction* kwa haraka zaidi.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema na mimi nimesoma ni mifumo tofauti. Lakini hata kama ni *two minutes*, hata kama ni *five minutes, it is within 48 hours.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa maana hiyo nazungumzia wawe na *fixed time,* walau wawe *within* huo muda, kwa sababu wengine wanaweza wakaa na fedha za mteja na wakazifanyia biashara, kwa hiyo, anaweza akakaa hata mwezi amekaa na fedha za mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo suala langu hilo, nilikuwa nasema walau kuwe na *fixed time 48 hours* kwa sababu kama Waziri anavyosema ni kweli kuna mifumo ina muda mfupi, je, atuambie basi, hiyo mifumo ambayo ina muda wa juu zaidi ni muda gani ili walau hawa *service providers* waweze kukidhi mahitaji ya wateja. Kwa sababu wateja wanakuwa na kazi hizo fedha, lakini tayari zimechukuliwa zinafanya biashara.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wasiwasi wa Mheshimiwa Lyimo, lakini akisoma Ibara ndogo ya (2) ile imeeleza kwamba benki itatoa. Kwa Kiingereza wanasema *the bank shall prescribe the specific time of effecting transfer of the funds on customers account with respect to the payment system time.* Hivi ilivyo ime-*take care of concern* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *sub section (3)* pia kama anataka kufanyia biashara kwa maana hiyo anayosema Mheshimiwa Lyimo, ni kosa la jinai liko pale, kwa hiyo, atachukuliwa hatua na kuadhibiwa *accordingly*. Kwa hiyo, kadri tunavyo-*develop,* halafu ambavyo pia tume-*improve system* zetu za *payment,* kutakuwa kuna mabadiliko. Kwa hiyo, tuiachie tu benki ina-*regulate* zile *time specifically as we go on,* kama tukifikia hatua unaweza *within a second* kama anavyosema Mheshimiwa Waziri, *you are done and then* hatuna haja ya kuiweka hivi. Naomba kushauri kifungu hiki kibaki kama ambavyo kilivyo kwenye sheria.

**MWENYEKITI:** Jamani hizi ni biashara zao na ndiyo wanaishi hapa. Hivi hata ukisema 48 *hours,* sidhani kama ni… yaani *it doesn't sound,* hata tunavyo-*fit* hapa hai-*fit* tu. Naomba kifungu kifikiwe kama kilivyo hapa.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Mabadiliko Yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan, *immediately* ni lugha nzuri na kwamba inampa *room* hata yeye mwenyewe ahangaike, ni biashara. Tuendelee!

Ibara ya 49

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 49, marekebisho yangu ni kwamba hawa *TCRA* wahusishwe katika mambo haya kwa sababu hapa imezungumzwa kwa madhumuni ya kufanya uchunguzi, ukaguzi na usimamizi, chini ya sheria hii benki inaweza kuidhinisha maafisa wake kwa maandishi.

Sasa, nilichotaka tu kwamba "*bank in collaboration with Tanzania Communication Regulatory Authority,* iongezwe hivyo kwamba hawa wanajibu na wana utaalam. Kwa hiyo, haya makampuni ya simu kuna baadhi ya mambo wanaweza wakayafanya, pengine benki tu bila ya kutumia utaalam wa haya makampuni ya simu wasielewe, lakini ukitumia makampuni ya simu inakuwa hawana ujanja. Kwa hiyo, ningeomba tu *TCRA* wahusishwe hapa ikiwa Benki Kuu wataona wapate msaada wa hapa yaani waweze kuhusishwa itajwe kisheria. Ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi, lakini tukikiacha chenyewe kama kilivyo tunampa Benki Kuu afanye mawasiliano *not only with TCRA* lakini katika *institution* yoyote *for the purpose* ya ku-*conduct investigation* atakwenda. Anaweza akafika Polisi, anaweza kufika katika taasisi nyingine na nyingine. Tukimfunga hapa tutakuwa tunasema tu kwamba…, yaani tuna *focus* tu makampuni ya simu, *we are dealing with payment systems* na siyo makampuni ya simu hapa. Kwa hiyo, tumuachie Benki Kuu aweze kufanya *investigation,* akiwa anahitaji aende katika taasisi yoyote ambayo yeye mwenyewe anaona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Mnyaa?

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nimekubali!

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Marekebisho Yoyote)*

Ibara ya 50

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 51

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ndiyo pale ambapo pana mambo ya *Gaming Act,* panapohusiana na mambo ya bahati nasibu. Mimi nilichotaka hapa ni kuingiza hiki kifungu mara tu baada ya *sub clause (2)* kwamba, "*notwithstanding the provision of sub clause (1) it is hereby prohibited for communication companies to subscribe their customers automatically to the gaming activities after they have recharged airtime*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba, huu mtindi wa kutumia *recharging* halafu mteja akaingizwa moja kwa moja kwenye bahati nasibu kunatofautiana na imani za watu. Kwa hiyo, bahati nasibu ziwe mbali, anayetaka kucheza bahati nasibu acheze bahati, na ku-*recharge* simu yako isiingize mambo ya bahati nasibu. Kwa hiyo, hapa makampuni ya simu yatofautishe, yawe na sheria ya kutofautisha mambo hayo. Hivi sasa mtindo wanaoendelea nao unawakwaza watu wengine. Nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutakumbuka Mheshimiwa Waziri, Profesa Mbalawa alipokuwa akichangia alieleza kwamba Jumatatu

*Inshallah* kuna Miswada inakuja; *Electronic Transactions Bill* na *Cybercrimes Control Bill,* hapa ndipo mahala pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama utakapoona katika *scheme* nzima ya sheria hii huoni hata sehemu moja neno *Telecommunications Company* limetumika. Sasa kwenye sheria hiyo sasa ndiyo tutayaweka yale, na kweli kama anavyosema yanaudhi, kwenye simu zetu wanaleta *message,* wanatu-*charge* hata sisi hatujazihitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nashauri kwamba, ibara hivi kama jinsi ilivyo kwenye sheria hii ibaki hivi na mapendekezo ya Mheshimiwa Mnyaa yatazingatiwa kwenye sheria zinazokuja.

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshakiri katika Kamati yako hii maalum, Kamati ya Bunge Zima au Bunge hili, kwa hiyo mimi sina tatizo ikiwa sheria hii italelwa na mambo haya ya-*stop* sasa. Kwa hiyo, sina tatizo kwamba Serikali imeshaji-*commit* wataileta wataingiza katika sheria inayokuja, *fine, thank you* sina tatizo.

**MWENYEKITI:** Na wewe uwe macho siku hiyo sheria ikija.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Marekebisho Yoyote)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Marekebisho Yoyote)*

Ibara ya 56

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo langu halikuwa kwenye kifungu hicho kwenye upande wa Kingereza, tafsiri ya Kingereza isipokuwa ilikuwa kwenye tafsiri ya Kiswahili ambapo najua wengi tunasoma Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama utaniruhusu ni kwamba ukiangalia tafsiri katika Kiswahili na Kingereza zina tofauti kubwa. Utaona kwamba Ibara 56(1)(2)(3) kwenye Kingereza lakini kwenye Kiswahili kuna kifungu cha (1) na cha (2). Kwa hiyo, nilikuwa nimeleta marekebisho ili kile kifungu cha (2) ambacho hakikutafsiriwa kwa Kiswahili kiwepo. Kwa hiyo hayo ndiyo yalikuwa marekebisho. Kwa maana hiyo kifungu hicho kingekuwa cha pili 56(2) ambacho kingesomeka "bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Gavana wa Benki atatunga Kanuni katika maeneo yafuatayo, ambayo hiyo itakuwa iko baada ya namba 56(1). Nadhani umenielewa.

**MWENYEKITI:** Mmemuelewa Mheshimiwa? Hamjamuelewa? Yeye amesoma zote, ya Kingereza na Kiswahili, akaona ya Kiswahili ina maelezo ambayo kwenye Kingereza hayapo, kwa hiyo, angetaka hayo yaingie huko. Mheshimiwa *AG,* kimo humo humo ndani, iko kule nyuma kwenye Kiswahili. Hebu tuambieni nini mantinki? Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali mapendekezo ya Mheshimiwa Susan Lyimo na hiki kifungu sasa kitatafsiriwa.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 57

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Hapo hapo kwenye kifungu namba 57 pana *typing error* ambayo tulikuwa tumesema tunaiomba irekebishwe. Badala ya pale kwenye 57(2) *after expiry of 6 month following the date of commencement of this Act, commit an offence and is liable on conviction to a fine of not less than "five one hundred"* ni makosa ni *"not less than One Hundred Million Shillings"* ile "*five*" inaondoka pale haipo ni *typing error* na kuna marekebisho yamekuja katika hili.

**MWENYEKITI:** Mbona inasema *defendant is liable on conviction to a fine not exceeding one hundred million shillings.* Ndiyo unasema nini wewe?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Kwenye hii ya kwanza ambayo wengi wanatumia inasomeka "*five one hundred*".

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, inatakiwa isomekeje?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** *One Hundred* ile *Five* ni kosa ambalo baadae limekuja na karatasi nyingine imechelewa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, *a fine* siyo *fine*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** *Of not less than One Hundred* hii *five* inaondoka kabisa.

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu Kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Pamoja na Marekebisho Yake)*

Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60

*(Vifungu Vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima Bila Marekebisho Yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

***Muswada wa Sheria ya Mfumo ya Malipo ya Taifa wa Mwaka 2015 (The National Payment Systems Bill, 2015)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria wa Mifumo ya Malipo ya Taifa ya mwaka, 2015 (*The National Payment Systems Bill, 2015*) kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na marekebisho yake. Naomba kutoa hoja kwamba Muswada huo sasa ukubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosema, hili ni jambo kubwa ambalo limefanywa na Serikali, lakini kwa sababu ya mabadiliko mengi katika mifumo hii, angalau muendelee kufuatilia kila wakati. Ni kweli kabisa ni nchi peke yake sasa hivi, tutakuja kuaibika Watanzania. Unaenda mahali unaulizwa *"do you have a credit card*?" Unasema hauna, unaanza kutoa maburungutu yako, haiji, haiji jamani!

Waheshimiwa Wabunge, hebu tubadilike kabisa, kwa sababu tunafanya kazi na watu wengine, ni aibu sana! Kuna nchi nyingine ukishakuwa na maburungutu haya, wanakuambia wewe unatembea na *money,* ni *money laundering*. Kwa hiyo, mu-*improve* na tunaomba Mheshimiwa Waziri na *system* zako tufanye kama wengine wanavyofanya.

Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir!

**MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Namjua alikuwa anaitwa Vicky, kwa hiyo ndiyo maana nashindwa kutamka jina lake.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Kwegyir! *(Kicheko)*

**MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE**

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana kunipa nafasi hii adhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo binafsi kwa mjibu wa Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013 inayotamka wazi kuwa, "Mbunge yeyote anaweza kwa idhini ya Spika kutoa Maelezo Binafsi Bungeni yanayolenga kufafanua kuhusu jambo lolote linalomhusu na lililoifikia jamii".

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum mwenye Ulemavu wa Ngozi ninayewakilisha watu Wenye Ulemavu kwenye hili Bunge lako Tukufu. Aidha, mimi ni miongoni mwa Wahanga wanaojihami dhidi ya watu makatili wanaosaka viungo vya walemavu wa ngozi kwa kutukata mikono na miguu yetu pamoja na kuwauwa kabisa katika maeneo ya Kanda ya Ziwa na Mikoa Jirani kutokana na imani potofu za kishirikina bila ya kujali utu wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kukithiri kwa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi, nimeona ni vyema nilete maelezo binafsi, mbele ya Bunge lako tukufu ili Bunge liweze kuelewa na kulitolea tamko jambo hili baya na linaloitia aibu nchi yetu kitaifa na kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako naomba Serikali kupitia vyombo mbalimbali vinavyohusika na upelelezi wa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi kuhakikisha upelelezi wa kesi zinazouhusu mauaji au ukataji wa viungo wa watu wenye ulemavu wa ngozi ufanyike kwa haraka ili kuondoa shaka iliyojengeka miongoni mwetu sisi watu wenye ulemavu wa ngozi

kwa kudhani kuwa Serikali inapuuzia au kudharau ufuatiliaji na upelelezi wa kesi hizo kwa sababu kumekuwa na ukimya sana kila baada ya matukio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama, nashauri Bunge lako kuziomba Mahakama zinazoshughulika na kesi hizi zilizokamilisha upelelezi wa mauaji au ukatwaji wa viungo kwa watu wenye ulemavu, kuziendesha kesi hizo upesi na kutoa hukumu kwa uwazi zaidi. *(Makofi)*

Aidha, ikiwezekana kesi hizo zifanyike mbele ya macho ya jamii ili adhabu itakayotolewa iwe fundisho kwa wale wote wanaotamani au kudhani kuwa kupata viungo vya watu wenye ulemavu wa ngozi vinaweza kuwasaidia kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia Bunge lako kupitia upya sheria za mauaji zilizopo kwa sasa, ikiwezekana zirekebishwe ili kumlinda zaidi mlemavu mara anapofanyiwa ukatili wa namna hiyo na pia itolewe adhabu kali zaidi na kuwahukumu kwa namna ya kipekee kabisa wale wote watakaokutwa na hatia ya kuua watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, makofi haya yanaashiria kwamba wote wanakubaliana na maneno uliyosema. Lakini kwa kweli inasikitisha sana na hii ni tabia ya watu wasioendelea tu. Mtu unaacha kufanya kazi kihalali ukifikiria mwili wa mwenzako utakufanyia utajiri. Ni mambo ya watu ambao hawajaendelea na ni fikra finyu kabisa. Halafu utamkuta mtu mwenyewe anayehangaika hivyo basi yeye ndiyo kabisa afya yake ni mbaya zaidi kuliko kiwango, sijui kwa nini hawajiulizi hivyo.

Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, sisi tuna wajibu pia wa kuyaona haya na kuyakemea kila wakati kadri inavyostahili na mapendekezo aliyoweka Mheshimiwa nadhani Serikali wameyapokea na wote tufanye kama ni *operation,* ifike mahali tunaacha kuendelea na tabia hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, hatuna kazi nyingine, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho Saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.36 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 24 Machi, 2015 Saa Tatu Asubuhi)*